

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Sitini – Tarehe 28 Juni, 2021

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Tatu na kikao chetu cha leo ni cha sitini; bado vikao viwili tu tufunge Mkutano wetu Tatu. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KWASILISHA MEZANI

SPIKA: Hati za Kuwasilisha Mezani, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo.

MHE. EDWIN E. SWALLE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni tarehe 9 Februari, 2021 kwenye Mkutano wa Pili wa Bunge.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Swalle kwa niaba ya Kamati ya Sheria Ndogo. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Tunaanza na TAMISEMI Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same.

Na. 499

Ahadi ya Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Same

MHE. DKT. DAVID M. DAVID aliuliza:-

Wananchi wa Wilaya ya Same bado wanaendelea kutaabika sana kwa kukosa huduma bora za afya kwenye Hospitali ya Wilaya licha ya ahadi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa ya ujenzi wa hospitali mpya ya Halmashauri ya Wilaya ya Same.

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa ikizingatiwa kuwa eneo la ujenzi wa hospitali hiyo tayari limeshatengwa?

SPIKA: Majibu ya uhakika kuhusu Hospitali ya Wilaya ya Same, Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI - Dkt. Festo Dugange, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Jimbo la Same Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kujenga na kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya nchini zikiwemo Hospitali za Halmashauri. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga shilingi bilioni 55.7 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Hospitali 68 za Halmashauri zilizoanza kujengwa katika mwaka wa fedha 2018/2019. Pia Serikali imetenga

shilingi bilioni 11.4 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Hospitali 27 za Halmashauri zilizoanza kujengwa katika mwaka wa fedha 2019/2020 na shilingi bilioni 14 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali 28 za Halmashauri katika Halmashauri 28 ambazo hazikuwa na Hospitali za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa Hospitali kongwe 43 za Halmashauri ambazo zina uchakavu wa miundombinu ikiwemo Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Same. Kupitia Programu ya Ujenzi na Ukarabati wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya nchini; Hospitali hizo zitaanza kujengwa upya kwa awamu kuanzia mwaka wa fedha 2022/2023. Ahsante.

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Mathayo David.

MHE. DKT. DAVID M. DAVID: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kunipa nafasi hii lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kutupa majibu yenyewe matumaini kwa Jimbo la Same Magharibi na Wilaya nzima ya Same, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa hii ni ahadi ya Waziri Mkuu kujenga Hospitali ya Wilaya ya Same na kwa kuwa Hospitali ya Wilaya ya Same ipo katika barabara kuu inayokwenda Arusha ambapo ajali nyingi sana zinatokea na watu wote wanaopata matatizo haya wanategemea kupata huduma katika Hospitali ya Wilaya ya Same na kwa kuwa eneo limeshatengwa kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Same.

Je, Serikali inapoanza kujenga hospitali mpya 43; Wilaya ya Same itapewa kipaumbele ili iweze kujengwa hospitali na kuletwa vifaa tiba pamoja na wafanyakazi wa kutosha?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa Sera ya Serikali ni kuwa na zahanati angalau kwa kila kijiji na kituo cha afya kila kata; na kwa kuwa katika Jimbo langu tumejenga zahanati za kutosha takribani asilimia 80 lakini hatuna wafanyakazi na hatuna vitendea kazi.

Je, Serikali ni lini itapeleka watumishi wa afya kwenye zahanati hizo ili tuache kuzifunga zianze kutumika kusaidia wananchi wa Wilaya ya Same?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili muhimu kwa watu wa Same. Mheshimiwa Naibu Waziri - TAMISEMI tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa David Mathayo David kwa juhudzi zake za kuhakikisha mara kwa mara anawasiliana na Serikali kuhakikisha Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Same inajengwa; na mimi nimuhakikishie Serikali itaendelea kushirikiana naye lakini na wananchi wa Same kuhakikisha katika vipaumbele hivi tunakwenda kujenga Hospitali ya Wilaya ili kuboresha huduma za afya kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, hii ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, na kama ilivyo ada ahadi za viongozi wetu wa Kitaifa zinapewa kipaumbele; na mimi naomba nimuhakikishie kwamba Serikali tayari imeshaainisha ahadi zote za kitaifa za viongozi wetu wa kitaifa na zinakwenda kufanyiwa kazi kwa awamu na hospitali hii ya Same ikiwemo.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, ni kweli tuna sera ya zahanati katika vijiji na vituo vya afya katika kata, lakini tumeamua kufanya mapitio ya sera ile ili tuwe na ujenzi wa zahanati kimkakati zaidi, lakini pia ujenzi wa vituo vya afya kimkakati zaidi badala ya kuwa kila kijiji na kila kata. Lakini nimuhakikishie vituo hivi vyote ambayo vimejengwa Serikali inaendelea kuajiri na watumishi hao 2,726 walioajiriwa wapo ambao watapelekwa Same na katika awamu nyingine za ajira tutahakikisha tunapeleka watumishi Same. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Nilikuona Mheshimiwa Jackson Kiswaga.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wa Kijiji cha Magulilwa, Kata ya Magulilwa, Jimbo la Kalenga walishamaliza boma la kituo cha afya siku nyingi sana; je, ni lini Serikali itatukamilishia ujenzi wa boma hilo? Ahsante.

SPIKA: Sina hakika kama Naibu Waziri analifahamu hilo boma. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri - TAMISEMI; inabidi uyajue maboma yote nchi hii. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jackson Kiswaga, Mbunge wa Kalenga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ilikiwemo boma hili la Magulilwa la kituo cha afya na maboma mengine yote ya vituo vya afya na zahanati, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumefanya tathmini na kuorodhesha maboma yote na mpaka tarehe 31 Mei, 2021 tulikuwa na jumla ya maboma 8,003 ambayo tunayapa kipaumbele cha kutenga fedha kwa awamu ili yakamilike. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba boma hili la Magulilwa litapewa kipaumbele. Ahsante.

SPIKA: Bado tupo TAMISEMI Waheshimiwa, swali linalofuata ni la Mheshimiwa Nicodemas Maganga. Mheshimiwa Nico.

Na. 500

Hitaji la Vifaa Tiba Katika Hospitali Mpya Nchini

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka vifaa tiba ikiwemo *x-ray* pamoja na vifaa vingine vya kupima wagonjwa katika hospitali zilizojengwa hivi karibuni hasa katika Wilaya mpya ikwemo Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Daktari.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais -TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mbunge wa Jimbo la Mbogwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imetoa shilingi billioni 34 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika Hospitali 67 za Halmashauri zilizoanza kujengwa katika mwaka wa fedha 2018/2019. Fedha hizo zimepelekwa Bohari Kuu ya Dawa na utaratibu za kupeleka vifaa tiba katika Hospitali 67 zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali ilipatia Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe Shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali mpya ya Halmashuari.

Aidha, mwezi Mei, 2021 Serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Hospitali ambapo majengo mapya matano yamejengwa na yameyakamilika. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga shilingi milioni 300 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Hospitali na shilingi milioni 487 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika Hospitali ya Wilaya ya Mbogwe. Ahsante.

SPIKA: Watu wa Mbogwe wameridhika, tunaendelea na Wizara ya Maji. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo.

Na. 501

Kuongeza Kina cha Bwawa la Maji la Lukuledi-Masasi

MHE. AGNES E. HOKORORO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusafisha na kuongeza kina cha Bwawa la Maji Lukuledi-Masasi linalohudumia Vijiji vya Lukuledi, Nambawala, Mraushi, Mwangawaleo na Ndomoni?

SPIKA: Majibu ya swalii hilo, Mheshimiwa Waziri wa Maji mwenyewe. Mheshimiwa Aweso, tafadhalii.

WAZIRI WA MAJI alijibuu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jukumu la Serikali ni kuhakikisha maeneo mbalimbali yanapata huduma ya maji ya uhakika na kipaumbele ni maji kwa matumizi ya nyumbani ambapo Vijiji vya Lukuledi, Ndomoni na Nambawala vinapata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza.

Katika mwaka wa fedha 2021/2022 kazi ya ujenzi wa miundombini ya kufikisha maji Kijiji cha Mraushi pamoja na Kitongoji cha Mwangawaleo, utekelezaji unaendelea ambapo utahusisha ulazaji wa bomba lenye urefu wa kilometra sita, vituo vya kuchotea maji 16 na ujenzi wa tanki la lita 100,000 kuongeza upatikanaji wa maji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Vijiji vya Lukuledi, Nambawala, Mraushi na Ndomoni wanatumia maji ya Bwawa la Lukuledi. Hivyo, kutokana na umuhimu huo katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali itakamilisha usanifu na kuanza ukarabati wa bwawa hilo ili liwe na uwezo wa

kuhifadhi maji mengi ya kukidhi mahitaji ya shughuli hizo za maendeleo.

SPIKA: Mheshimiwa Agnes Hokororo swalii la nyongeza.

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza nashukuru kwa majibu mazuri yenyewe matumaini yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri kwa wananchi wa maeneo ambayo walikuwa na shida kubwa ya maji, lakini pamoja ma majibu hayo mazuri naomba kuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba kwa kuwa katika Kata za Mpanyani, Namatutwe, Msikisi, Namajani ambao pia Nambawala ipo katika Kata ya Mpanyani, wananchi hawa hawajawahi kuona maji salama kwa maana ya mabomba na naomba kuuliza; je, Serikali ina mpanga gani wa kuharakisha uchimbaji wa mabwawa katika kata hizo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, katika Kijiji cha Mraushi na vitongoji vyake ambapo katika majibu ya msingi Serikali imethibitisha kwamba ujenzi wa mradi wa kuwapatia maji wananchi hao umeanza kwa bajeti ya mwaka 2021/2022. Ni lini mradi huo utakamilika ambapo pia nina uhakika Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuambatana na mimi kwenda kujionea kadhia ya hali ya maji katika maeneo hayo?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso Waziri wa Maji, tafadhali.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nimpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake mkubwa na si mara moja amekuja katika Wizara yetu ya Maji kuhakikisha wananchi wake kuwa wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, kwanza nilishukuru sana Bunge lako Tukufu sisi Wizara ya Maji kutuidhinishia zaidi ya shilingi

bilioni 680. Lakini kwa namna ya kipekee Mheshimiwa Rais kwa dhamira yake njema ya kuhakikisha kwamba anakwenda kumtua mwana mama ndoo kichwani ametupatia fedha ya nyongeza zaidi ya shilingi bilioni 207; hajjawahi kutokea; nataka nimuhakikishie fedha zile moja ya mipango ni kuhakikisha kwamba tunakwenda kununua vitendea kazi kwa maana ya magari ya kisasa kwa ajili ya ujengaji wa mabwawa pamoja na uchimbaji wa visima. Kata zake alizoainisha tutakwenda kuzipa kipaumbele katika kuhakikisha kwamba tunakwenda kutatua tatizo la maji. Ahsante sana.

SPIKA: Nilikuona Mchungaji Innocent Bilakwate.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwenye Wilaya ya Kyerwa kuna mradi wa vijiji 57, mradi huu Serikali imesema utajengwa kwa awamu, lakini kwenye bajeti kuna Kata ya Kikukulu, Kata ya Songembele, Kichwechwemkula na Rukaija havikuwekwa bajeti. Nini kauli ya Serikali juu ya kata hizi ambazo hazikuwekwa kwenye bajeti? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Waziri wa Maji - Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, tafadhalii.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpungeze Mheshimiwa Mbunge kaka yangu Bilakwate kwa namna anavyopigania jimbo lake la Kyerwa, kubwa ambalo nataka nimuhakikishie mkakati wa Wizara yetu ya Maji ni kuhakikisha tunatumia vyanzo toshelevu ikiwemo Mto Kagera.

Sasa moja ya vijiji ambavyo vingi tunakwenda kutatua tatizo la maji zaidi ya 50. Tumesema mradi huu tunakwenda kuutekeleza kwa awamu, kata ambazo hazipo katika bajeti hii tutahakikisha bajeti ijayo tunaziweka ili kuhakikisha kwamba wananchi wake wanaweza kupata huduma hii muhimu ya maji. Ahsante sana.

SPIKA: Bado tupo Wizara ya Maji swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa.

Na. 502

Hitaji la Maji Vwawa – Songwe

MHE. JAPHET N. HASUNGA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo la maji katika Mji wa Vwawa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri lini Vwawa itapata maji, tafadhalii.

WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya maji ya Mji Vwawa ni zaidi ya lita milioni 10 kwa siku ambapo kwa sasa hali ya upatikanaji wa huduma ya maji ni asilimia 43.2.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mipango ya muda mfupi na muda mrefu ili kuboresha huduma ya maji safi na salama katika Mji wa Vwawa ambapo katika mpango wa muda mfupi mwaka 2020/2021, Wizara imechimba visima virefu vitatu yenyewe uwezo wa kuzalisha maji lita 600,000 kwa siku. Ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji ya visima hivyo utafanyika ndani ya mwaka wa fedha 2021/2022 na kuongeza huduma ya upatikanaji wa maji kwa wakazi wa Mji wa Vwawa kufikia asilimia 70.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa muda mrefu wa kuboresha huduma maji safi, salama na yenyewe kutosheleza kwa wakati wa mji huo Serikali imepanga kujenga mradi kuititia chanzo cha maji cha Mto Bupigu uliopo Wilaya ya Ileje wenye uwezo wa kuzalisha maji kiasi cha lita milioni

73 kwa siku. Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kufanya Usanifu wa Kina yaani *detailed design* wa mradi huu anatarajiwa kupatikana katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/2022 mradi huu utanufaisha Miji ya Vwawa, Mlowo na Tunduma katika Mkoa wa Songwe.

SPIKA: Mheshimiwa Hasunga nilikuona, swali la nyongeza.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri na jitihada za Serikali ambazo imefanya. Nashukuru kwa mpango wa muda mrefu, lakini mpango wa muda mrefu utachukua muda mrefu, sasa kwa mpango wa muda mfupi pale kwenye Mto Mantengu pale Vwawa; iwapo mnaweza kufunga *pump* mbili zenyenye uwezo wa kusukuma maji tunaweza tukapunguza upungufu wa maji katika Mji wa Vwawa kwa kiwango kikubwa.

Sasa je, ni lini Serikali itakuwa na mpango wa kufunga *pump* mbili kubwa za kuweza kusukuma maji katika katika Mto Mantengu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Rais wa Awamu ya Tano alipotembelea Mji wa Vwawa mwaka 2019 alitoa shilingi milioni 100 na ndio zikaenda kuchimba visima vitatu katika eneo la Ilolo, *Old Vwawa* na Nailhanda. Lakini visima hivyo vilitelekezwa mpaka leo bado havijafunga miundombinu.

Sasa je, Mheshimiwa Waziri utakuwa tayari kuambatana na mimi baada ya kipindi hiki cha Bunge ili twende tukaangalie hali halisi na tutatue changamoto ya muda mrefu ya wananchi wa Mji wa Vwawa? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, kuhusu maji Vwawa tafadhalii Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ukimuona mtu mzima analia ujue kuna jambo. Sasa nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge maji hayana mbadala na kwa kuwa

tukiweka ama tukifunga *pump* mbili wananchi wako wanakwenda kupata maji toshelevu, nikuombe baada ya saa Saba tukutane tutoe fedha kuhakikisha kwamba *pump* zile zinapatikana na wananchi wako wanapata huduma ya maji safi na salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini swalii la pili, nipo tayari kuongozana na wewe Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha kwamba tunakwenda kukulindia jimbo lako la Vwawa. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana hayo ndiyo majibu yanayoridhisha wananchi. Nakuona Mheshimiwa Sophia Mwakagenda swalii la nyongeza. (*Makofi*)

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Wilaya ya Rungwe katika Kijiji cha Masukulu kumekuwa na shida sana ya maji japokuwa Serikali ilipeleka fedha. Je, hamuoni kuna haja ya kutuongezea fedha ili maji yaweze kuenea katika vijiji vinavyozunguka Kata ya Masukulu?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri majibu, hata Rungwe nako kuna shida ya maji? Majibu tafadhalii.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, lakini kubwa ambalo nataka nimuhakikishie, Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan, dhamira yake kumtoa mwana mama ndoo kichwani, kwa hiyo sisi tupo tayari kutoa fedha kuhakikisha wananchi wako wa Masukulu wanapata huduma ya maji sasa.

SPIKA: Mheshimiwa Neema Mgaya nilikuona, swalii la mwisho la nyongeza.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Spika ahsante kwa kunipa nafasi, Wilaya ya Wanging'ombe kuna Mradi wa Maji wa Igando - Kijombe wa shilingi bilioni 12 ultakiwa uwe

ushakamilika tangu mwaka 2019 lakini hadi sasa hakuna kitu kinachoendelea. Nilitaka kujua lini Serikali itakamilisha mradi huu?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji natumaini unaujua mradi huo wa maji wa Wanging'ombe, majibu tafadhali.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, sawa na nataka niseme tu unatosha mpaka chenji inabaki, lakini kubwa ambacho ninachotaka kuhakikisha utekelezaji wa miradi ya maji inategemeana na fedha, sasa sisi tumeshapatiwa fedha kuhakikisha kwamba tunakamilisha miradi mbali mbali, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaupa nguvu mradi wake, kuhakikisha tunapeleka fedha kwa wakati, ili mradi ukamilike na wananchi waweze kupata huduma maji safi na salama.

SPIKA: swali la Mheshimiwa Mbunge wa Kilolo kuelekea Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Justin Nyamoga.

Na. 503

Ujenzi wa Barabara ya Iringa Mjini - Kilolo

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya kutoka Iringa Mjini hadi Kilolo ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer Godfrey Kasekenya Msongwe*, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Iringa Mjini hadi Kilolo yenye urefu wa kilometra 33.6 ni sehemu ya barabara ya Iringa iliyoanzia Ipogolo – Idete yenye urefu wa kilometra 67.7 ambayo ni barabara ya Mkoa inayosimamiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara nchini (*TANROADS*). Kilometra 9.9 za barabara hiyo ni za lami na kilometra 23.7 nyingine ni za changarawe.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara ya Iringa Mjini hadi Kilolo, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara nchini (*TANROADS*) ilikamilisha Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hiyo mwaka 2009. Kwa sasa ujenzi wa kilometra 10 kwa kiwango cha lami kati ya kilometra 23.7 za changarawe unaendelea huku marejeo ya usanifu wa mwaka 2009 yakiendelea.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa kilometra 13.7 zilizosalia kadri ya upatikanaji wa fedha. Aidha, Serikali itaendelea kuifanya matengenezo mbalimbali barabara yote kutoka Iringa Mjini hadi Idete kuhakikisha kuwa inapitika vipindi vyote vya mwaka, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Kilolo uliza swali lako la nyongeza.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Spika ahsante sana, kwanza nishukuru sana kwamba wakati wa kuchangia Mpango nilielezea kutokurudhishwa kuhusu mkandarasi aliyekuwa anaweka ile lami ya kilometra 10 na amebadiliswa na *speed* yake sasa yule anaeendelea kwa kweli ni nzuri na inaridhisha.

Sasa maswali yangu, kwa sababu ukiangalia kuna *Project* ya *World Bank* ambayo barabara hii kilometra zote 33.6 zilikuwemo na ninafahamu kwamba Waziri wa Fedha

alisaini mkataba na hawa watu wa *World Bank* kwa ajili ya hiyo *project*. Je, upatikanaji wa fedha hizo utaondoa huo ujenzi wa awamu na kufanya barabara hii iweze kujengwa yote na kukamilika?

Mheshimiwa Spika, swalil pili; je, Waziri atakuwa tayari kuambatana pamoja na mimi kwenda kuangalia hasa maeneo ya milimani kwa barabara hii ambayo hayapitiki ili tuweze kupata ufumbuzi na wananchi waweze kupita vizuri?

SPIKA: Mheshimiwa Nyamoga milimani ambako hakupitiki umpeleke Waziri atapandaje huko. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi - *Engineer Godfrey Kasekenya Msongwe*, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru kwa kutambua jitihada za Serikali na kwamba ni sikivu, alichokiomba tumeshakitekeleza kama Wizara. Pia nimpongeze kwa kuwapigania sana watu wa Kilolo kuhusu hii barabara, sasa majibu yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema kwamba Waziri wa Fedha amesha saini mkataba huu na labda tu nielezee kwamba mkataba huu unafadhiliwa na Benki ya Dunia ambao umechukua muda kutokana na ukweli kwamba mradi huu ulikuwa una *cover mikoa michache*, kwa hiyo Serikali iliona huu mradi utanuliwe, pia ulikuwa unalenga sana barabara za changarawe, kwa hiyo, Serikali ikaona hatuwezi tukachukua fedha *World Bank* kwa ajili ya changarawe, kwa hiyo, kukawa na majadiliano ili kuuboresha, kwanza uchukue mikoa mingi pia uwe ni kwa kiwango cha lami ambapo ni barabara za kutoka vijijini kuunganisha na barabara za mikoa na barabara kuu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo baada ya kusaini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii kilometra zote 33 zipo kwenye mpango, na zitajengwa ndio maana tunafanya *design* upya kuhuisha ile *design* iliyokuwepo ili iendani na kiwango cha sasa cha barabara.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mimi Mheshimiwa Mbunge nimhakikishie kwamba nipo tayari kuambatana naye kwa ajili ya kwenda kuangalia hizi barabara na kuhakiki jinsi ujenzi unavyoendelea, ahsante.

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Mbunge wa Liwale, uliza swali la nyongeza.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Iko barabara ya kiuchumi barabara ya ukombozi kwa Wilaya ya Liwale, barabara ya Nangurukuru - Liwale. Barabara hii bajeti ya mwaka jana ilitengewa fedha kwa ajili ya kufanyiwa upembuzi yakini na usanifu wa kina, na mwaka huu pia imetengwa kwenye kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Wana Liwale wangetaka kusikia, ni lini barabara hii itakwisha kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, na hatimaye kujengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo fupi la nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zuberi Kuchauka Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti tuliyopanga, tunauhakikia tutakamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara yote, lakini pia katika maeneo yale kofoi, tumemuagazi Meneja wa TANROADS ayape kipaumbele ili kuhakikisha kwamba yanatengenezwa vizuri ili yasiathiri kupita kipindi kile cha masika, ahsante.

SPIKA: Ahsante, bado tupo Ujenzi na Uchukuzi, swali linaulizwa na Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 504

Kukarabati Kipande cha Reli ya Kati Manyoni – Singida

MHE. NUSRAT S. HANJE aliuliza:-

(a) Je, kwa nini kipande cha reli ya kati kutoka Manyoni hadi Singida hakipo kwenye mpango wa ukarabati?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kukarabati kipande hicho cha reli ili kusaidia kuchochea ukuaji wa uchumi wa mkoa wa Singida?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kuititia Shirika la Reli Tanzania (*TRC*) inaendelea na mpango wa ukarabati wa mtandao wa reli iliyopo na kufufua njia za reli zilizofungwa kwa awamu kwa kuanzia na njia kuu (*main line*). Katika kutekeleza jukumu hilo, Serikali inazingatia Mpango wa Miaka Mitano wa Taifa ambao unaanzia 2021/2022 – 2025/2026. Aidha, Serikali itaendelea na ukarabati wa matawi ya reli ikiwemo kipande cha reli kutoka Manyoni hadi Singida kulingana na mahitaji ya ukuajiwa uchumi na uwezo wa kifedha. Lengo la Serikali ni kuboresha miundombinu ya reli ili kurahisisha huduma za uchukuzi nchini.

Mheshimiwa Spika, sehemu (b); Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo na miundombinu ya reli imara katika kuchochaea uchumi wa nchi. Hata hivyo, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi sehemu (a), Serikali itaendelea kufungua njia zote zilizokuwa zimefungwa ikiwa ni mkakati wake wa kurejesha huduma za usafiri wa reli wenyewe uhakika nchini na kuchochaea ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali kupitia *TRC* imepanga kufanya tathmini kwa ajili ya ufunguaji wa njia zilizokuwa zimefungwa kwa lengo la kujua gharama za ukarabati. Maeneo ya reli yatakayohusika ni pamoja na Kilosa – Kidatu na Manyoni – Singida. Hivyo, naomba Mheshimiwa Mbunge aelewewe kwamba Serikali inafanya kazi eneo la reli Manyoni – Singida, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Nusrat ameridhika, uliza swali la nyongeza.

MHE. NUSRAT SH. HANJE: Mheshimiwa Spika ahsante, pamoja na majibu Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Mkoa wa Singida ni mkoa muhimu sana pamoja na Mkoa wa Dodoma na Simiyu katika uchumi wa nchi, kwa sababu inatambulika kwamba Singida sasa hivi ni *pilot* kwenye zao la alizeti mahususi kwa ajili ya nchi, kwa hiyo pamoja na jibu lake kwamba mwaka 2022/2023 kwamba ndio ataweka kwenye mpango.

Je, Wizara haioni umuhimu wa kutafakari upya jambo hili kulinganisha na umuhimu wa Mkoa wa Singida kwa sasa kwenye bajeti ya mwaka huu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mkoa wa Singida kwenye miundombinu ya barabara bado kuna changamoto sana. Je, Wizara ina mpago gani wa kuhakikisha kwamba inaunganisha Mkoa wa Singida kwa barabara za lami ili kuhakikisha kwamba wakulima wa alizeti na vitunguu wanafikiwa mpaka kwenye vijiji vyao? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Waitara, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba nifanyiwa mswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge Nusrat kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nifanyiwa marekebisho huu mwaka unasomeka 2021/2022; maana yake kuanzia Julai tathmini inafanyika tuweze kupata gharama ili tulipishe eneo la kipande cha reli ambacho kimetajwa.

Sehemu ya pili; Mheshimiwa Mbunge amesema kuunganisha barabara hizi za lami kwenye eneo lake Mkao wake wa Singida, ni kweli kwamba tunao utaratibu mzuri wa kila Mkao, kwa maana Meneja wa TANROADS Mkao anapaswa kuratibu zoezi la barabara katika Mkao wake husika. Sasa tupokee hoja yako kama kuna eneo ambalo halipitiki kabisa kwa sasa, nielekeze Meneja wa TANROADS wa Mkao wa Singida afanyie kazi kama kuna sehemu ya kuchukua dharura tufanye hivyo ili kufanya maboresho kwa wakulima wa alizeti, vitunguu na maeneo mengine wapate huduma nzuri ya usafiri, ahsante.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Mtaturu.

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Spika, nakushkuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni miundombuni ya reli ni muhimu sana katika usafirishaji wa mizigo pamoja na abiria, na kwa sababu reli hii ilianzishwa na Baba wa Taifa; Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kumuenzi Baba wa Taifa kwa kuifanya haraka kuijenga reli hii na iweze kutumika?

SPIKA: Majibu Mheshimiwa Naibi Waziri, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtaturu, Mbunge kutoka Mkao wa Singida kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba Serikali inatambua umuhimu wa reli hii, kama alivyosema imeasisiwa na Baba wa Taifa, na tukifanya tathmini ya kujua gharama tutaiboresha reli hii. Hii reli iliopo ni ya zamani itabadilishwa tuweke iwe kubwa zaidi iweze kubeba mzigo mkubwa Zaidi.

Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge tupe muda mwaka huu mpaka mwakani utapata majibu ya ujenzi wa reli Singida – Manyoni na maeneo mengine.

SPIKA: Bado tupo Singida Waheshimwia Wabunge, swali linauzwa na Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhan wa Singida Kaskazini kwa Wizara ya Nishati.

Na. 505

**Kupeleka umeme katika vijiji na kata ambazo hazina
umeme Singida Kaskazini**

MHE. ABEID R. IGHONDÖ aliuliza:-

Je, ni lini Vijiji na Kata katika Jimbo la Singida Kaskazini ambavyo havijapata umeme vitapata umeme?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Naibu Waziri Nishati, Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhan, Mbunge wa Singida Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vijiji 26 vya Jimbo la Singida Kaskazini ambavyo havijapata umeme kati ya vijiji 84 vitapelekewa umeme kupitia utekelezaji wa Mradi wa REA Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili ulioanza mwezi Machi, 2021. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Desemba, 2021 na gharama ya mradi ni shilingi bilioni 26.6.

SPIKA: Mheshimiwa Ighondo, swali la nyongeza.

MHE. ABEID R. IGHONDO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba niulize mswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, kuna baadhi ya vijiji ambavyo vimeachwa katika huu mkakati ambao sasa unaenda kutekelezeka wa vijiji hivi 29, mathalani Vijiji vya Sagara, Itaja, Kinyamwenda, Mwighanji, Itamka, Endesh, Sefunga, Namrama havijaonekana.

Sasa Serikali inampangao gani kuhakikisha vile vijiji vyote vilivyoachwa vionekane sasa katika ramani ili navyo vinufaika na mradi huu?

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ambayo yameshapatiwa umeme, kuna vitongoji vikubwa vyenye hadhi ya kijiji na taasisi za umma kama vile shule na zahanati, lakini umeme umeishia pale tu *center*, na hapo hapo kuna maeneo ambayo tayari walishafanya na *wiring* waliagizwa wafanye *wiring* na umeme haujafika.

Sasa ningependa kujuu Serikali ina mpango gani kuhakikisha maeneo yale ambayo ni makubwa yana hadhi ya kijiji nayo yapatiwe umeme? Naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili Naibu Waziri Nishati - Mheshimiwa Byabato, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abeid, Mbunge wa Singida Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna vijiji ambavyo vilionekana vimebakı katika kuchukuliwa kwa awamu ya tatu mzunguko wa pili wa *REA*, na amevitaja vijiji sita, vijiji vitatu vya Endesh kinyamwenda na Endesh nyengine viko katika mradi wa *backbone* ambao unatoka Iringa kwenda kupeleka umeme mpaka Namanga, kwa hiyo ule mradi mkubwa umechukua vijiji vitatu ambavyo tutavipatia umeme. Mkoा wa Singida una vijiji saba ambavyo tumeviweka kwenye ule mradi, vijiji vitatu viko Singida Kaskazini na vitaingia kwenye huo mradi na vitachukuliwa na vitapatiwa umeme kufikia mwishoni mwa mwezi Julai.

Mheshimiwa Spika, vijiji vyengine vitatu vinavyobakia vimechukuliwa katika hivyo 26; kama tulivyosema hapo awali kwamba kuna maeneo ambayo yalikuwa yamebaki na takriban vijiji 680 vyote yameingizwa kwenye *REA* Awamu ya Tatu mzinguko wa pili, na yote yatafanyiwa kazi kwa pamoja ili inapofika Disemba 2022 vijiji vyote Tanzania Bara viwe vimepata umeme.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la pili ni kweli kwamba kuna maeneo yetu ya vitongoji bado hayajapata umeme, na kama ambayo tunavyokuwa tukisema maendeleo ni hatua taratibu tunawafikia, tulanza kwenye vijiji na tunamaliza Disemba mwakani, kwenye vitongoji tunaendelea kufika na *speed* yetu ni nzuri na tunamini kwamba muda kabla haujawa mrefu sana, kila kitongoji kitakuwa kimepatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, kwenye vitongoji *TANESCO* ni jukumu lao la kila siku wanaendelea kupeleke kwenye maeneo yetu, na *REA* Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili unapoingia kijijini utafika pia kwenye vitongoji na pia miradi yetu mingine ikiwemo *densification* ambayo tunatarajia ianze mwezi wa 10 itachukua walau sehemu ya vitongoji ili zoezi

hilo la kupeleka umeme kwenye vitongoji liweze kukamilika na wananchi waweze kupata umeme, ahsante.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Mbunge wa Manyoni Magharibi, uulize swalii la nyongeza.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa dhamira ya Serikali ni kupeleka umeme katika vijiji vyote katika nchi ya Tanzania nzima ikiwemo na vitongoji, lakini kuna changamoto katika Wilaya ya Manyoni feederya Manyoni kutoka Singida ambayo inahusisha Wilaya ya Ikungi, Wilaya ya Manyoni na Halmashauri ya Itigi, umeme wake una katikakatika mara kwa mara, na ipo dhamira njema ya Serikali ya kujenga vituo vya kupozaa umeme katika Mkoa wa Singida vipo vitatu ikiwepo Manyoni, Mitundu katika Jimbo langu na Iramba; je, ni lini ujenzi wa vituo hivi unaanza?

SPIKA: Majibu ya swalii hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa mgunge wa Singida kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba yapo baadhi ya maeneo ambayo umeme wake unakuwa haufiki vizuri kwa sababu ya laini kuwa ni ndefu, lakini Mkoa wetu wa Singida ni mkoa mmojawapo wenye kituo kikubwa sana cha kupoza umeme pale mjini, na umeme unatokea pale kuelekea maeneo ya jirani, na tunao umeme wa kutosha kuweza kuhudumia maeneo yote. Ni kweli tunatarajia kuweka vituo vyengine vya kupoza umeme katika maeneo yetu ya Singida, mchakato wa kutafuta wazabuni na maeneo sahihi ya kuweka unaendelea, kabla ya mwaka huu haujaisha Waheshimiwa Wabunge wataona maendeleo katika maeneo yao na ikiwemo kwenye Jimbo lake ambapo tunatarajia kuweka kituo cha kupoza umeme kwa ajili ya

kuweza kusambaza umeme kwa karibu zaidi katika maeneo yake.

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa uliza swali lako la nyungeza.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto kubwa katika Mkoa wa Manyara ya upandishwaji wa gharama za umeme kutoka kwa wananchi kutoka *unit zero* mpaka kupelekwa *unit one*. Changamoto hiyo imetokea wananchi walikuwa wanalipa umeme wa shilingi 5,000 wanapata *unit 41*, na kwa sasa hivi wananchi wakinunua umeme shilingi 5,000 wanapata umeme *unit 14*; na Wilaya zilizoathirika ni Wilaya za Hanang, Mbulu, Babati, Simanjiro kwa ujumla wake mkoa mzima wa Manyara.

Nini kauli ya Serikali juu ya kuwapa umeme kwa bei ya kawaida wananchi wa Manyara ili waweze kujiinua kiuchumi na wasilale giza? Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Majibu ya swali hilo Naibu Waziri Nishati, Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge wa Taifa Vijana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba gharama za umeme ziko juu hata hizo zinazosemwa ni ndogo sisi bado tunaziona ziko juu. Nia ya Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha umeme unakuwa wa gharama nafuu na kila mmoja anaweza kuupata kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi pia na ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, *tariff* tunazozitumia sasa zilitengenezwa mwaka 2016 na *EWURA* ndiyo msimamizi wa gharama za utoaji wa umeme kwa watu mbalimbali. Sasa

naomba nieleze kinachotokea; zile *tariff*, ile kanuni ya gharama inasema mtu anayetumia *unit* sifuri mpaka *unit* 75 atakuwa-*charged* shilingi 100 kwa *unit* moja, yule anayetumia zaidi ya *unit* 75 na kuendelea gharama zake ni shilingi 200 hadi 350 kulingana na yuko kwenye *tariff I*, *tariff II* au *tariff III*.

Sasa kuna kifungu kwenye kanuni ile kiliwekwa kwamba wananchi wote wanaotumia umeme wakiwa maeneo ya vijijini wapate gharama hiyo ya *unit* moja shilingi moja na wanaozidi 75 waendelee kwingine. Wale ambao sio wa maeneo ya vijijini hawapati nafuu ya punguzo hilo la gharama.

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya kuona kwamba kanuni hizo zilitengenezwa kipindi ambacho kulikuwa na shida sana ya upatikanaji wa umeme wa gharama nafuu kwa maana ya kutumia mafuta mazito na mitambo mingine, lakini sasa tuanzalisha umeme kutoka kwenye maji ambako ni nafuu, tunayo gesi yetu ya kutosha kabisa kwa ajili ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana na wenzetu wa *TANESCO*, wakae chini, wa-review hizo gharama za kuuza umeme ili tuweze kupata umeme mwangi zaidi na tukauza kwa gharama ndogo.

Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Asia pamoja na Waheshimiwa wengine watuvumilie kidogo, tuko katika mapitio mazuri kabisa ya kushusha gharama za kuuza umeme na kila mmoja atapata gharama hiyo ya umeme nzuri kabisa kwa ajili ya maendeleo kwenye maeneo yetu ya mijini na maeneo ya vijijini ili ile nia ya uwekezaji ambayo Mheshimiwa Rais anaitaka kwa Watanzania wote iweze kufikiwa kwa kila mmoja. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Bado tuko Nishati, Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kwa niaba yake.

Na. 506

Mwendelezo wa Miradi ya Gesi Nchini

MHE. TUNZA I. MALAPO K.n.y. MHE. SHAMSIA A. MTAMBA aliuliza:-

Serikali ilikuwa na mpango mzuri juu ya uwepo wa nishati ya gesi asilia nchini, lakini mpaka sasa kumekuwa na sintofahamu juu ya mwendelezo wa uwekezaji wa miradi hiyo ikiwemo gesi ya Mkoa wa Mtwara.

Je, nini kauli ya Serikali juu ya mwendelezo wa miradi hii nchini?

SPIKA: Majibu ya swali hilo la watu wa Mtwara, Naibu Waziri wa Nishati, bado tupo kwako.

NAIBU WAZIRI NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba Mbunge wa Mtwara Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (*TPDC*) inaendelea na uwekezaji katika sekta ya rasilimali ya gesi nchini kuanzia shughuli za utafutaji, uchorongaji na uendelezaji wa shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa takribani mikataba 11 ya utafutaji na uchimbaji wa gesi asilia inaendelea kufanyiwa kazi kati ya makampuni mbalimbali ya uwekezaji kwa ushirikiano na Serikali kupitia *TPDC*. Hadi sasa gesi iliyogunduliwa imefikia futi za ujazo triliioni 57.54. Sehemu ya gesi hii hutumika katika kuzalisha umeme kwa asilimia zaidi ya 50 ya umeme wote nchini, lakini pia viwandani, katika majumba na katika magari.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa gesi hiyo inaendelea kunufaisha Taifa, Serikali inaendelea kutekeleza

mradi mkubwa wa kimkakati wa kuchakata gesi kuwa katika kimiminika (*Liquefied Natural Gas – LNG*) unaotarajiwa kuanza ujenzi ifikapo mwaka 2023. Serikali kupitia tayari imelipa fidia ya shilingi bilioni 5.71. Gharama ya mradi ni dola za Marekani bilioni 30.5. Mradi unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2028.

SPIKA: Mheshimiwa Tunza Malapo uliza swalii lako kuhusu gechi. (*Kicheko*)

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru; mionganii mwa ahadi za uendelezaji wa nishati ya gesi ni pamoja na ujenzi wa kiwanda kikubwa cha mbolea. Naomba nipate ufanuzi wa Serikali ni lini kiwanda hicho kitajengwa katika mkoa wa Mtwara?

Mheshimiwa Spika, swalii langu la pili; sisi watu wa Mtwara kila siku tunaauliza gesi kwa sababu hatuoni ile michakato ambayo tulikuwa tunaiona pale nyuma. Sasa hivi Mtwara habari ya gesi ni kama haipo, kama imelala. Hata Ripoti ya CAG ukiisoma inaeleza kwamba matumizi ya gesi bado yako chini.

Sasa nataka tu kujua kauli ya Serikali; ni nini hasa inafanya ili sisi watu wa Mtwara turidhike kwamba ile gesi iliyogundulika Mtwara inafanya lile ambalo limekusudiwa na kuinua uchumi wa watu wa Mtwara na Taifa kwa ujumla? Nakushukuru. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili muhimu. Kiwanda cha Mbolea na gechi yetu.

NAIBU WAZIRI NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Tunza Malapo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali ilianza majadiliano na wawekezaji wa viwanda vya kutengeneza mbolea kwa kutumia gesi almaarufu kama *petrochemicals*. Hiyo gesi ndiyo malighafi kubwa katika utengenezaji wa hizo mbolea na vitu vya namna hiyo. Sasa kilichotokea ni kwamba

biasara ile ilionekana haikuwa ya kutusaidia na kutufaa kwa kipindi hicho kwa sababu wakati duniani wanataka kununua kwa dola tatu sisi wa kwetu walikuwa ana bei ya chini kabisa ambayo ilionekana haitakuwa faida kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sasa tumefungua upya milango ya majadiliano na wawekezaji mbalimbali wanaotaka kuwekeza katika viwanda kama hivyo akiwemo mwekezaji mkubwa wa Dangote naye ameonesha nia na bado tunaendelea kupokea maombi na majadiliano mbalimbali yanafanyika kuhakikisha kwamba sasa tunaweza kutumia gesi kutengeneza viwanda vya malighafi mbalimbali kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunakoelekea ni kuzuri na viwanda vya *petrochemicals* na vingine vitakuja. Gesi tutaitoa huko iliko na kuitumia kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la pili; ni kweli kwamba kwa muda mrefu kidogo pameonekana kama pamelala kwamba hakuna kilichokuwa kinaendelea. Kimsingi kilichokuwa kinaendelea ni kikubwa kuzidi kilichokuwa kinaonekana. Tunayo mikataba inayoitwa *Production Sharing Agreement (PSA)* ni mikataba ambayo inaingiwa kati ya Serikali na wale wawekezaji wanaokuja kuwekeza katika maeneo yetu ya gesi. Tukikubaliana tutazalishaje, tutagawana vipi na tutatumia vipi.

Mheshimiwa Spika, sasa majadiliano hayo yamechukua muda mrefu na marekebisho na mapitio ya mikataba hiyo imechukua muda mrefu, lakini sasa yamekamilika na tayari Serikali imetoa maelekezo na sasa kinachofanyika ile Kamati ya Serikali ya ku-*negotiate* mikataba imerudi tena kazini na tunatarajia mwezi wa 10 itakuwa imekamilisha kazi yake ya ku-*negotiate* sasa mikataba ya matumizi na unufaikaji wa gesi na tunatarajia kuanzia mwezi wa 11 basi mambo yataanza kuwa vizuri. Gesi hii tunayoitoa na kuitumia sasa itaongezeka zaidi kwa ajili ya manufaa ya nchi kwa ujumla. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Chikota nilikuona umesimama.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nataka kuulizia kwamba mradi wa *LNG* wa Lindi mazungumzo yake yamechukua muda mrefu sana; ni zaidi ya miaka saba na hata wawekezaji wengine ambao wanataka kuwekeza kwenye shughuli za *petrochemicals* wameshakata tamaa. Ni nini sasa kauli ya Serikali kwamba mazungumzo hayo yanatarajija kukamilika?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati tafadhali.

NAIBU WAZIRI NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Chikota kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema majadiliano yalismama ili kupisha mapitio ya mikataba ya uzalishaji wa gesi na sasa majadiliano yameanza tena kuanzia mwezi wa nne na tunatarajia mwezi wa 10 majadiliano hayo yatakuwa yamekamilika na mwekezaji anaweza akaanza kuwekeza muda wowote baada ya hapo.

Mheshimiwa Spika, *LNG* ikitolewa kule tunakwenda mbele zaidi na kuisambaza katika maeneo mengine. Tutajenga vituo vitano vya ku-compress gesi na kuweza kuiiza kwa wananchi Dodoma ikiwa ni mojawapo.

Kwa hiyo, tutaweza kupata gesi asilia tukiwa hapa hapa Dodoma baada ya kukamilisha majadiliano na kuanza kujenga vituo vingine ambapo katika bajeti ya wenzetu wa *TPDC* imetengwa takribani shilingi bilioni 28 kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivyo vitano katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwishoni mwa mwaka huu wataanza kufurahia matumizi ya gesi kwa sehemu kubwa ya nchi yetu.

SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, sasa swali litaulizwa na Mheshimiwa Francis Isack Mttinga, Mbunge wa Iramba Mashariki.

Na. 507

Boma la Kihistoria la Mjerumani - Mkalama

MHE. FRANCIS I. MTINGA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakarabati boma la kihistoria la Mjerumani lililopo Wilayani Mkalama ili liendelee kuweka historia na kumbukumbu kwa vizazi vijavyo na kuzalisha mapato kwa Serikali?

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Isack Mttinga, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Malikale ya mwaka 2008, watu binafsi, Taasisi za Umma na Taasisi za Kidini, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zinaruhusiwa kuhifadhi, kuendeleza na kunufaika na urithi wa malikale.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mambo ya Kale Sura 333 kifungu cha 16 kinazipa mamlaka Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kutunga sheria ndogo ndogo za kutunza na kuhifadhi maeneo ya malikale katika maeneo yao. Boma la kihistoria lililopo Wilaya ya Mkalama linasimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama. Hivyo, tunaishauri Halmashauri husika kulikarabati na kulihifadhi ili kiwe chanzo cha mapato na Halmashauri iweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, Wizara iko tayari kutoa ushirikiano na miongozo ya namna ya kulikarabati na kulihifadhi boma hilo la kihistoria lililopo Mkalama ili kulindwa kwa mujibu wa Sheria ya Mambo ya Kale. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mtinga nimekuona, swali la nyongeza.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mkalama ni wilaya mpya na ina mapato madogo sana. Naomba tu niseme Wizara itakuwa tayari kulipokea boma hili kama sisi Halmashauri ya Mkalama tutaamua kuwakabidhi ili walikarabati liweze kuleta manufaa kwa nchi na kwa jamii ya Mkalama; swali la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Naibu Waziri atakuwa tayari baada ya Bunge twende naye mpaka Mkalama ili akaone hali halisi ya boma hili na aone umuhimu wake ili aharakishe mchakato wa kulichukua kama tutawakabidhi? Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Francis Mtinga, Mbunge wa Iramba Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Francis Mtinga, amekuwa ni mfuatiliaji sana kwenye eneo hili la kuboresha malikale liliwemo hili boma la historia lilioko katika Wilaya ya Mkalama. Nimpongeze sana na pia niwapongeze wananchi wa Mkalama Iramba Mashariki kwa kuwa na Mbunge mahiri anayefuatilia maeneo haya ya kihistoria ambayo ni mojawapo ya chanzo cha mapato katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa haya maeneo ni maeneo muhimu kwa ajili ya kuhamasisha utalii lakini pia kuongeza mapato katika sekta zetu hizi, nimuahidi kwamba tutaenda kulitembelea

lakini pia kama Halmashauri itashindwa kulikarabati boma hili basi Wizara iko tayari kulipokea na kulikarabati na liwe eneo mojawapo ya chanzo cha mapato katika Serikali, ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Esther Matiko, uliza swali la nyongeza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, ahsante; Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ni mtu ambaye anaheshimika Tanzania na duniani kote na kwa kufanya hivyo kule Butiama ni sehemu ambayo amezaliwa lakini pia ni sehemu ambayo amezikwa.

Je, ni kwa nini sasa Serikali haioni umuhimu wa kuboresha maeneo yale ya Hayati ili pawe ni *historical site* ambapo ataelezea kila kitu ili tuweze kupata watalii wengi na kuongeza mapato kama vile ilivyo kwa mwenzetu Hayati Mandela wa Afrika Kusini ambapo watu wengi wanakwenda wanamimika kuweza kujifunza zaidi? (*Makof*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Naibu Waziri Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mary Francis Masanja.

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali ina maeneo mengi ya kihistoria, lakini tuna eneo muhimu la kumbukumbu ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere lililoko kule Butiama. Serikali ina mpango wa kuanzisha utalii wa Kiswahili, tuanita *Swahili Tourism* ambayo kwenye maeneo haya yenye kumbukumbu tutaanzisha *Swahili Tourism* iwe ni motisha; mtalii anapofika kwenye maeneo hayo basi kwanza atajifunza Kiswahili lakini atasimuliwa historia na kumbukumbu ya waasisi wetu walikuwaje na walifanya nini na ukizingatia kwamba Mwalimu Nyerere alikuwa ni mmojawapo wa waasisi wa kuboresha lugha yetu hii ya Kiswahili.

Nimhakikishie tu Mbunge kwamba eneo hili ni la muhimu na Mbunge wa eneo hilo alishanialika kwenda kule kwa ajili ya kuangalia namna ya kuboresha eneo hili ili liwe chanzo cha mapato ya Serikali. Kwa hiyo, niwatoe wasiwasi Wabunge na hata wale wengine amba wana maeneo mengine yenye historia kupitia bajeti hii mliyotupitishia tutahakikisha kwamba maeneo haya tunayasmamia kikamilifu ili kuweza kuboresha sekta yetu hii ya utalii, ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza. Mheshimiwa Ester Bulaya, samahani.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru; sera yetu ya utalii mbali ya kwamba inatuingizia mapato, pia wananchi wanaozunguka maeneo yenye hifadhi pia wananaufaika. Halmashauri ya Mji wa Bunda imezungukwa na mbuga ya Serengeti.

Sasa swali langu, Mheshimiwa Waziri mbali ya kwamba wananchi wanalinda Hifadhi ya Serengeti lakini tembo wanapokuja kwa wananchi kuharibu mazao pamoja na nyumba zao wamekuwa hawalipwi fidia. Kwa mfano, Mcharo wananchi 350, Guta, 403, *Bunda Store*, 86, Kunzugu 65, Nyatwali 51 na Mheshimiwa Waziri nimeshaleta ofisini kwako watu hawa wanadai fidia kwa muda mrefu takriban watu 900. Lini watalipwa fidia yao? (*Makof*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo kwa kuwa tayari limeshafika ofisini kwako Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii tafadhalii.

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimtoe wasiwasi Mbunge. Mbunge wa Jimbo alishawahi kunifuata akanipa orodha ya wanaodai, lakini pia hata ye ye mwenyewe ameshanipa orodha ya wanaodai. Kwa hiyo, tulikubaliana kwamba

nitaenda mimi mwenyewe kuongea na wananchi, lakini wale wote wanaodai nitahakikisha kwamba Serikali imewalipa, lakini pia tutaongea na wananchi waendelee kuwa wahifadhi, maana hao ndiyo wanaotusaidia sisi hata kuhifadhi maeneo yanayozunguka hifadhi, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Tuhamie Mambo ya Ndani ya Nchi Waheshimiwa Wabunge, swali la Mheshimiwa Mohamed Suleiman Omar, Mbunge wa Malindi Mjini.

Na. 508

**Polisi Kutotoza Faini za Papo kwa Papo kwa
Wasiotumia *EFD* Zanzibar**

MHE. MOHAMED SULEIMAN OMAR aliuliza:-

Je, ni kwa nini wananchi wa Tanzania Bara wanatozwa na polisi faini za papo kwa papo kwa kutotumia mashine za *EFD* wakati Polisi wa Zanzibar hawatozi faini za papo kwa papo kwa wananchi wasiotumia mashine hizo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Suleiman Omar, Mbunge wa Jimbo la Malindi kutoka Mkoa wa Mjini Zanzibar kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sheria zinazotawala sekta ya usafiri wa barabarani nchini zipo chini ya mamlaka mbili tofauti huku msimamizi wa sheria zake ni Jeshi la Polisi Tanzania. Kwa upande wa Tanzania Bara sheria inayosimamia masuala ya barabarani ni Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 ya mwaka 1973 iliyorejewa mwaka 2002 na kanuni zake, na kwa upande wa Tanzania Visiwani sheria inayosimamia masuala

ya barabarani ni Sheria ya Usafiri Barabarani Sura ya 7 ya mwaka 2003 na kanuni zake.

Mheshimiwa Spika, sheria zote mbili zinatambua adhabu ya tozo ya papo kwa papo kwa Tanzania Bara kifungu kinachotumika ni cha 95 Sura ya 168 ya 1973 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002 na kanuni namba 30 ya mwaka 2015 na kwa Tanzania Visiwani kifungu kinachotumika ni cha 183 Sura ya 7 ya mwaka 2003 na kanuni namba 64 ya mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti makosa ya usalama barabarani ambayo yanasaababisha ajali zinazoleta vifo, ulemavu, majeraha na uharibifu wa mali. Serikali kupitia Jeshi la Polisi linahimiza sheria na kanuni zilizowekwa zifuatwe kama zilivyoelezwa kwa mamlaka zote zinazosimamia usalama barabarani na usafiri wa barabarani ili kuzuia ajali barabarani zisitokee. Nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Mohamed Suleiman Omar swal la nyongeza

MHE. MOHAMED SULEIMAN OMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza nashukuru majibu ya Serikali kwa kufuatia maswali yangu haya; lakini swal iangu la kwanza katika maswali yangu ya nyongeza kwamba kama kwa mujibu wa majibu aliyonipa Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba inakiri kwamba Mamlaka ya kule Zanzibar pia inayo sheria yake ambayo inatambua hizi sheria za faini za papo kwa papo; je, ni kwa nini Jeshi la Polisi sasa limeshindwa kusimamia sheria hizi za papo kwa papo pale barabarani kwa kutumia hizi mashine za *EFD?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swal la pili kwamba ni lini sasa Wizara ya Mambo ya Ndani itakaa na mamlaka husika za kule Zanzibar ili kuona Jeshi la Polisi zinaanza kutumia mashine hizi na ukizingatia kwamba itapunguza malalamiko ya

wananchi na itapunguza masuala ya rushwa lakini pia itapunguza zile ajali ambazo zitaweza kuepukika? Nashukuru sana. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo mawili tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI: Mheshimiwa Spika, naomba ama napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Malindi Mheshimiwa Mohamed Suleiman Omar maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, je, kwa nini Jeshi la polisi limeshindwa? Jeshi la polisi halijashindwa kusimamia taratibu, kanuni na sheria za usalama barabarani katika hili suala la kutumia mashine hizi hapa kuja Jambo kidogo, Zanzibar kuna mamlaka inaitwa Mamlaka ya Usafirishaji au Mamlaka ya Usalama Barabarani ambayo ina sheria yake sheria namba saba na Bara kuna Baraza la Taifa la kusimamia usalama barabarani ambalo nalo lina sheria yake kama tulivyoeleza, lakini kama hilo halitoshi mamlaka hivi zote zina utaratibu wake na kanuni zake ambazo zinasimamia pamoja na kwamba Jeshi la Polisi ndio muhimili mkubwa ambao unasimamia mamlaka hizi.

Kwa hiyo, haijashindwa kusimamia tatizo liliokuwepo ni changamoto ya sheria kwamba hawa wanasheria yao, wana kanuni yao, hawa wana mamlaka yao pamoja na kwamba Jeshi la polisi ndio hilo. Kwa hiyo jeshi la polisi halijashindwa kusimamia sheria hii.

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili; je, ni lini sasa Serikali hasa kule Zanzibar itaruhusu matumizi ya hizi mashine? Nimwambie tu kwamba kwa kuwa sheria ipo na mamlaka inayosimamia usalama barabarani ipo na sheria yake ipo kikubwa ni kwamba sasa hivi tupo katika harakati za kukamilisha kanuni itakayokuja kusimamia sheria hizi ili sasa hii sheria ya kutumia hizo mashine kwa ajili ya kukinga hizo ajali na mambo mengine zianze kutumika.

Mheshimiwa Spika, kubwa nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge awe na subira kidogo sana ili tumalize hizo kanuni na sheria zianze kutumika kote kote.

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge swalii namba 509 Serikali imeliondoa majibu yake yatakuja wakati mwingine, kwa hiyo huo ndio mwisho wa maswali.

Tunaenda kwenye matangazo mbalimbali sasa, tunao wageni wengi na tunafurahi sana kupata wageni wanaotutembelea, karibuni sana wageni wote.

Waheshimiwa Wabunge, nikianza na wageni kumi wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro - Waziri wa Maliasili na Utalii, ambao wanatoka Arusha na wanaongozwa na Mtanzania wa kwanza kupanda Mlima Everest Ndugu Rawan Dakik. (*Makof*)

Wale wa Arusha naomba msimame, huyu Rawan yupo wapi Rawan ndio wewe? *Okey*, basi ni Mtanzania aliyepanda Mlima Everest ule mlima mrefu kabisa duniani, hongera sana, ahsante sana. Kazi hiyo sio ndogo pevu. (*Makof*)

Wageni 105 wa Mheshimiwa Ummy Nderiananga ambao ni wanafunzi wenyе ulemavu wakiongozwa na Ndugu Gregory Balyomi, naomba msimame, wale wanafunzi wenyе ulemavu, karibuni sana, karibuni sana sana sana karibuni sana wanafunzi tunafurahi sana kuwa nanyi, karibuni sana na tunawapenda. (*Makof*)

Waheshimiwa hili suala la ulemavu hili kuna watu wanafikiria ulemavu uwe ni ule unaoonekana tu, kuna ulemavu mwingine hauonekani Waheshimiwa.

Wageni wawili wa Mheshimiwa Deo Ndejembu Ndugu Kareem Kasongo na Ndugu Patricia Wolinska, karibuni pale mlipo wale kule. (*Makof*)

Wageni 11 wa Mheshimwia Japhet Hasunga, wanafunzi wa kutoka *SUA* wakiongozwa na Ndugu Anna Mtondo, wale wa *SUA* karibuni mlipo maana *gallery* zetu zimejaa sana. (*Makof!*)

Wageni 20 wa Mheshimiwa Edwin Swalle Madiwani kutoa Njombe wakiongozwa na Neema Mbanga. Waheshimiwa wako pale, karibuni sana Waheshimiwa Madiwani bajeti ya mwaka huu imefanya mambo yenu kuwa mazuri, sasa mna uhakika wa kila mwezi mambo yenu ni *mswanu mswanu* na mengine yaliyobaki Waheshimiwa Wabunge wanaendelea kuyapigania kwa kweli mambo yenu yanazidi kuwa mazuri kila kukicha, muishukuru Serikali. (*Makof!*)

Wageni 45 wa Mheshimiwa Justin Nyamoga ambao ni wa Kanisa la KKKT Image wakiongozwa na Saidi Kiyeyeu ambao ni wanakwaya hawa, kwaya ya Image nafikiri hawakupata nafasi watakuja baadaye kidogo. (*Makof!*)

Wageni 67 wa Mheshimiwa David Kihenzile ambao ni wanafunzi wanaosoma vyuo mbalimbali hapa Dodoma wakiongozwa na Ndugu Geofrey Mtasiwa, wale pale, karibuni sana sana sana, karibuni hapa Bungeni wanafunzi mjifunze mambo mbalimbali karibuni sana. (*Makof!*)

Wageni 14 wa Mheshimiwa Edward Olelekaita hawa ni wazee wa Dosidosi hawa majirani zangu wanaongozwa na Mzee Hamza Mgia. Waliotoka Dosidosi, karibuni sana, karibuni sana, sana, sana na Mbunge wenu yupo hapa, natumaini mmemuona alipokaa, karibuni sana majirani. (*Makof!*)

Wageni wa Mheshimiwa Oscar Kikoyo na Mheshimiwa Charles Mwijage ni wanafunzi wa *UDOM* wanaotoka Wilaya ya Muleba Mkoani Kagera wakiongozwa na Melkizedek Kajage, wale *inshomile* wale, hawa *inshomile* kabisa kutoka Muleba karibuni sana mjengoni. (*Makof!*)

Wageni 12 wa Mheshimiwa Nicodemas Maganga ambaao ni wanafunzi wa *UDOM* wakiongozwa na Ndugu Meshack Maganga wale wa kutoka Mbogwe karibuni sana, hata wasukuma mpo *UDOM* kweli ni maendeleo makubwa wanaotoka kule Mbongwe, karibuni sana. (*Kicheko/Makofi*)

Katika wale wageni wa Kiteto yuko mzee mmoja Mzee Sulumbu ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Kiteto zamani karibu sana. Karibu sana Mheshimiwa karibu uone Bunge la sasa, karibu sana tunafurahi na kufarijika sana kuwa nawe karibu sana. (*Makofi*)

Tunaendelea na mgeni wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka Ndugu Habiba Lyengite kutoka Liwale karibu sana, karibu sana Habiba wasalimie sana watu wote kule Makunjiganga ahsante. (*Makofi*)

Wageni sita wa Mheshimiwa Antipas Mgungusi ambaao ni watawa wa Kanisa Katoliki kutoka Miyuji wanaongozwa na *Sister Leocadia Kasindye*, ahsante sana ma-sister kututembelea, muendelee katuombea ahsanteni sana. (*Makofi*)

Wageni 56 wa Mheshimiwa Furaha Matondo ambaao ni familia yake kutoka jijiji Dodoma wakiongozwa na Ndugu Kundi Matondo, karibuni sana tunafurahi kuwa nanyi. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Florent Kyombo mpiga kura wake kutoka kule Nzega Ndugu Witness Festo, karibu Witness. (*Makofi*)

Wageni 55 wa Mheshimiwa Flatei Massay ambaao ni Kamati ya Siasa ya Kata kutoka Mbulu Mkoani Manyara wakiongozwa na Ndugu Gabriel Sumawe. Kamati ya Siasa ya Kata, karibuni sana, sana, sana, karibuni sana. Tunafurahi sana kuwa nanyi, Waheshimiwa Kamati za Siasa ni muhimu. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Aysharose Mattembe ambaao ni viongozi wa Shirikisho la Vyama vyा

Walemavu Mkoani Singida; Ndugu Boniface Kitiku, Ndugu Ramadhani Mrisho na Ndugu Miriam Mkumbo, karibuni sana. (*Makof!*)

Mgeni wa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete rafiki yake kutoka Dar es Salaam Ndugu Azizi Mohamed, karibu sana Azizi yule kule karibu sana. (*Makof!*)

Wageni 14 wa Mheshimiwa Condester Sichalwe ambaao ni wanafunzi wa *UDOM* kutoka Jimbo la Mombasa wakiongozwa na Ndugu Omary Sinyinza. Wale wa Mombasa karibuni sana karibuni sana, sana, sana kwa kweli chuo chetu ya *UDOM* kinawakilisha kweli kweli. (*Makof!*)

Mgeni wa Mheshimiwa Amsabi Mrimi ambaye ni Diwani wa Kata ya Maji Moto Serengeti Ndugu Johannes Masirori, karibu sana Johannes Masirori karibu sana kule ulipo Mheshimiwa Diwani. (*Makof!*)

Wageni nane wa Mheshimiwa Esther Matiko ambaao ni wabunifu wa mitindo kutoka jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Nassibu Shaban karibuni sana, karibuni sana tunafurahi kuwa nanyi, lakini kipekee tunao watoto wa Mheshimiwa Esther Matiko hebu tuwatambue sijui watakuwa wapo wapi asimame kwanza Nicole Mkami, hongera sana Nicole, asimame Nicolson Mkami na asimame Alex Matiko, wanapendeza kweli kweli. (*Makof!*)

Wageni 69 kutoka Chuo cha Mipango hapa Dodoma ambaao wanaongozwa na Ndugu Ponches Medati; Mipango karibuni sana Chuo cha Mipango karibuni sana. (*Makof!*)

Wageni 86 kutoka Shule ya Sekondari ya Kiwanja cha Ndege wakiongozwa na Mwalimu Maseumbo karibuni sana Kiwanja cha Ndege Sekondari, karibuni sana sana sana. (*Makof!*)

Mwisho ni wageni 70 wa Mheshimiwa Stella Ikupa ambaao ni viongozi wa Vyama vyya Watu Wenye Ulemavu kutoka Mikoa yote nchini Tanzania wakiongozwa na Ndugu

Ernest Kimaya, karibuni sana sana sana, karibuni sana hapa Dodoma. (*Makofi*)

Nilalo tangazo maalum linalohusu *Ikupa Trust Fund*, Mheshimiwa Ikupa nakupa dakika mbili bwana hebu litoe mwenyewe tangazo lako. Mheshimiwa Ikupa. (*Makofi*)

MHE. STELLA I. ALEX: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii ya upendeleo na kuniruhusu niweze kulitoa tangazo hili mimi mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, nilipopata nafasi ya kuwa Mbunge niliona kwamba sitoweze kulifikia kundi hili la watu wenyе ulemavu hivyo mwaka 2015 niliweza kuanzisha shirika ambalo linashughulikia masuala ya watu wenyе ulemavu na nimekuwa nikifanya hivyo miaka yote na leo shirika hili limeandaa semina ama mafunzo ya kuweza kutoa uelewa wa masuala ya watu wenyе ulemavu kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kwamba baada ya mafunzo haya basi kila Mheshimiwa Mbunge katika michango yake ama katika maswali basi atawezza kuzungumzia masuala ya watu wenyе ulemavu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante, kwa hiyo mchana pale katika ukumbi wa *St. Gasper Hotel* waheshimiwa Wabunge wote tunaombwa kuhudhuria na masuala ya utawala yamezingatiwa vizuri, na mukutano huo wa pale *St. Gasper* umeandaliwa na *Ikupa Trust Fund*. Sasa mnawenza mkaelewa yaani *Ikupa Trust Fund* yaani kule *St. Gasper*. (*Makofi*)

Lakini pia leo hapa naomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba baada ya kumaliza mambo yetu mchana hapa kuna semina kuhusu mkakati wa utekelezaji wa anuani za makazi (*post code*) hapa nchini, suala la utekelezaji wa *post code* hapa nchini, semina hiyo

itafanyika katika ukumbi wa Pius Msekwa. Semina hiyo itaendeshwa na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kwa hiyo wengine mnaweza mkawa hapo wengine mkaenda *St. Gasper*. Uje Bungeni mambo ni mengi kwa hiyo utaangalia nini cha kufanya. (*Makofi*)

Baada ya matangazo hayo Waheshimiwa kama mnavyojua jana rafiki zetu wa Yanga walifanya Mkutano wao Mkuu tunawapongeza, lakini kipekee kwa kuchagua wadhamini ambao baadhi yetu ni Wabunge wenzenzu. (*Makofi*)

Wadhamini wa klubu pamoja na Mama Fatma Karume, lakini wadhamini wengine atakuwa na Dkt. Mwigulu Nchemba ambaye ni Mbunge mwenzetu, mdhamini anayefuata ni Mheshimiwa Waziri Geoffrey Mwambe, Mbunge mwenzetu; Kepteni Mstaafu George Huruma Mkuchika, lakini pia Mbunge wa Kinondoni Mheshimiwa nani tena huyu jina linataka kunitoka. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Tarimba Abbas. (*Makofi/Kicheko/*)

SPIKA: Eeh, huyo huyo, kwa hiyo, wanne katika watano ni Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hii inaonesha kwamba kwakweli klubu zetu kubwa na wana michezo nchini wanaimani sana na Waheshimiwa Wabunge, kabisa kwa moyo ya dhati ningependa niwapongeze walioteuliwa na niwatakie kila la heri wajitahidi tu kuhakikisha kwamba Yanga inashika hiyo namba mbili ambayo ndio wanahangaikia, maana ndio uwezo wao umeishia hapo kuwa washindi wa pili. (*Makofi/Kicheko*)

Walikuwa na mpango wa kuweka mpira kwapani tarehe 3 Julai, 2021 sasa hata wakiweka kwapani tarehe 3 Julai, 2021 kuna Kigoma napo shughuli iko pale pale, usiyemtaka kaja. Kwa hiyo shughuli kweli kweli safari hii, Ridhiwani tafuta kwa kukimbia rafiki yangu. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kesho kutwa siku ya Jumatano tunamaliza shughuli zetu hapa za Bunge baada ya kipindi cha miezi mitatu kwa kweli kazi kubwa imefanyika, hasa nimesikia kuna Wabunge wanafanya mpango kwamba siku hiyo nitakapohoji wanaoafiki tuahirishe na wasioafiki wao watasema hapana. (*Kicheko*)

Jamani natania, nawakumbusha tu kwamba kesho kutwa tunahitimisha, kwa hiyo, wale wenye madeni madeni ya *guest* huko na nini *hotel/msije* mkamuachia Spika maana yeeye ndio anabaki kulinda mjengo hapa, tu-*clear* madeni na ya dada zangu wa Dodoma hapa madeni yote yaishe kaka zangu. (*Kicheko/Makofi*)

Tunaye mgeni Dkt. Mwinyi Omar Mwinyi pale alipo karibu sana mgeni wetu, ahsante sana ahsante. (*Makofi/Kicheko*)

Katibu!

MHE. HALIMA J. MDEE: Mwongozo wa Spika.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mwongozo wa Spika.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA
ANDOGO KUHUSU UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO
ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA PILI WA BUNGE**

SPIKA: Nimeona miongozo Mheshimiwa Halima Mdee, halafu nani tena Sophia ni hiyo tu miwili. Haya tuanze Halima.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kuititia Kanuni ya 76 kufuatia jambo ambalo limetokea mapema kwenye Mkutano huu wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, unakumbuka wakati wa majadala wa Wizara ya Kilimo hoja ya Stakabadhi Ghalani ilijadiliwa kwa mapana sana na kwa uchungu mkubwa sana na Wabunge wako na nkinukuu majibu ya Wizara ya Kilimo ilitoa kauli kuwa mazao ya soya, dengu, choroko, mbaazi na ufuta hayatakuwa katika mfumo wa Stakabadhi Ghalani isipokuwa mikoa ya Pwani, Lindi, Mtwara na kwa Mkoa wa Ruvuma Stakabadhi Ghalani iliruhusiwa Wilaya ya Namtumbo kutokana na namna ambavyo wao wako *well-coordinated*.

Mheshimiwa Spika, sasa kiti chako kilielekeza kwamba Wizara itoe waraka kule chini kwa ajili ya utekelezaji. Sasa kinachoendelea sasa hivi kwenye mikoa mbalimbali ambayo inalima haya mazao, lakini hususan baadhi ya maeneo ya mkoa wa Ruvuma kumekuwa kuna kero kubwa na usumbufu mkubwa sana. (*Makofii*)

Sasa kwa kuwa kiti chako kilitoa maelekezo, nilikuwa naomba mwongozo wako na kwa sababu Bunge ndiyo linaishia ili mosi, tuweze kujua kama Wizara ilishusha maelekezo kule chini na utekelezaji wa hayo maelekezo ukoje kwa sababu wananchi wanateseka sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. (*Makofii*)

SPIKA: Bahati nzuri Wizara ya Kilimo wapo, Mheshimiwa Naibu Waziri nakuona.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, nashukuru; sisi kama Wizara tumeshatoa *guidance* na tumepeleka Waraka na Mkoa wa Ruvuma mkoaa pekee ambaao umefanya msimamo wa wao kama mkoaa ni mkoaa wa Ruvuma na kusema kwamba wao wanaendelea na Mfumo wa Stakabadhi ya Ghala na leo sisi kama Wizara ya Kilimo tumepeleka watu kwenda kuangalia *situation* iliyoko katika Mkoa wa Ruvuma, timu yetu imeondoka leo kuelekea Mkoa wa Ruvuma ili kuangalia hicho wanachokisema mkoaa wao kama mkoaa hakileti athari kwa wakulima na hakisababishi usumbufu.

Mheshimiwa Spika, lakini bado kama Wizara, zao moja katika mazao yote kwa sababu *situation* iliyoko katika Mkoa wa Ruvuma ni kwamba zao la soya linalimwa wilaya ya Nyasa, lakini Stakabadhi ya Ghala inaenda kuwa *practice* katika Wilaya ya Songea. Kwetu sisi kama Wizara tumeona kwamba hilo siyo sahihi sana ndiyo maana tumepeleka wataalamu waende wakaliangalie na *then* tutatoa *final position* kwa sababu mkoa wenyewe wametuletea taarifa kutuambia kwamba kwa mazingira yao wanadhani kwamba hilo jambo linaweza kutekelezeka. (*Makofî*)

Lakini sisi tumesema wazi kwamba zao kama linalimwa Wilaya A na wakulima wenyewe wanaamua kulifanya kwa Stakabadhi ya Ghala iwe ni *decision* ya wakulima na wala isiwe *decision* ya mtu mwingine ye yote. (*Makofî*)

Kwa hiyo tumepeleka watu na tunaamini mpaka kufikia kesho mchana tutakuwa na majibu kama Wizara juu ya hiyo *position* ya Mkoa wa Ruvuma.

SPIKA: Ahsante sana tunakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi ninasimama kwa Kanuni ya 76 sitaisoma kutokana na muda.

Mheshimiwa Spika, Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina Wabunge wa aina mbili, lakini tukiwa humu ndani tunakuwa wote ni Wabunge. Ninajua kwamba nchi yetu ilipitia *Maputo Protocol* ndiyo maana kuna Wabunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Spika, wewe pia umekuwa mlezi wa Umoja wa Wanawake wa Bunge ndani ya Bunge hili na umetusaidia na kutu-*empower* kama wanawake kujiona tunafanya kazi yetu vizuri na bila kukosea.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na kawaida ya Mawaziri wakijibu majibu ya Wabunge humu ndani hasa Wabunge wanawake wanapouliza maswali wanasema Mbunge wa Jimbo hasa akiwa mwanaume alikwisha kuliuliza.

Ninaomba mwongozo wako ninapouliza swali kama Mbunge wa Viti Maalum ninajua ninawakilisha wanawake na wanaume wa Tanzania hii, hivyo basi mimi ninategemea Serikali ijibu sawasawa na Mbunge husika anayeuliza swali. (*Makofi*)

Ninaomba mwongozo wako kama hii iko sahihi na kibaya zaidi wanawake Mawaziri hao ndiyo wanaotuangusha wanasema Mbunge mwanamme aliwahi kuuliza swali. Naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Kanuni inasema Spika anaweza akajibu hapo hapo au wakati mwingine. Naomba hili nijibu wakati mwingine, ahsante sana (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa naona miongozo ilikuwa hiyo miwili tu? Tunaendelea sasa naomba nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, anakuja Makamu wa Mwenyekiti Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa karibu sana.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba taarifa yote kama ilivyowasilishwa mezani na kiambatisho chake iingie katika Taarifa Rasmi ya Bunge yaani *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, nakushukuru kwa kutoa idhini chini ya kifungu cha 11(3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 ili Kamati iwasilishe taarifa yake ya kwanza ya uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Pili wa tarehe 9 Februari, 2021.

Mheshimiwa Spika, idhini hiyo imekuwa ikitolewa tangu kipindi cha Bunge la Kumi na Moja, baadaye chini ya usimamizi makini wa uongozi wa Bunge la Kumi na Moja utaratibu wa kuwasilisha taarifa za uchambuzi wa sheria ndogo ukaboreshwaa kupitia marekebisho ya Kanuni za Bunge. Uboreshaji huo umeongeza umakini wa Bunge katika kusimamia utatuzi wa kero za wananchi zinazoweza kusababishwa na utekelezaji wa kanuni za Wizara, Taasisi mbalimbali na sheria ndogo za Halmashauri nchini.

Mheshimiwa Spika, nilihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa taarifa hii itawezesha na kuvutia majadiliano kuhusu sheria ndogo kutokana na jinsi hoja zilivyofafanuliwa kwa ubainishaji wa dosari, madhara yake na maoni yaliyobainishwa katika kujenga hoja kwa sababu hiyo naomba kubainisha muundo wa taarifa ninayowasilisha kwa ajili ya kurahisisha ufuatiliaji kabla ya mjadala wa jumla taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza ni utangulizi ambayo inatoa maelezo ya jumla kuhusu madaraka ya kutunga sheria, udhibiti wa sheria ndogo na namna Kamati iliyofanyakazi.

Sehemu ya pili ni maelezo kuhusu uchambuzi ambayo inafafanua matokeo na hoja zilizobainishwa kutokana na uchambuzi wa sheria ndogo. Aidha, sehemu ya tatu inatoa mtazamo wa Kamati kuhusu hoja zilizobainishwa katika uchambuzi na kujenga msingi wa mapendekezo katika uamuzi na ushauri wa Bunge; na mwisho ni sehemu ya nne ambayo inabainisha mapendekezo na maadhisho pamoa na kuhitimisha kwa kutoa hoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kueleza sehemu ya taarifa inayorejea maelezo kuhusu madaraka ya kutunga sheria nchini, udhibiti wa Bunge wa sheria ndogo na Kamati inavyosaidia udhibiti wa Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 64 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania mwaka 1977 imelipa Bunge la Jamhuri ya Muungano la Tanzania mamlaka yote ya kutunga sheria juu ya mambo yote ya Muungano na yasiyo ya Muungano yahusuyo Tanzania Bara. Hata hivyo Ibara ya 97(5) ya Katiba inaliruhusu Bunge kukasimu madaraka yake kutunga sheria kwa mtu yejote au idara yoyote ya Serikali. Sheria zinazotungwa kwa utaratibu huu huitwa sheria ndogo. Msimamo huu wa Katiba kuhusu utungaji wa sheria ndogo unakubalika na kutumika katika mabunge mengine duniani, lakini mabunge hayo yameweka utaratibu wa udhibiti wa sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa sheria ndogo unaofanywa na Bunge la Tanzania ni wa kawaida kama katika Mabunge ya nchi za Jumuiya ya Madola lengo ni kuwezesha Bunge kujiridhisha Iwapo madaraka ya kutunga sheria yaliyokasimiwa na mamlaka nyingine yametumika kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa utungaji na udhibiti wa sheria ndogo nchini Tanzania umefafanuliwa katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya Kwanza (*Interpretation Act Cap. 1*) kifungu cha 37(1) na (2) cha sheria hii kinataka sheria ndogo itangazwe katika Gazeti la Serikali kabla ya kuanza kutumika. Aidha, kifungu cha 38(1) cha sheria hiyo kimeweka sharti la sheria ndogo zinazotangazwa katika Gazeti la Serikali kuwasilishwa Bungeni ndani ya siku sita za vikao vya Bunge vinavyofuata baada ya tarehe ya kuchapisha Toleo la Gazeti lilitangazwa.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 43(2) ya Kanuni za Bunge imeweka utaratibu wa sheria ndogo kuwasilishwa Bungeni kwa utaratibu huo baada ya sheria ndogo kuwekwa mezani fasihi ya 8 ya Kanuni 43 ikisomwa pamoja na kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge inataka sheria ndogo hizo zihadiliwe na kamati ya sheria ndogo na katika utaratibu huo fasihi ya pili ya kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kinamtaka

Mwenyekiti wa Kamati kumjulisha Spika kwa maandishi baada ya Kamati kukamilisha uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, masharti ya Kanuni za Bunge yamezingatiwa jambo linalowezesha kutumia mamlaka yaliyopewa chini ya fasihi ya tatu ya kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge na kuagiza taarifa hii iwekwe katika orodha ya shughuli za leo ili Bunge lipokee na kujadili hatimaye kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 9 Februari, 2021 Serikali iliyasilisha mezani nakala ya magazeti ya Serikali na nyongeza zake ikiwemo jumla ya sheria ndogo 915 ambazo mchanganuo wake unaoneshwa; Sheria za Halmashauri (*by-laws 61*); Kanuni za Wizara (*Regulation 106*); Amri (*Orders 427*), Hati (*Instrument 1*) Matangazo Notisi (*Notice 294*), Rules 25 na Sheria ambayo ni Matamko (*Proclamation 1*).

Mheshimiwa Spika, jukumu la uchambuzi wa sheria ndogo iliyooongozwa na masharti ya fasihi ya kwanza kifungu cha 11 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Kifungu hicho kinaitaka Kamati kujiridhisha iwapo sheria ndogo zimekidhi na kuendana na maelekezo ya Katiba, sheria kuu ya sheria ndogo inayohusu pamoja na sheria nyingine za nchi.

Katika kujiridhisha uchambuzi ulifanywa kwa kutumia vigezo vikuu vitano ambavyo ni; moja, uzingatiaji wa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya nchi mwaka 1977; pili, kutokinanza kwa masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutunga sheria ndogo inayohusika; tatu, uzingatiaji wa masharti bora ya uandishi wa sheria (*Drafting Principles*); nne, uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi ya walengwa na viwango vya adhabu na faini inayotiliwa maanani; na tano, ufasihhi na ufasaha wa uandishi wa majedwali ya sheria ndogo inayohusika.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi yanabainisha jumla ya dosari 119 zilizoripotiwa katika taarifa hii kwa urahisi wa kufuatizia dosari hizo taarifa hii

imeambatisha jedwali la uchambuzi ambayo ni sehemu ya taarifa hii kwa ajili ya rejea wakati wa mjadala na uamuvi.

Mheshimiwa Spika, dosari za kutozingatia masharti ya Katiba; Katiba ni sheria kuu ya nchi na miongoni mwa kazi zake ni kuonesha mgawanyo wa madaraka kati ya dola na jamii na mgawanyo huo miongoni mwa mihimili ya Serikali. Kutokana na ukuu wa Katiba Bunge haliwezi kuruhusu mamlaka nyingine kutunga sheria ndogo inayokiuka masharti ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, sheria ndogo iliyokutwa na hoja za kukinzana na masharti ya Katiba ni Sheria Ndogo ya Kilimo na Hifadhi ya Chakula za Halmashauri ya Itilima ya mwaka 2020. Katika sheria hiyo kifungu cha 16(d) kinamshurutisha mfugaji kuijunga na vyama vya ufugaji. Sharti hili linakinzana na masharti ya Ibara ya 20 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inayohusu uhuru wa mtu kushirikiana na wengineo. Kwa msingi huu Bunge lako Tukuru halitarajii kupuuza matumizi ya kifungu cha sheria ndogo kinachoshurutisha jambo liliopewa hiari na Katiba; pili, kukinzana na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutunga sheria ndogo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 36(1) cha Sheria Tafsiri ya Sheria kinataka sheria ndogo yoyote inayotungwa isikinzane na mashari yaliyowekwa katika sheria mama, lakini uchambuzi umeonesha kuwa jumla ya sheria ndogo tatu zina dosari ya kukinzana na sheria mama. Kwa mfano sheria ndogo ya *Tanzania Teachers Professional Board General Regulations* ya mwaka 2020 imebainisha kukinzana na sheria mama.

Mheshimiwa Spika, katika sheria ndogo hiyo kanuni ya 37(3) imempa Waziri mamlaka ya kuteua Kamati ya kushughulikia rufaa kinyume na kanuni ya 49 ya sheria mama ambayo kimemtaka Waziri mwenyewe kuwa mamlaka ya rufaa. Kwa kuwa utaratibu wa kuteua Kamati haukuwekwa katika sheria mama mamlaka hayo ya Waziri ni batili kwa

kifungu cha 36(1) cha sheria ya tafsiri; tatu, Kutoendana na masharti bora ya uandishi wa sheria.

Mheshimiwa Spika, sheria inayotungwa na Bunge huzingatia misingi bora ya uandishi wa sheria, sheria ndogo 15 zimebainika kuwa na hoja zinazohusu misingi ya uandishi wa sheria; kwa mfano katika Sheria Ndogo ya Ada, Ushuru, Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Same ya mwaka 2020 imeonesha hivyo. Kifungu cha pili cha sheria ndogo hiyo kinatafsiri neno madini ya ujenzi kwa kutaja aina 12 za madini ya ujenzi ikiwemo chokaa. Hata hivyo jedwali la pili la sheria hizo linalohusu ushuru halitaji madini ya chokaa. Uandishi wa namna hii unaweza kuondoa uhalali wa kutoza ushuru wa madini ya chokaa na kuikosisha Halmashauri mapato. Aidha, uandishi huo unaweza kusababisha halmashauri kutozwa ushuru wa chokaa bila mwongozo wa viwango Jambo ambalo linaweza likazua kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika utungaji wa sheria huzingatia uhalsia ikiwemo hali halisi na mazingira ya watumiaji wa sheria inayohusika. Sheria ndogo 11 zimebainika kuwa na dosari zinazokinzana na uhalsia, kwa mfano Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashari ya Kiteto ya mwaka 2020 sehemu ya nne kipengele cha 8 jedwali la kwanza inaweka sharti la malipo ya ada kwa shughuli za jando na unyago ya kiasi cha shilingi 20,000 kwa tukio. Shughuli hizi si shughuli za kijamii na lengo lake ni kutoa mafunzo ya maisha ya kijamii kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, Bunge linapokasimu mamlaka ya kutunga sheria linataraji mamlaka inayohusika itafanya hivyo kwa namna yenye maana ya kwa jamii kwa utekelezaji wa sheria mama au sheria nyingine za nchi. Bunge haliwezi asilani kuachia mamlaka zilizoruhusiwa na sheria ya Bunge zitunge sheria ndogo zinazoakisi shabaha na madhumuni ya sheria mama.

Mheshimiwa Spika, tozo za shilingi 20,000 kwa tukio la jando na unyago si jambo lenye mantiki yoyote katika maisha ya jamii ya wakazi wa Kiteto, kuendelea kuwatoza wananchi

ada ya shughuli za jando na unyago ni kuongeza kero na adha kubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, makosa ya uandishi wa majedwali ya sheria ndogo; uandishi mzuri wa sheria unawezesha sheria inayohusika kueleweka na kuelezeka kama ilivyokusudiwa. Uandishi huu ni pamoja na uandishi fasaha wa majedwali ambayo hutoa maelezo na ufanuzi wa kina wa kifungu na kanuni inayohusika. Majedwali hayo yatakuwa na maana iwapo yatawekwa kwa namna inayorejea kwa ufasaha kifungu na kanuni wezesha inayoeleza mantiki, madhumuni na maudhui ya jumla ya sheria hiyo. Mfano dosari za uandishi wa majedwali inadhihirika katika Kanuni ya Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza ya mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 14 cha jedwali la kwanza kinaweka utafiti wa mambo ya filamu katika orodha ya mambo yanayopaswa kuongezwa kuombewa kibali katika Bodi ya Filamu. Kipengele hiki hakionyeshi kama utafiti wa kitaalamu unaohusu uandishi wa tasnifu (*thesis*) utapaswa kuombewa kibali au la uandishi wa namna hii unafanya majedwali kukosa ubayana na kusababisha kutoeleweka kwa sehemu inayojusudiwa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya sita; wadau muhimu kutoshirikishwa katika mchakato wa utungaji wa kanuni ya Bodi ya Ualimu. Ushirikishwaji wa wadau hasa wale wanaoguswa moja kwa moja na sheria au kanuni inayotungwa ni jambo linalozingatia umuhimu wa mtazamo wa wengi. Bunge kwa upande wake limeweka masharti ya kuwashirikisha wadau wakati wa utungaji wa sheria kama ilivyoelezwa katika kanuni 97(2) na kanuni ya 136(9) ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa mchakato wa kutengeneza Kanuni ya Bodi ya Ualimu ya mwaka 2020 ilihuisha mamlaka mbalimbali za Serikali bila kuwashirikisha wadau wanaoguswa moja kwa moja wadau hao ni kama Chama cha Walimu (CWT) na mashirika yanayojihusisha na masuala mbalimbali ya walimu. Kwa hakika kuna haja ya

mamlaka inayohusika na kanuni ya Bodi ya Walimu kukaa na wadau ili kupata mawazo jumuishi kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kanuni hiyo.

Mheshimiwa Spika, dosari za Kanuni ya Filamu na Michezo ya Kuigiza kuwa na makatazo kwa namna inayokatanisha utekelezaji wake; kwa umuhimu wa uandishi wa sheria kutokuweka masharti ambayo yanaweza kuleta utatanishi katika utekelezaji wake imeelezwa. Uchambuzi wa Kamati umebaini Kanuni ya 16 ya Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza ya mwaka 2020 imeainisha makatazo mbalimbali ya maudhui mabaya katika filamu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa mantiki ya zuio la maudhui hayo ni kana kwamba Kanuni zinalenga kuzuia uigizaji wa filamu zinazohusu masuala kama vile ulevi, matumizi ya dawa za kulevyia na ukahaba, hali inayoweza kudumaza uigizaji kwenye vipengele mbalimbali vyenye lengo la kuonesha uhalisia na kutoa mafunzo kwa jamii. Msisitizo wa Bunge ni kuona haja ya kufanya marekebisho katika sehemu hiyo ili kuondoa baadhi ya maneno yanayoonesha kukataza moja kwa moja uigizaji wa masuala yenye mtazamo hasi yanayofikisha ujumbe kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, sehemu/jambo la nane ni dosari ya msisitizo katika udhibiti na tozo zaidi kuliko ufanuzi na mwongozo. Kamati imebaini kuwa Kanuni ya Filamu na Michezo ya Kuigiza ya mwaka 2020 zimejielekeza zaidi katika kudhibiti na kuweka tozo pasipo kujikita zaidi katika kutoa ufanuzi wa miongozo mbalimbali ya namna ya kulea na kustawisha tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza nchini.

Mheshimiwa Spika, Bunge linasisitiza umuhimu kwa mamlaka zinazosimamia tasnia mbalimbali na hasa zinazohusisha vijana wengi nchini, kutunga kanuni zinazotoa miongozo na ufanuzi wenye lengo la kustawisha shughuli zao na hatimaye ziendelee kutoa ajira nydingi kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tisa ni ushirikiano katika masuala yanayohusuru Wizara zaidi ya moja; inatarajiwu

kwamba pale ambapo kuna masuala yanayotekelawa na mamlaka zaidi ya moja basi mamlaka hizo zinapaswa kuwasiliana ili kuhuisha masuala wanayoyasimamia kwa pamoja ili kutoleta changamoto katika usimamizi wake.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini Kanuni ya Filamu na Michezo ya Kuigiza ya mwaka 2020 zilizo chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Sheria Ndogo za Ada za Vibali vya Burudani za Halmashauri mbalimbali nchini zilizo chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa pamoja zinatoza ada za vibali vya kuendesha kumbi za cinema/video na michezo ya kuigiza. Utozaji huo unapelekea ugumu katika utekelezaji wa shughuli hizo katika jamii ya watu wenye kipato cha chini, jambo ambalo linaongeza kero kwa wananchi kinyume na matarajio ya kuboresha ustawi wao.

Mheshimiwa Spika, Bunge halitarajii kuona mamlaka zinazotekeleza majukumu yanayoingiliana zifanye kazi pasipo kushirikiana ili kuondoa uwezekano wa kuleta kero kwa wananchi wanaoguswa na shughuli zinazosimamiwa na mamlaka zaidi ya moja.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matokeo ya uchambuzi huo, Kamati ina maoni katika maeneo makuu matano yaliyojitekeza kama ifuatavyo:-

Moja; uzingatiaji wa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977; kutokuzingatiwa kwa misingi inayowekwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika uandishi wa sheria ndogo ni jambo linaloweza kusababisha mifumo, taasisi na mwelekeo wa jamii kutoendana na misingi ya Katiba. Hali hiyo, ni kinyume na inavyopaswa kuwa, ambapo masharti ya Katiba ni chimbuko la sheria zote za nchi.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa ukiukwaji wa misingi ya utawala bora, ukiukwaji wa upatikanaji wa haki mbalimbali zikiwemo haki za kisiasa, kiuchumi na kijamii zinaweza kutokea kutokana na dosari hizo.

Eneo la pili ni dosari za sheria ndogo kukinzana na sheria mama zinaathiri tija ya utekelezaji wa sheria; dosari hii ikiendelea, masharti yaliyowekwa kwenye sheria mama kwa lengo la kuiwezesha mamlaka inayohusika kutunga sheria ndogo yatakosa maana katika utekelezaji wa sheria. Ni maoni ya Kamati kuwa Bunge haliwezi kupuuza misingi ya utungaji wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa sheria zote kuendana na misingi ya uandishi bora wa sheria, dosari za sheria ndogo kutoendana na utaratibu bora wa uandishi wa sheria, si jambo la kuachwa katika utunzi wa sheria ndogo. Dosari hizo zinaweza kuwa dalili mbaya za utekelezaji wa sheria kwa kusababisha sheria mama isieleweke vizuri, hali hiyo si jambo linaloweza pia kupuuzwa na Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, Sheria ndogo kukinzana na uhalisia kwa kuwa na maudhui yasiyozingatia hali ya kiuchumi ya walengwa, zinaweza kuathiri utekelezaji na kusababisha matokeo mabaya ya sheria. Sheria ndogo zinapoweka viwango vikubwa vyta faini, ada, ushuru na adhabu kuliko uwezo na hali halisi zitakosa maana katika jamii na zinakinzana na busara zinazotakiwa na Bunge wakati wa utungaji wa sheria.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya majedwali katika uandishi wa sheria ndogo ni jambo la kuzingatiwa katika uchambuzi wa sheria. Majedwali hutumika kutoa maelezo au ufanuzi wa ziada wa vifungu au kanuni katika sheria ndogo. Kwa sheria ndogo kuwa na dosari ya uandishi wa majedwali zinaathiri ukamilifu wa sheria na kutatiza utekelezaji wa masharti yanayowekwa na vifungu vinavyohitajika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lizingatie maelezo ya jumla niliyoyatoa, ufanuzi wa matokeo ya uchambuzi na maoni ya Kamati ili kujadili na kutoa uamuzi. Ikumbukwe kuwa hoja hii inahusu eneo muhimu la utekelezaji wa sheria ambalo lisipoangaliwa kwa umakini linaweza kuwa mazalia ya kero, karaha na manung'uniko mionganoni mwa jamii.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja katika maeneo makuu matatu kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza; kutokana na matokeo ya uchambuzi, hoja ya Kamati inayohusu dosari za jumla zilizojitokeza katika sheria ndogo, inatokana na jukumu la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali la kuhakiki sheria ndogo. Kamati inatoa hoja kwamba:-

KWA KUWA, dosari za jumla kuhusu uandishi na utungaji wa sheria ndogo zimeendelea kujitokeza, jambo linalotofautiana na matarajio yatokanayo na nafasi ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kuhakiki sheria ndogo;

NA KWA KUWA, kubainika kwa dosari hizo mara kwa mara kunaashiria mawasiliano duni baina ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na mamlaka zilizotunga sheria ndogo zinazohusika, hali inayoathiri mafanikio ya utungaji na utekelezaji wa sheria ndogo;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iendelee kufuatilia mawasiliano na kuhakiki ipasavyo sheria ndogo zinatungwa ili kupunguza kama sio kuondoa dosari katika sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili; kuhusu hoja tano za maudhui na uandishi wa sheria ndogo. Uzingatiaji wa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, 1977:-

KWA KUWA, baadhi ya sheria ndogo zilizochambuliwa zimekutwa na dosari ya kuwa na msharti yanayokiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, jambo lisiloweza kuafikiwa na Bunge;

NA KWA KUWA, Kutorekebishwa kwa sheria ndogo hizo kunaweza kusababisha ukiukwaji wa misingi ya utawala bora, ukiukwaji wa upatikanaji wa haki mbalimbali zikiwemo haki za kisiasa, kiuchumi na kijamii zilizowekwa kwa mujibu wa Katiba na kuathiri ustawi wa jamii;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba mamlaka zinazotunga sheria ndogo ziliziotunga na dosari na kukinzana na masharti ya Katiba, zirekebishe dosari hizo haraka sana.

Mheshimiwa Spika, kukinzana na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutungwa kwa sheria ndogo:-

KWA KUWA, baadhi ya sheria ndogo zilizochambuliwa zimebainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi, jambo linaloweza kuathiri tija ya utekelezaji wa sheria mama inayohusika;

NA KWA KUWA, sheria inayokinzana na sheria mama au sheria nyingine za nchi, inakaidi masharti ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, hali inayosababisha sheria ndogo hiyo kuwa batili kwa mujibu wa Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba mamlaka zilizotunga sheria ndogo zilizobainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine zirekebishe sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, tatu; kutozingatia misingi ya uandishi bora wa sheria:-

KWA KUWA, kwa kuwa zipo sheria ndogo zilizobainika kuwa na dosari ya kutozingatia misingi ya uandishi bora wa sheria (*Drafting Principles*);

NA KWA KUWA, dosari hizo zinaonesha dalili mbaya za utekelezaji wa sheria na kusababisha sheria mama isieleweke vizuri, hali inayoathiri utekelezaji wa sheria iliyotungwa na Bunge;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizotunga sheria ndogo zenye dosari za kutozingatia misingi ya uandishi bora wa sheria zinarekebishwa dosari hizo.

Mheshimiwa Spika, nne; dosari za uandishi wa majedwali ukilinganishwa na vifungu vyaheria:-

KWA KUWA, baadhi ya sheria ndogo zilizochambuliwa zimebainika kuwa na dosari mbalimbali katika uandishi wa majedwali ambayo hutoa ufanuzi wa ziada wa vifungu au kanuni katika sheria ndogo;

NA KWA KUWA, dosari ya uandishi wa Majedwali kwenye sheria ndogo inaathiri ukamilifu wa sheria na kutatiza utekelezaji wa sheria inayohusika;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga sheria ndogo zilizobainika kuwa na dosari zirekebishe dosari hizo.

Mheshimiwa Spika, tano; masharti yasiyo na uhalisia:-

KWA KUWA, zimebainisha sheria ndogo zilizo na dosari ya kuweka vifungu vyenye masharti yanayokinzana na uhalisia kutoekana na kuwa na maudhui yasiyozingatia hali ya uchumi wa walengwa wala uwezekano wa utekelezaji;

NA KWA KUWA, dosari hizo zinaweza kuathiri utekelezaji na kusababisha matokeo mabaya ya sheria, kwa hiyo kuweka viwango vikubwa vyta faini, ada, ushuru na adhabu kuliko uwezo na hali halisi, vinaongeza kero kwa wananchi na kuzuia ustawi wa maisha yao;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizopewa mamlaka ya kutunga sheria ndogo hizo zilizobainika ziondoe dosari hizo ili ziendane na na uhalisia wa maisha ya watu.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni kuhusu hoja nne za sheria ndogo mahsus; wadau muhimu kutoshirikishwa katika mchakato wa utungaji wa Kanuni za Bodi ya Kitaaluma ya Walimu:-

KWA KUWA, ushirikishwaji wa wadau katika utungaji wa sheria yoyote unawezesha mawazo jumuifu na kurahisisha utekelezaji bora wa sheria inayohusika, lakini mchakato wa utungaji wa Kanuni za Bodi ya Kitaaluma ya Walimu ya

mwaka 2020 umebainisha kutowashirikisha wadau wanaoguswa moja kwa moja na sheria hiyo;

NA KWA KUWA, kutowashirikisha wadau wanaoguswa moja kwa moja na Kanuni hizo, kunasababisha changamoto ya utekelezaji ikiwemo kutoeleweka vizuri, manung'uniko ya wadau na kutotambulika kwa manufaa ya kanuni hizo;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka iliyokabidhiwa madaraka ya kuweka Kanuni za Bodi ya Kitaaluma ya Walimu, ikutane na wadau wa sekta ya elimu wanaoguswa moja kwa moja na Kanuni hizo ili kupata maoni yao kabla ya kuziboresha na kuripoti matokeo ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mbili; dosari ya Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza kuwa na makatazo kwa namna inayotatanisha utekelezaji wake:-

KWA KUWA, imebainika kukosekana kwa ufanuzi bayana wa makatazo ya Kanuni ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, ikiwemo kuzuia uigizaji wa ulevi, matumizi ya dawa za kulevyta, ukahaba na mengineyo kwa namna ya kukataza kama vile havikatazwi;

NA KWA KUWA, kukosekana kwa ufanuzi huo bayana wa maudhui ya Kanuni hiyo kunatatanisha utekelezaji wake, jambo linaloweza kusababisha uonevu na kuathiri ubora wa sanaa ya uigizaji;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba maneno yanayoonesha hali ya kukataza moja kwa moja uigizaji wa masuala yenye mtazamo hasi kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa jamii yarekebishwe katika kanuni hiyo.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu; dosari ya msisitizo katika udhibiti na tozo zaidi kuliko ufanuzi na mwongozo:-

KWA KUWA, uchambuzi umebaini dosari ya Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza kujikita katika maudhui ya

kuweka tozo na kudhibiti, kuliko kuweka miongozo yenye lengo la kuilea na kuistawisha jamii hiyo;

NA KWA KUWA, hali hiyo inaweza kudhoofisha ukuaji wa tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza ambayo imeajiri idadi kubwa ya vijana nchini na kuchangia kwa kiasi fulani kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, serikali iangalie namna ya kuboresha Kanuni hizi ili zitoe miongozo ya kuboresha tasnia za filamu na michezo ya kuigiza kwa lengo la kuchochaea ushiriki wa vijana.

Mheshimiwa Spika, eneo la nne; ushirikiano katika masuala yanayohusu Wizara zaidi ya moja:-

KWA KUWA, Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza ya mwaka 2020 zilizotungwa na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Sheria Ndogo za (Ada za Vibali vya Burudani) za Halmashauri mbalimbali nchini chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, kwa pamoja zinatoza ada za vibali vya kuendesha kumbi za cinema/video na michezo ya kuigiza;

NA KWA KUWA, utozaji huo unaweka ugumu wa utekelezaji wa shughuli hizo katika jamii ya watu wenye kipato cha chini, jambo ambalo linaongeza kero kwa wananchi kinyume na matarajio ya kuboresha ustawi wao;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo zikae pamoja ili kuona namna bora ya kuhuishaa viwango vya ada za kumbi za kuoneshea cinema na michezo ya kuigiza.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Bunge lako Tukufu kwa kuweka utaratibu wa taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa naomba nimshukuru Mhe. Jenista Mhagama, Mbunge – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu) kwa kuendelea kuweka utaratibu mzuri wa kuwasilisha Mezani Magazeti ya Serikali pamoja na viambatisho vyake (Sheria Ndogo). Aidha, niwashukuru Mawaziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wa Wizara kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati na pia kwa kuanza hatua za utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ili kuondoa dosari mbalimbali zilizojitokeza katika sheria ndogo.

Mheshimiwa Spika, aidha niwashukuru wadau mbalimbali waliofika mbele ya Kamati kwa ajili na kutoa maoni ambayo yamesaidia Kamati kufanya uchambuzi wa kina katika Kanuni hizo. Wadau hao ni Shirikisho la Filamu Tanzania, HAKIELIMU, Chama cha Walimu Tanzania, *Association of Real Estate Professionals of Tanzania* na UWEZO TANZANIA.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Pili wa Bunge na hatimaye kufanikisha kazi hii, naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Spika, aidha napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, Katibu wa Bunge kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati hii ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, nimshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein akisaidiwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Gerald Magili, kwa usimamizi mzuri wa shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, niwashukuru Makatibu wa Kamati ya Sheria Ndogo Ndugu Mkuta Masoli na Ndugu Stanslaus Kagisa, wakisaidiwa na Bi.

Imelda Ntimba - Msaidizi wa Kamati kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi imekamilika taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba kutoa hoja, ahsante. (*Makofii*)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA
NDOGO KUHUSU UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO
ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA PILI WA
BUNGE - KAMA ILIVYOWASILSIHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

**1.0 MAELEZO YA JUMLA
1.1 Utangulizi**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, nakushukuru kwa kutoa idhini chini ya Kifungu cha 11 (3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020 ili Kamati iwasilishe **Taarifa yake ya Kwanza ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo**. Idhini hiyo imekuwa ikitolewa tangu kipindi cha Bunge la Kumi na moja. Baadaye chini ya usimamizi makini wa uongozi wa Bunge la Kumi na Moja, utaratibu wa kuwasilisha taarifa ya uchambuzi wa Sheria ndogo ukaboreshwu kupitia marekebisho ya Kanuni za Bunge. Uboreshaji huo umeongeza umakini wa Bunge katika kusimamia utatuzi wa kero kwa wananchi zinazoweza kusababishwa na utekelezaji wa kanuni za wizara au taasisi mbalimbali na sheria ndogo za halmashauri nchini.

Mheshimiwa Spika, fursa hii adhimu, inaiwezesha Kamati kulisaidia Bunge katika ufuatiliaji na udhibiti wa madaraka yake ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka mbalimbali serikalini. Nilihakikishie Bunge lako tukufu kuwa Taarifa hii itawezesha na kuvutia majadiliano kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni tarehe 09 Febuari, 2021 wakati wa Mkutano wa Pili. Uhakika huo unazingatia mambo makuu matatu:-

(i) Jinsi hoja mbalimbali zinavyofafanuliwa katika taarifa hii;

(ii) Namna iliyotumika kubainisha dosari na madhara yake ; na

(iii) Maoni ya Kamati kutokana na matokeo ya uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, Kamati imeona umuhimu wa kuonesha mawanda (*scope*) ya maudhui (*content*) ya taarifa hii ili kuwezesha ufuatiliaji wenyе ufanisi. Kwa madhumuni hayo, nitangulie kueleza kuwa taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

(i) Sehemu ya kwanza ambayo ni ya utangulizi inatoa maelezo ya jumla kuhusu madaraka ya kutunga sheria, udhibiti wa sheria ndogo na namna Kamati ilivyofanya kazi;

(ii) Sehemu ya pili ambayo ni maelezo kuhusu uchambuzi, inafafanua matokeo na hoja zilizobainika kutokana na uchambuzi wa sheria ndogo;

(iii) Sehemu ya tatu ambayo ni maoni na mapendekezo inaeleza mtazamo wa Kamati kuhusu hoja zilizobainika wakati wa uchambuzi; na

(iv) Sehemu ya nne inabainisha mapendekezo ya maazimio kuhusu hoja zilizojitokeza na kuhitimisha kwa kutoa hoja.

Mheshimiwa Spika, muundo huo wa taarifa na uwasilishaji unalenga kufanikisha mjadala wa Bunge utakaowezesha uamuzi wenyе manufaa kwa wananchi. Aidha, ili kuwezesha rejea kwa urahisi, Taarifa hii inasomwa kwa pamoja na Jedwali la Uchambuzi lilioambatishwa ambalo ni sehemu ya Taarifa hii na linaingia kwenye kumbu kumbu za majadiliano ya Bunge (Taarifa Rasmi za Bunge) Jedwali hilo linalobainisha dosari katika jumla ya sheria ndogo Ishirini na Tatu (23) ambazo ni sehemu ya sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Pili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo, nitangulie kusema kuwa ili taarifa hii iwezeshe tija iliyokusudiwa, kuna umuhimu wa kurejea maelezo kuhusu madaraka ya kutunga

Sheria nchini, Udhibiti wa Kibunge wa sheria ndogo na Kamati inavyosaidia udhibiti wa sheria ndogo. Baada ya ufanuzi huo ambao ni msingi mkuu wa majadiliano ya Bunge lako tukufu, Taarifa hii inabainisha matokeo ya uchambuzi ili kuonesha chimbuko la maoni ya Kamati na kubainisha hoja na mapendekezo juu ya uamuzi wa Bunge unaotarajiwa.

1.2 Madaraka ya Kutunga Sheria

Mheshimiwa Spika, madaraka ya kutunga sheria zote nchini yamewekwa chini ya mamlaka ya Bunge. Ibara ya 64 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 (Kama ilivyofanyiwa Marekebisho mara kwa mara), imelipa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka yote ya kutunga Sheria juu ya mambo yote ya Muungano na yasiyo ya Muungano yahusuyo Tanzania bara. Aidha, Ibara ya 97 ya Katiba imeweka utaratibu ambao unapaswa kuzingatiwa na Bunge katika kutekeleza madaraka yake ya kutunga Sheria.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mamlaka hayo ya Bunge, Ibara ya 97 (5) ya Katiba inaliruhusu Bunge kukasimu madaraka yake ya kutunga Sheria kwa mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali. Utaratibu huo wa kukasimu madaraka ya kutunga sheria unatokana na sababu mbalimbali ikiwemo:

- (i) Bunge kukosa muda wa kutosha wa kutunga sheria kuhusu masuala yote ambayo utekelezaji wake unahitaji kuwepo kwa sheria;
- (ii) Mahitaji ya sheria kwa dharura kwa kipindi ambacho Bunge haliwezi kukutana ili kutunga sheria inayokidhi mahitaji hayo kadiri inavyohitajika;
- (iii) Uzingatiaji wa masuala yanayohitaji utaalamu mahsusini;
- (iv) Mambo mengine yanayoendana na mahitaji ya utungaji wa sheria.

Mheshimiwa Spika, maelezo hayo ni msingi wa Bunge lako tukufu kuzingatia katika utaratibu wa kukasimu madaraka yake ya kutunga sheria. Kwa kufanya hivyo, Bunge linatambua kuwa utaratibu huo ni halali na unafaa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini iwe ni kwa madhumuni maalumu na mipaka, ukomo au upeo uliobainishwa kwa utaratibu unaodhibitiwa. Msimamo huu si wa Bunge la Tanzania pekee bali unakubalika na kutumika pia katika mabunge mengine duniani. Kwa kawaida Mabunge duniani yanahitaji kuhakikisha kuwa madaraka ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka nyingine yanatumika vizuri bila kuwa kero isiyokusudiwa kwa wananchi. Kuwezesha hilo, utaratibu unaotumiwa na Mabunge duniani unajumuisha mambo makuu yasiyopugua matano. Mambo hayo ni:-

- (i) Madaraka ya kutunga sheria ndogo yanapaswa kukasimiwa kwa mamlaka yenye kuaminika na kukubalika kitaifa;
- (ii) Wigo na mipaka ya sheria ndogo inayoweza kutungwa katika utekelezaji wa Sheria Mama (*Principal legislation*) ibainishwe dhahiri;
- (iii) Utekelezaji wa madaraka ya kutunga Sheria unapaswa kuzingatia umuhimu wa kuwahuishwa wadau;
- (iv) Mchakato wa utungaji wa sheria ndogo na matumizi yake uwezeshe sheria ndogo inayohusika kujulikana kwa umma; na
- (v) Ujulikane mfumo, utaratibu na mamlaka inayowezesha marekebisho au zuio la kutumika kwa sheria ndogo iwapo kama itahitajika hivyo.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza hadi la tatu hufanyiwa kazi na Bunge kabla ya mamlaka inayohusika na utungaji wa sheria ndogo haijaanza utekelezaji wa mamlaka hayo. Jambo la nne na tano katika hayo, yanasisitiza msingi wa utaratibu unaotumiwa na Bunge la Tanzania kusimamia sheria

ndogo nchini. Kwa mantiki hiyo, hoja inayojadiliwa katika kikao cha leo ni mionganoni mwa hoja zinazohitaji ufuatiliaji, majadiliano na uamuzi unaojengwa kwa kuzingatia hali halisi na maisha ya watu inavyostahili.

1.3 Udhibiti wa Kibunge wa Sheria Ndogo

Mheshimiwa Spika, Udhibiti wa Kibunge wa sheria ndogo (*Parliamentary Control Over Subsidiary Legislation*) ni utaratibu wa kawaida katika Mabunge ya nchi za Jumuiya ya Madola. Utaratibu huu unalenga kuliwezesha Bunge kujiridhisha kikamilifu iwapo utekelezaji wa madaraka ya kutunga sheria yaliyokasimu kwa mamlaka nyingine umefanyika ilivyokusudiwa na Bunge lenyewe. Udhibiti huo, hufanyika kwa kulinganisha sheria ndogo na masharti ya sheria kuu (Sheria Mama) pamoja na misingi mingine illyowekwa na Sheria zilizotungwa na Bunge. Tanzania ambayo ni mionganoni mwa nchi za Jumuiya ya Madola, hutumia utaratibu wa kudhibiti sheria ndogo kwa kuweka kwanza kifungu kwenye sheria mama kinachobainisha madaraka yanayokasimiwa katika sheria ndogo inayoweza kutungwa. Kifungu hicho kinaweza kuainisha sheria ndogo inayoweza kutungwa na mamlaka inayopewa madaraka ya kutunga sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, mchakato huo wa utungaji na udhibiti wa sheria ndogo nchini Tanzania umefafanuliwa katika *Sheria ya Tafsiri ya Sheria*, Sura ya 1, (*The Interpretation of Laws Act, Cap. 1*). Kifungu cha 37 (1) na (2) cha Sheria hii kinataka sheria ndogo itangazwe kwenye Gazeti la Serikali kabla ya kuanza kutumika. Aidha, kifungu cha 38 (1) cha Sheria hiyo kimeweka sharti kwa sheria ndogo zinazotangazwa kwenye Gazeti la Serikali kuwasilishwa (kuwekwa mezani) Bungeni ndani ya siku sita za vikao vya Bunge vinavyofuata baada ya tarehe ya kuchapisha toleo la Gazeti lilitangaza. Masharti hayo yamewekewa utaratibu katika mchakato wa Kibunge kwa kufafanuliwa na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 43 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, imeweka utaratibu wa sheria ndogo zilizotangazwa

katika gazeti la serikali kuwasilishwa Bungeni. Baada ya sheria ndogo kuwekwa mezani, Kanuni ya 43 (8) ikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inataka sheria ndogo hizo zihadiliwe na Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo. Katika Utaratibu huo, Kifungu cha 11 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kinaelekeza kuwa, Kamati inapokamilisha kazi ya Uchambuzi Mwenyekiti wa Kamati anapaswa kumjulisha Spika kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo ya Kanuni za Bunge yamezingatiwa ipasavyo na kukuwezesha kutumia mamlaka uliyopewa chini Kifungu cha 11 (3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kuagiza Taarifa hii iwekwe kwenye Orodha ya Shughuli za Leo. Katika hatua hii, niliombe Bunge lako Tukufu liipokee na kujadili kwa kina Taarifa ninayoiwasilisha na hatimaye litoe uamuzi kwa maazimio yanayotokana na Uchambuzi wa sheria ndogo zilozowasilishwa wakati wa Mkutano wa Pili. Majadiliano hayo yazingatie kuwa Kifungu cha 38 cha *Sheria ya Tafsiri ya Sheria*, kimebainisha uwezo wa Bunge kufanya marekebisho katika sheria ndogo au kuibadilisha sheria ndogo inayohusika.

Mheshimiwa Spika, Mantiki ya kujadili Taarifa hii ni utaratibu na utamaduni wa mabunge duniani kufanya sehemu kubwa ya kazi yake kwa kutumia Kamati zake. Kwa desturi za kibunge, Taarifa hii ni nyenzo ya msingi kwa Bunge lako tukufu kutekeleza wajibu wake wa kudhibiti sheria ndogo nchini. Katika kufanikisha wajibu huo wa Bunge, Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo inaweza kutumia namna kuu mbili ambazo ni:-

- (i) Kuchambua sheria zilizowekwa Mezani; na
- (ii) Kuchambua sheria ndogo zinazoendelea kutumika.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inatoa matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowekwa mezani wakati wa Mkutano wa Pili wa Bunge. Kwa sababu hiyo, bado zipo sheria ndogo

nyingine nyingi ambazo hazijawahi kuchambuliwa na kujadiliwa na Bunge ingawa zinatumika. Utaratibu huu wa kutumika kwa Sheria Ndogo kabla ya kuchambuliwa na kujadiliwa na Bunge unaruhususiwa katika mfumo wa udhibiti wa sheria ndogo usio wa moja kwa moja (*Indirect control*) ambao Tanzania unaoufua na kuutumia.

1.4 Namna Kamati ilivyofanya Kazi

Mheshimiwa Spika, ili kuzingatia ipasavyo masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge yanayoitaka Taarifa hii kubainisha njia na mbinu zilizotumika katika utekelezaji wa jukumu la kuchambua sheria ndogo, naomba kulijulisha Bunge hili kuwa Kamati ilitumia njia na mbinu kuu zifuatazo:-

- (i) Kufanya uchambuzi wa awali ili kubaini sheria zinazohitaji kufanyiwa uchambuzi na mambo yatakayopaswa kuzingatiwa wakati wa uchambuzi wa kina;
- (ii) Kuwaalika wadau kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 139 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge;
- (iii) Kujadiliana na Mamlaka iliyotunga sheria ndogo inayohusika; na
- (iv) Kufanya uchambuzi kwa kuhusianisha, kulinganisha, kuoanisha, kufananisha na kutofautisha matokeo ya uchambuzi wa awali, maoni ya wadau na majadiliano kati ya Kamati na mamlaka iliyotunga sheria ndogo inayohusika.

Mheshimiwa Spika, njia na mbinu ya uchambuzi wa awali illiwezesha Kamati kubaini sheria ndogo zenye hoja za aina tano zifuatazo:-

- (i) kukiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- (ii) kuwa kinyume na masharti ya Sheria inayotoa mamlaka ya kutunga sheria ndogo au sheria nyingine yoyote;
- (iii) kutozingatia misingi bora ya uandishi wa Sheria (*drafting principles*);

- (iv) kutoendana na uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini; na
- (v) makosa ya uandishi katika Majedwali (Kutorejea Kanuni sahihi, kurejea Kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa Kanuni na Maudhui ya Jedwali tofautiana na Vifungu vinavyoyaanzisha).

Mheshimiwa Spika, usikilizaji wa maoni ya wadau (*Public hearing*) uliwezesha Kamati kuzingatia masharti ya Kanuni za Bunge. Mbinu hiyo imejengwa katika msingi kwamba sheria ndogo ndizo zinazofafanua utekelezaji wa Sheria iliyotungwa na Bunge, hivyo zinawagusa moja kwa moja wadau na jamii nzima. Kwa sababu hiyo, bila ya kuwaalika wadau, isingelikuwa rahisi kujiridhisha ipasavyo na namna sheria ndogo inavyowezesha ustawi wa wananchi amba ni lengo kuu la serikali kwa mujibu wa Ibara ya 8 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika hatua hii naomba kukiri kuwa wadau waliofika mbele ya Kamati wamefanikisha utekelezaji wa majukumu ya Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, aidha Kamati ilikutana na mamlaka zilizotunga sheria ndogo kuhusu sheria ndogo zilizochambuliwa na Kamati, majadiliano yalilenga kupata ufanuzi wa hoja zilizoibuliwa na Kamati. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa katika uchambuzi wa sheria ndogo hizi, Kamati ilipata ushirikiano uliohitajika na kuwezesha kukamilisha kazi ya uchambuzi inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sehemu inayofuata ya taarifa hii italiwezesha Bunge kujadili inavyopaswa na hatimaye kufanya uamuzi wenye tija na manufaa kwa wananchi na maisha yao kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nitumie fursa hii kulisihii Bunge lako tukufu liendelee na msisitizo wake wa kuona sheria ndogo haziwi kero kwa wananchi wala kikwazo cha ustawi na maendeleo yao. Msisitizo huu unatokana na sheria ndogo

kugusa moja kwa moja shughuli za watanzania walio wengi zikiwemo:-

- (i) Kilimo cha mazao ya biashara na chakula;
- (ii) Ufugaji na Uvuvi;
- (iii) Biashara za mama lishe na baba lishe;
- (iv) Sanaa (Muziki, Sinema, Uchongaji, Michezo ya Kuigiza n.k.);
- (v) Vikoba;
- (vi) Machinga;
- (vii) Biashara ya usafiri wa bodaboda, bajaji, daladala; na
- (viii) Uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa shughuli hizo kwa uhai na maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla, Bunge lina kila sababu ya kuwa na jicho lake katika sheria ndogo. Kufanya hivyo, kutasaidia kuondoa kero mbalimbali na hatimaye kuchochaea maendeleo ya shughuli hizo.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI

2.1 Ufafanuzi kuhusu Sheria zilizochambuliwa

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 9 Februari, 2021 Serikali iliwasilisha Mezani nakala za Magazeti ya Serikali na nyongeza zake zikiwemo jumla ya **Sheria Ndogo Mia Tisa Kumi na Tano (915)**. Mchanganuo wa sheria ndogo hizo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Sheria Ndogo za Halmashauri (*By-Laws*) – **61**;
- (ii) Kanuni za Wizara (*Regulations*) – **106**;
- (iii) Amri (*Orders*) – **427**;
- (iv) Hati (*Instrument*) – **1**;
- (v) Matangazo (*Notices*) – **294**;
- (vi) *Rules* – **25**; na
- (vii) *Proclamations* – **1**.

2.2 Vigezo vilivyotumika katika uchambuzi

Mheshimiwa Spika, jukumu la uchambuzi wa Sheria Ndogo liliongozwa na masharti ya Kifungu cha 11(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Kifungu hicho kinaitaka Kamati kujiridhisha iwapo Sheria Ndogo zimekidhi na kuendana na maelekezo ya Katiba, Sheria Kuu ya Sheria Ndogo inayohusika pamoja na sheria nyingine za nchi. Katika kujiridhisha huko, wakati wa Uchambuzi Kamati ilitumia vigezo vifuatavyo:-

- (i) Uzingatiaji wa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- (ii) Kutokinzana na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutungwa kwa sheria ndogo inayohusika;
- (iii) Uzingatiaji wa misingi bora ya uandishi wa sheria (*drafting principles*);
- (iv) Uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini ulivyotiliwa maanani; na
- (v) Usahihi na ufasaha wa uandishi wa majedwali ya sheria ndogo inayohusika. Mfano, kutorejea kanuni kwa sahihi, kutorejea Kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa Kanuni inayohusika pamoja na kutofautiana kati ya maudhui ya Jedwali na vifungu vinavyoyaanzisha Jedwali.

2.3 Hatua za Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, hatua za uchambuzi wa sheria ndogo unaoripotiwa leo, ziliwezesha Kamati kujikita katika kubaini kama sheria zilizotungwa zimetokana na madaraka ya Bunge na iwapo madaraka hayo hayakutumika tofauti. Mchakato ulianza kwa kuingiza uchapishwaji wa sheria ndogo kwenye Kumbukumbu za Bunge ambapo tarehe 9 Februari, 2021, kupitia utaratibu wa hati za kuwasilisha mezani, sheria ndogo hizi zikiwa sehemu ya nyongeza ya matoleo ya gazeti la serikali ziliwasilishwa mezani, Bungeni. Baadaye sheria ndogo

hizo zilipelekwa kwenye Kamati ya Sheria Ndogo na kuanza kuchambuliwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kulitaarifu Bunge kuwa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo yameisaidia Kamati kuja na taarifa hii itakayoliwezesha Bunge kuamua inavyostahili.

2.4 Matokeo ya Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi yanabainisha jumla ya dosari 119 zinazoripotiwa katika taarifa hii. Kwa urahisi wa kufuatilia dosari hizo, Taarifa hii imeambatisha Jedwali la Uchambuzi kwa rejea wakati wa mjadala na uamuzi. Kwa ujumla, mchanganuo wa dosari hizo unaonesha kuwa:

- (i) Sheria Ndogo moja (1) imekutwa na dosari ya kutozingatia masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- (ii) Jumla ya sheria ndogo tatu (3) zimekutwa na dosari ya kukinzana na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutungwa kwa sheria ndogo inayohusika;
- (iii) Sheria ndogo kumi na tano (5) zimekuwa na dosari ya kutoendana na misingi bora ya uandishi wa sheria (*drafting principles*)
- (iv) Sheria Ndogo kumi na moja (11) zimekosa uhalisia wa mambo na kutokuwa na urahisi wa utekelezaji wake; na
- (v) Jumla ya sheria ndogo nne (4) zimekutwa na makosa ya uandishi wa majedwali ya sheria ndogo inayohusika jambo linaloathiri utekelezaji wake.

2.4.1 Dosari ya kutozingatia masharti ya Katiba

Mheshimiwa Spika, nchini Tanzania, Katiba ni Sheria kuu ya nchi na ambayo mionganoni mwa kazi zake kuu na za msingi ni kugawa madaraka kati ya dola na jamii pamoja na mgawanyo wa madaraka mionganoni mwa mihimili ya serikali. Kwa maelezo hayo, sheria zote za nchi zinatokana na

mgawanyo wa madaraka uliowekwa na Katiba. Kutokana na ukoo wa Katiba, Bunge haliwezi na haliruhusiwi kutunga sheria au kuweka masharti ya sheria yanayokinzana na Katiba. Hali kadhalika, Bunge halina uwezo wa kuruhusu mamlaka nyingine kutunga sheria ndogo yenyé masharti yanayokiuka masharti ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Pili wa Bunge, yanadhihirisha sheria ndogo iliyokutwa na hoja ya kukinzana na masharti ya Katiba. Sheria hiyo ni **Sheria Ndogo za Kilimo na Hifadhi ya Chakula za Halmashauri ya Wilaya ya Itilima, 2020 (GN. NA. 1006/20 Novemba, 2020)** zilizotungwa chini ya **Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) (Sura 287)**. **Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 16 (d) cha sheria ndogo hizo, kinamshurutisha mfugaji kujiunga na vyama ufugaji. Sharti hilo linakinzana na masharti ya Ibara ya 20 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayohusu uhuru wa mtu kushirikiana na wengine. Bunge linapoweka katika sheria masharti yanayokabidhi kwa mtu ye yoyote au kwa idara yoyote ya Serikali madaraka ya kuweka Kanuni za nguvu ya kisheria au kuzipa nguvu ya kisheria Kanuni zozote zilizowekwa na mtu ye yoyote au idara yoyote ya Serikali, halithubutu kutoa uwezo wa kukiuka msharti ya Katiba. Kwa shauku hiyo, Bunge lako tukufu halitarajiwu kupuuza matumizi ya kifungu cha sheria ndogo kinachoshurutisha jambo liliopewa hiari na Katiba.

2.4.2 Kukinzana na Masharti ya Sheria inayotoa Mamlaka ya Kutunga Sheria Ndogo

Mheshimiwa Spika, Bunge linaporuhusu mamlaka inayohusika kutunga sheria ndogo, hufanya hivyo kwa madhumuni maalumu yanayoendana na lengo kuu la Sheria mama. Kwa sababu hiyo, Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, kinataka sheria ndogo yoyote inayotungwa iendane na masharti yaliowekwa kwenye Sheria mama. Hata hivyo, uchambuzi umeonesha kuwa baadhi ya sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Pili wa Bunge ziliikuwa na maudhui yanayotofautiana na masharti ya Sheria Mama au

Sheria Nyingine za Nchi. Jumla ya sheria ndogo tatu (3) zilibainika kuwa na dosari ya kukinzana na Sheria Mama.

Mheshimiwa Spika, Mfano wa sheria ndogo hizo ni *The Tanzania Teachers' Professional Board General, Regulations 2020* (GN. NA. 686/28 Agosti, 2020) ambazo zimetungwa chini Sheria ya *The Tanzania Teachers' Professional Board Act*, (Sura 314). Uchambuzi umebainisha kuwa, Kanuni ya 37(1) inaruhusu kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa bodi ya walimu ndani ya siku 30 baada ya kutolewa kwa uamuzi. Masharti hayo ya kukata rufaa yaliyowekwa na sheria ndogo, yanatofautiana na masharti yaliyoweka na Bunge katika Sheria mama ambayo ni Siku 90.

Mheshimiwa Spika, dosari hiyo imeweka masharti yanayopunguza siku za kukata rufaa zilizoruhusiwa na Bunge katika Sheria, Jambo ambalo linakinzana na sheria ya Tafsiri ya Sheria. Aidha, dosari hiyo inapunguza wigo wa haki uliotolewa na Bunge, jambo ambalo Bunge lako tukufu haliwezi kuruhusu. Madhara ya dosari hiyo ni kuminya haki kwa siku sitini (60) za mrufani kuweza kujianaa vema na rufaa yake dhidi ya uamuzi wa bodi ya walimu. Uminyaji huo wa siku umepora takriban asilimia 66.7 ya muda uliokuwa umetolewa na Bunge na hivyo, kuwa mionganoni mwa kero katika utekelezaji wa Sheria ya Bodi ya Kitaalamu ya Walimu Tanzania, Sura 314.

Mheshimiwa Spika, dosari nyingine ya sheria ndogo hii kutofautiana na sheria mama, inajitokeza katika Kanuni ya 37(3) inayompa Waziri mamlaka ya kuchagua Kamati mara baada ya kuwa amepokea rufaa. Bunge halikumpa Waziri mamlaka hayo ya kuunda Kamati ya Rufaa. Kifungu cha 49 cha sheria mama kimemtaka Waziri mwenyewe kuwa mamlaka ya rufaa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu wa kuchagua Kamati ya kushughulikia rufaa haupo kwa mujibu wa sheria mama, mamlaka anayopewa Waziri ya kuteua Kamati hiyo ni batili. Hii inatokana na masharti yanayowekwa na kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri kinalekeza kuwa sehemu ya sheria

ndogo inayokinzana na sheria mama itahesabika kuwa batili kama kinavyoeleza:

A subsidiary legislation shall not be inconsistent with the provisions of the written law under which it is made, or of any Act, and subsidiary legislation shall be void to the extent of any such inconsistency.

Mheshimiwa Spika, kwa masharti hayo ya Sheria ya Tafsiri, Kamati itakayoundwa na Waziri kushughulika rufaa itakuwa ni batili. Madhara ya dosari hiyo ni utekelezaji batili wa sheria iliyotungwa na Bunge hali inayoathiri matarajio ya utekelezaji wa sheria ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine wa sheria ndogo kukinzana na sheria mama ni sheria ndogo iitwayo, **Kanuni za Usajili wa maeneo ya Famasi, za mwaka 2020 (The Pharmacy (Premises Registration) Regulations, 2020 (GN. NA. 269/17 Aprili, 2020)** ambayo imetungwa chini ya **Sheria ya Famasi, Sura ya 311 (The Pharmacy Act, (CAP. 311)**. Kanuni hizi zilibainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya sheria mama iliyotungwa na Bunge mwaka 2011. Kanuni ya 2 inatoa tafsiri ya duka la jumla la kuuza dawa (*wholesale pharmacy*). Tafsiri hiyo inajumuisha ununuzi wa dawa kutoka kwa wazalishaji wa ndani (*local manufactures*) tofauti na tafsiri inayotolewa katika Kifungu cha 2 cha Sheria Mama.

Mheshimiwa Spika, tafsiri ya maneno " *wholesale pharmacy*" katika kanuni hiyo inasomeka:

"wholesale pharmacy" means a pharmacy that buys medicines, medical devices or cosmetics from importers or local manufacturers and sells in bulk to the retailer pharmacy." Tafsiri hiyo ni tofauti na ile inayotolewa na Sheria mama ambayo imetafsiri maneno " *whole sale pharmacy*" kwa kueleza kuwa:

"Wholesale pharmacy" means a pharmacy that buys medicines, medical devices or cosmetics from importers and sells in bulk to the retailer."

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kwamba, uandishi wa kuweka tafsiri inayojumuisha ununuzi wa dawa kutoka kwa

wazilishaji wa ndani (*local manufacturers*) una lengo jema la kuchochea soko la ndani. Nia njema hiyo, inapata dosari kwa mujibu wa Kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria. Kifungu hicho kinachohusu masharti ya jumla ya madaraka ya kutunga sheria ndogo, kinazuia sheria ndogo kukinzana na Sheria Mama. Dosari hiyo inaweza kusababisha mkanganyiko katika uelewa wa jumla wa sheria za nchi jambo linalopaswa kuepukwa na mamlaka kuu ya utungaji wa sheria.

2.4.3 Kutoendana na Misingi Bora ya Uandishi wa sheria

Mheshimiwa Spika, Sheria zinazotungwa na Bunge huzingatia misingi bora ya uandishi wa sheria. Kwa msingi huo, kipimo cha kuangalia uandishi bora wa sheria ni jambo kilizingatiwa wakati wa uchambuzi wa sheria ndogo. Matokeo ya uchambuzi yameonesha jumla ya sheria ndogo kumi na tano (15) zimekutwa na hoja zinazohusu misingi ya uandishi wa sheria. Mfano wa hoja hizo umebainika katika **Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru wa Madini ya Ujenzi) ya Halmashauri ya Wilaya ya Same, 2020 (GN. NA. 460/12 Juni, 2020)** ambazo zimetungwa chini ya **Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa (Sura 290)**.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 2 cha sheria ndogo hizo kinatoa tafsiri ya neno “madini ya ujenzi” kwa kuainisha aina kumi na mbili (12) za madini, yakiwemo madini ya chokaa. Hata hivyo **Jedwali la Pili la sheria ndogo** hizo linahusu ushuru na halitaji madini ya chokaa na ushuru.

Mheshimiwa Spika, Uandishi wa aina hiyo unaweza kuondoa uhalali wa kutoza ushuru wa madini ya chokaa na kuikosesha Halmashauri mapato yanayokusudiwa. Aidha, uandishi huo unaweza kusababisha halmashauri kutoza ushuru wa madini ya chokaa bila mwongozo wa viwango na kusababisha kero kwa wananchi. Bunge hili halipaswi na haliwezi kuona mazalio ya kero kwa wananchi wa Same au kwингineko na kutochukua hatua yoyote.

Mheshimiwa Spika, mfano mwagine wa sheria ndogo kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria ni sheria ndogo iitwayo, **Kanuni za Usajili wa Maeneo ya Famasi, za mwaka 2020 (The Pharmacy (Premises Registration) Regulations, 2020 (GN. Na. 269/17 Aprili, 2020)** ambayo imetungwa chini ya **Sheria ya Famasi, Sura ya 311 (The Pharmacy Act, (CAP. 311).** **Mheshimiwa Spika**, Kanuni hizo zimerejea **Kifungu cha 34 cha Sheria Mama** kama moja ya Kifungu kinachotoa mamlaka ya kutungwa kwa sheria ndogo hiyo. Hata hivyo, **Kifungu cha 34** hakihuksiki moja kwa moja na Mamlaka ya Waziri kutunga Kanuni hizo, badala yake kinaweka katazo la kufanya shughuli zinazohusu uuzaaji, utoaji na ugawaji wa dawa bila usajili. Dosari hiyo inaweza kuvuruga mantiki na madhumuni ya kifungu cha Sheria mama, jambo linaloweza kuwa na changamoto katika utekelezaji wa sheria mama.

2.4.4 Kukosa Uhalsia

Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika, utungaji bora wa Sheria huzingatia uhalsia katika utekelezaji ikiwemo hali halisi na mazingira ya watumiaji na walengwa wa sheria inayohusika. Uchambuzi umebaini jumla ya sheria ndogo kumi na moja (11) zenye hoja inayohusu dosari ya kuwa na vifungu visivyozingatia uhalsia. Mfano wa sheria ndogo zenye hoja hiyo ni **Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, 2020 (GN. NA. 1024/11 Disemba, 2020)** zilizotungwa chini ya (**Sheria ya Fedha ya Serikali ya Mitaa**) (**Sura 290**).

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi umebainisha kuwa **Sehemu ya 4 kipengele cha 8 cha Jedwali la Kwanza** inaweka sharti la malipo ya ada kwa shughuli za jando na unyago ya kiasi cha shilingi 20,000/- kwa tukio. Shughuli hizo si shughuli za kijamii na lengo lake ni kutoa mafunzo ya maisha ya kijamii kwa vijana. Ugharimiaji wa shughuli hizo mara nyingi ni kwa wanajamii kujibana kwa mambo mbalimbali ili kufanikisha azma ya mafunzo ya kijamii. Kwa sababu hiyo kutoza ushuru au malipo yoyote kwa shughuli za aina hiyo zinazotokana na wananchi kujibana ni jambo lisilo na maana yoyote kwa utekelezaji wa sheria na uendeshaji wa shughuli za umma kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, Bunge linapotunga Sheria na kuruhusu mamlaka nyininge itunge sheria ndogo, linatarajia mamlaka inayohusika itafanya hivyo kwa namna yene maana kwa jamii na kwa utekelezaji wa Sheria ya mama au Sheria nyininge ya nchi. Katu, Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi haliwezi kuachia mamlaka zilizoruhusiwa na sheria ya Bunge zitunge sheria ndogo zisizoakisi shabaha na madhumuni ya sheria mama.

Mheshimiwa Spika, tozo za ada ya shilingi 20,000/- kwa tukio la jando na unyago, si jambo lenye maana na mantiki yoyote katika maisha ya jamii zilizopo za wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto. Kuendelea kutumia sheria ndogo hizo na kuwatoza wananchi ada ya shughuli za jando na unyago ni kuongeza kero na adha kubwa kwa wananchi. Bunge hili haliwezi kuendeleza udhia kwa wananchi unaotokana na sheria kwa kuwa si dhamira ya utungaji wa sheria kutunga sheria zenye maudhi kwa watu.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine wa sheria ndogo zilizobainika kuwa na vifungu visivyo na uhalisia ni **Sheria Ndogo za (Ada za Vibali vya Burudani za Halmashauri ya Wilaya ya Moshi), 2020** (GN. NA. 529/10 Julai, 2020) ambazo pia zimetungwa chini ya **Sheria ya Fedha ya Serikali za Mita (Sura 290)** na **Kanuni za Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, 2020** zilizotungwa chini ya **Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, (Sura 230)**.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi umebainisha kuwa Sehemu D, kipengele cha 4 cha Jedwali la Kwanza la **Sheria Ndogo za (Ada za Vibali vya Burudani za Halmashauri ya Wilaya ya Moshi), 2020** kimeweka ada inayotatanisha. Kiwango kinachowekwa ni kuanzia shilingi 300,000/- hadi 1,000,000/- kwa ajili ya kibali cha kuonesha Cinema au video. Aidha, sharti la utozaji wa ada katika sheria ndogo hiyo pia limewekwa katika **Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza**, 2020. Sehemu ya tano ya Jedwali Tatu, imeweka ada ya kibali cha kuendesha shughuli za kuonesha filamu kuanzia shilingi 50,000/- hadi 500,000/- kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa sheria ndogo hizo kuanzisha ada zinazotozwa na mamlaka mbili tofauti katika chanzo kimoja ni jambo linaloharibu mantiki ya tozo hiyo na kuifanya ikose maana halisi katika maisha ya watu. Jambo hilo linaongeza ugumu wa shughuli hizo kwa jamii ya watu wenyewe kipato cha chini. Bunge halipaswi kuruhusu mamlaka ya kutunga sheria ndogo kwa kiwango cha kuleta karaha na maudhi kwa jamii ya watu wenyewe kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, sheria ndogo nyingine iliyobainika kuwa na maudhui yanayokosa uhalisia ni **Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Njombe 2020 (GN. NA. 777/18 Septemba, 2020)** zilizoanzishwa chini ya **Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, (Sura 290)**. Uchambuzi ulibainisha kwamba, **Sehemu ya Sita (VI) ya Jedwali la Kwanza kipengele cha 1 na Kipengele cha 5(c)** vinaweka sharti la malipo ya ushuru wa shillingi 1,000/- wa maegesho kwa pilkipiki na basi ndogo zisizozidi abiria arobaini na wanne (44).

Mheshimiwa Spika, utozaji huo wa viwango vya ushuru ulio sawa kati ya pilkipiki na basi lisilozidi abiria arobaini na wanne (44) yanakosa uhalisia unaolingana kutokana na tofauti ya ukubwa na matumizi ya vyombo hivi vya usafiri. Haikubaliki akilini kwa mtu mwenye busara ya kawaida kwamba wakati pilkipiki inapotoka eneo la maegesho linakuwa na msingi wa pato unaolingana na basi la abiria. Bunge haliwezi kutunga sheria inayokataana na busara ya kawaida na wala haliwezi kutunga sheria inayokasimu utungaji wa kanuni kwa kiwango cha kukinzana au kukosa uhalisia.

2.4.5 Makosa ya Uandishi wa Majedwali ya Sheria Ndogo

Mheshimiwa Spika, Uandishi mzuri wa sheria unawezesha sheria inayohusika kueleweke na kutekelezeka kama ilivyokusudiwa. Sheria ya Bunge inapokabidhi madaraka ya kutunga sheria ndogo, haikusudii kupuuza umuhimu wa uandishi wa sheria unaowezesha utekelezaji wake. Uandishi huo ni pamoja na uandishi fasaha wa majedwali ambayo kwa kawaida yanasaidia kutoa maelezo na ufanuzi wa kina wa kifungu au kanuni inayohusika.

Mheshimiwa Spika, majedwali katika sheria au sheria ndogo yatakuwa na maana iwapo yatawekwa kwa namna inayorejea kwa usahihi kifungu au kanuni wezeshi (*enabling provision*). Inapotokea Majedwali ya sheria yana dosari ya kutorejea Kanuni sahihi, kurejea Kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa Kanuni au Maudhui ya Jedwali kutofautiana na kifungu wezeshi au vifungu vingine vya sheria au sheria ndogo inayohusika, inaathiri mantiki, madhumuni na maudhui ya jumla ya sheria. Bunge hili tukufu halitakuwa tayari kuruhusu mamlaka zinazokabidhiwa uwezo wa kutunga sheria ndogo, litekeleza kwa namna isiyowezesha lengo na madhumuni ya sheria mama.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, uchambuzi wa sheria ndogo ulizingatia pia umuhimu wa sheria hizo kutokuwa na makosa ya uandishi katika majedwali. Matokeo ya uchambuzi yameonesha kuwa jumla ya sheria ndogo kumi na nne (14) zimekuwa na hoja zinazohusu dosari katika uandishi wa majedwali. Mfano wa dosari hizo unaonekana katika sheria ndogo ya *The Valuation and Valuers Registration (Training Examination) Rules 2020 (GN. NA. 282/28 Agosti 2020)* ailiyotungwa chini *Sheria ya The Valuation and Valuers Registration Act, (Sura 138)*. Jedwali la Pili linaoneshwa kuwa limeanzishwa chini ya Kanuni ya 32(2) ambayo haipo. Kosa hilo la uandishi linaning'iniza Jedwali katika mtiririko wa uandishi na kuharibu azma ya ufanuzi uliokusudiwa. Dosari nyingine ya sheria ndogo hii, ni **Kanuni ya 34 (2)** kurejea Jedwali la Pili ambalo halioneshi kama limeanzishwa chini ya Kanuni hii.

Mheshimiwa Spika, dosari ya kutorejea vifungu sahihi sio tu inaondoa maana ya masharti ya Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria ambacho kinatambua Majedwali kuwa ni sehemu ya sheria, bali pia inaleta changamoto katika usomaji mzuri wa sheria husika na wakati mwingine kusababisha mkanganyiko. Bunge halitaacha kuzisisitiza mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga kanuni au sheria ndogo nyingine kuzingatia uandishi bora wa Majedwali katika sheria.

Mheshimiwa Spika, mfano wa tatu wa dosari za uandishi wa majedwali unadhihirika katika **Kanuni za Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, 2020 (GN. NA. 488/26 Juni, 2020)** ambazo zimetungwa chini ya **Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, (Sura 230)**. Kipengele cha 14 cha Jedwali la Kwanza katika Kanuni hizi kinaweka utafiti wa mambo ya filamu katika orodha ya mambo yanayopaswa kuombewa kibali cha Bodi ya Filamu pasipo kuonesha iwapo utafiti unaokusudiwa unahusisha pia watu wanaoandika tasnifu (*thesis*) baada ya utafiti wa kitaaluma kuhusu filamu katika fani za sanaa au nyinginezo. Tatizo katika uandishi huu ni kutokutoa ufanuzi unaoonesha kama tafiti za kitaaluma hazibanwi na masharti ya Kanuni hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Majedwali hulenga kutoa ufanuzi zaidi wa maudhui yaliyo katika vifungu vya sheria, kitendo cha kuweka maudhui ambayo hayajelezi bayana katika Majedwali inasababisha kutokueleweka kwa mantiki ya maudhui sehemu inayohusika katika sheria hivyo inasababisha kutofikiwa malengo yaliyokusudiwa na sheria.

2.4.6 Wadau muhimu kutoshirikishwa katika mchakato wa utungaji wa Kanuni za Bodi ya Ualimu

Mheshimiwa Spika, ushirikishaji wa wadau na hasa wale wanaoguswa moja kwa moja na sheria au kanuni inayotungwa ni jambo linalozingatia umuhimu wa mtazamo wa wengi (*popular perspective*). Bunge kwa upande wake limeweka sharti la kuwashirikisha wadau wakati wa utungaji wa sheria kama inavyoelekeza Kanuni ya 97(2) na 136(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni 2020. Kwa uzito huo huo, Kamati ilipokutana na mamlaka zilizokabidhiwa jukumu la kutunga sheria ndogo, ilitaka pia kujua iwapo mchakato wa utungaji wa sheria ndogo ulizingatia umuhimu wa kuwashirikisha wadau.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa mchakato wa kutengeneza Kanuni za Bodi ya Ualimu, 2020 ulihusisha mamlaka mbalimbali serikalini bila kuwashirikisha wadau waliotarajiwa kuguswa moja kwa moja na masharti ya Kanuni

hizo. Katika majadiliano ilibainika kuwa wadau kama vile Chama cha Walimu Tanzania (CWT) na mashirika yanayojihusisha na masuala mbalimbali ya walimu hawakushirikishwa, hivyo kusababisha masuala muhimu yanayowahusu walimu kutowekwa katika Kanuni au kuwekwa kwa namna inayoweza kuleta changamoto katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Bunge halitaacha kuona haja kwa mamlaka inayohusika na Kanuni za Bodi ya Kitaaluma ya Walimu kuona haja ya kukaa na wadau mbalimbali wanaoguswa na Kanuni ili kupata mawazo jumuishi kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa Kanuni hizo.

2.4.7 Dosari ya Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza kuwa na makatazo kwa namna inayotatanisha utekelezaji wake

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kwa uandishi wa sheria kutokuweka masharti ambayo yanaweza kuleta utatanishi katika utekelezaji wake. Uchambuzi wa Kamati imebaini **Kanuni ya 16 ya Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza, 2020** imetaja makatazo mbalimbali ya maudhui mabaya katika filamu. Kamati inaona kuwa mantiki ya zuiola maudhui hayo ni kana kwamba Kanuni zinazuia uigizaji wa filamu zinazohusu masuala kama vile ulevi, matumizi ya dawa za kulevya, ukahaba. Hali hiyo, inayoweza kudumaza uigizaji kwenye vipengele (*segments*) vyenye lengo la kuonesha uhalisia na kutoa mafunzo kwa jamii. Msisitizo wa Bunge ni kuona haja ya kufanya marekebisho katika sehemu hiyo ili kuondoa baadhi ya maneno yanayoonesha hali ya kukataza moja kwa moja uigizaji wa masuala yenye mtazamo hasi yanayofikisha ujumbe kwa jamii.

2.4.8 Dosari ya Msisitizo katika udhibiti na tozo zaidi kuliko ufanuzi na mwongozo

Mheshimiwa Spika, mamlaka zinazoanzishwa kusimamia tasnia mbalimbali pamoja na malengo mengine, pia huangalia namna bora ya ustawi wa tasnia wanazosimamia

kwa kuweka miongozo, ufanuzi na kutengeneza mazingira yanayowezesha utekelezaji wa masuala mbalimbali katika tasnia zinazohusika. Kamati imebaini kuwa, Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza, 2020 zimejielekeza zaidi katika udhibiti na kuweka tozo nyingi ikilinganishwa na kutoa ufanuzi na miongozo mbalimbali. Hali hiyo haisaidii kuilea, kuistawisha na kuipa tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza viwango vinyavokubalika nchini.

Mheshimiwa Spika, upo umuhimu kwa mamlaka zinazosimamia tasnia mbalimbali na hasa zinazohusisha vijana wengi nchini, kutunga Kanuni zinazotoa miongozo na ufanuzi wenyewe lengo la kustawisha shughuli zao. Hali hii itachochea ajira nyingi kwa vijana nchini.

2.4.9 Ushirikiano katika Masuala yanayohusu Wizara zaidi ya moja

Mheshimiwa Spika, inatarajiwa kwamba pale ambapo kuna masuala mtambuka, Mamlaka zinazohusika zitawasiliana ili kuhuisha masuala wanayoyasimamia kwa pamoja. Kufanya hivyo, kutasaidia kuepuka changamoto katika usimamiaji wa mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza, 2020 zilizo chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na sheria ndogo za (Ada za Vibali vya Burudani) za Halmashauri mbalimbali nchini chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa pamoja zinatoza ada za vibali vya kuendesha kumbi za cinema/video na michezo ya kuigiza. Utozaji huo, unaweka ugumu katika utekelezaji wa shughuli hizo katika jamii ya watu wenyewe kipato cha chini. Ugumu huo, unaongeza kero kwa wananchi kinyume na matarajio ya Bunge lilipotunga Sheria mama.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako tukufu halitarajii kuona mamlaka zinazotekeleza majukumu yanayoingiliana zifanye kazi pasipo kushirikiana, ili kuondoa uwezekano wa kuleta kero kwa wananchi wanaoguswa na shughuli zinazosimamiwa na mamlaka zaidi ya moja.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI

3.1 Maelezo

Mheshimiwa Spika, maelezo yote niliyoyatoa kabla ya sehemu hii, yanaonesha kuwa sheria ndogo hutungwa mara kwa mara kulingana na mahitaji yanayojitekeza. Hali hiyo inachangia utungaji wa sheria ndogo kwa kiasi kikubwa na haja ya utaratibu madhubuti wa kuhifdhni na kulinda heshima ya mamlaka ya kutunga sheria nchini. Bunge ambalo ni chombo kikuu cha utungaji wa sheria linaendelea kuwa na wajibu wa kuangalia utekelezaji wa madaraka ya kutunga sheria. Kwa kuwa Bunge hufanya kazi kwa kutumia Kamati zake, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya sheria ndogo yenye jukumu la kuchambua sheria ndogo, imetekeliza majukumu yake na kuonesha matokeo ya uchambuzi niliyofafanua.

3.2 Maoni

Mheshimiwa Spika, kutokana na matokeo hayo, Kamati ina maoni katika maeneo makuu matano yaliyojitekeza kama ifuatavyo:-

3.2.1 Uzingatiaji wa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977

Mheshimiwa Spika, kutozingatiwa kwa misingi inayowekwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika uandishi wa sheria ndogo ni jambo linaloweza kusababisha mifumo, taasisi na muelekeo wa jamii kutoendana na misingi ya Katiba. Hali hiyo, ni kinyume na inavyopaswa kuwa, ambapo masharti ya Katiba ni chimbuko la sheria zote za nchi.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa ukiukwaji wa misingi ya utawala bora, ukiukwaji wa upatikanaji wa haki mbalimbali zikiwemo haki za kisiasa, kiuchumi na kijamii unaweza kutokea kutokana na dosari hiyo.

3.2.2 Kutokinanza na masharti ya sheria mama

Mheshimiwa Spika, dosari ya sheria ndogo kukinzana na sheria mama inaathiri tija ya utekelezaji wa Sheria. Dosari hiyo

ikiendelea, masharti yaliyowekwa kwenye sheria mama kwa lengo la kuiwezesha mamlaka inayohusika kutunga sheria ndogo yatacosa maana katika utekelezaji wa sheria. Hali hiyo ni kinyume na misingi ya utungaji wa sheria. Ni maoni ya Kamati kuwa, Bunge haliwezi kupuuza misingi ya utungaji wa sheria nchini.

3.2.3 Uzingatiaji wa Misingi ya Uandishi bora wa Sheria (Drafting Principles)

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa sheria zote kuendana na misingi ya uandishi bora wa sheria, dosari za sheria ndogo kutoendana na utaratibu bora wa uandishi wa sheria, si jambo la kuachwa katika sheria ndogo. Dosari hizo zinaweza kuwa dalili mbaya za utekelezaji wa sheria kwa kusababisha sheria mama isieleweke vizuri. Hali hiyo si jambo linaloweza kupuuzwa na Bunge.

3.2.4 Uhaliwa wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vyta adhabu na faini

Mheshimiwa Spika, Sheria ndogo kukinzana na uhaliwa kwa kuwa na maudhui yasiyozingatia hali ya uchumi wa walengwa, zinaweza kuathiri utekelezaji na kusababisha matokeo mabaya ya sheria. Sheria ndogo zinapoweka viwango vikubwa vyta faini, ada, ushuru na adhabu kuliko uwezo na hali halisi zitakosa maana katika jamii na zitakinzana na busara inayozingatiwa na Bunge wakati wa utungaji wa sheria. Bunge linapaswa kujiridhisha na kuhakikisha kuwa, dosari za sheria ndogo za kutoendana na uhaliwa zinarekebishwa.

3.2.5 Usahihi na ufasaha wa uandishi wa majedwali ya sheria ndogo inayohusika

Mheshimiwa Spika, matumizi ya majedwali katika uandishi wa sheria ndogo ni jambo la kuzingatiwa katika uchambuzi wa sheria. Ni kawaida kuwa majedwali hutumika kutoa maelezo au ufanuzi wa ziada wa vifungu au kanuni katika

sheria ndogo. Majedwali husaidia kudhihirisha taarifa za kina za jambo linalorejeshwa kwenye jedwali ili kuweka mtiririko nadhifu unaowezesha sheria kueleweka. Kwa sheria ndogo kuwa na dosari ya uandishi wa Majedwali inaathiri ukamiliifu wa sheria na kutatiza utekelezaji wa masharti yanayowekwa na vifungu vinavyohusika.

SEHEMU YA NNE

4.0 HOJA NA MAPENDEKEZO

4.1 Maeleo

Mheshimiwa Spika, Baada ya kutoa maeleo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu lizingatie maeleo ya jumla niliyoyatoa, ufanuzi wa matokeo ya uchambuzi na maoni ya Kamati ili kujadili na kutoa umuzi wa hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Ikumbukwe kuwa hoja hii inahusu eneo muhimu la utekelezaji wa sheria ambalo lisipoangaliwa kwa umakini linaweza kuwa mazalio ya kero, karaha na manung' uniko mionganoni mwa jamii.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja katika maeneo makuu matatu kama ifuatavyo.

4.2 Hoja za Jumla

Mheshimiwa Spika, kutohana na yaliyobainika wakati wa uchambuzi, hoja ya Kamati inayohusu dosari za jumla zinazoendelea kujitokeza katika sheria ndogo, inatokana na jukumu la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali la kuhakiki sheria ndogo. Kamati inatoa hoja kwamba:

KWA KUWA, dosari za jumla kuhusu uandishi na utungaji wa sheria ndogo zimeendelea kujitokeza, jambo linalotofautiana na matarajio yatokanayo na nafasi ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kuhakiki sheria ndogo,

NA KWA KUWA, kubainika kwa dosari hizo mara kwa mara kunaashiria mawasiliano duni baina ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na mamlaka zilizotunga sheria ndogo

zinazohusika, hali inayoathiri mafanikio ya utungaji na utekelezaji wa sheria ndogo,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iendelee kufuatilia mawasiliano na kuhakiki ipasavyo sheria ndogo zinatungwa ili kupunguza uwezekano wa dosari katika sheria hizo.

4.3 Hoja kuhusu Maudhui na uandishi wa Sheria Ndogo

4.3.1 Uzingatiaji wa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977

KWA KUWA, baadhi ya sheria ndogo zilizochambuliwa zimekutwa na dosari ya kuwa na msharti yanayokiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano, jambo lisiloweza kuafikiwa na Bunge,

NA KWA KUWA, Kutorekebishwa kwa sheria ndogo hizo kunaweza kusababisha ukiukwaji wa misingi ya utawala bora, ukiukwaji wa upatikanaji wa haki mbalimbali zikiwemo za kisiasa, kiuchumi na kijamii zilizowekwa kwa mujibu wa Katiba ya nchi na kuathiri ustawi wa wananchi,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka iliyotunga sheria ndogo ziliziokutwa na dosari ya kukinzana na masharti ya Katiba, zirekebishe dosari hizo inavyostahili.

4.3.2 Kukinzana na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutungwa kwa sheria ndogo

KWA KUWA, baadhi ya sheria ndogo zilizochambuliwa zimebainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi, jambo linaloweza kuathiri tija ya utekelezaji wa Sheria mama inayohusika,

NA KWA KUWA, sheria inayokinzana na sheria mama au sheria nyingine za nchi, inakaidi masharti ya sheria ya tafsiri ya sheria, hali inayosababisha sheria ndogo hiyo kuwa batili kwa mujibu wa Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizotunga sheria ndogo zilizobainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine, zirekebishe sheria ndogo hizo.

4.3.3 Kutozingatia Misingi ya Uandishi Bora wa Sheria (Drafting Principles)

KWA KUWA, uchambuzi umebainisha sheria ndogo zenye dosari mbalimbali za kutozingatia misingi ya uandishi bora wa sheria (*Drafting Principles*);

NA KWA KUWA, Dosari hizo zinaweza kuwa dalili mbaya za utekelezaji wa sheria na kusababisha sheria mama isieleweke vizuri, hali inayoathiri utekelezaji wa sheria iliyotungwa na Bunge,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga sheria ndogo zenye dosari za kutozingatia misingi ya uandishi bora wa sheria zirekebishe dosari hizo.

4.3.4 Dosari ya Uandishi wa Majedwali ikilinganishwa na Vifungu vya Sheria

KWA KUWA, baadhi ya sheria ndogo zilizochambuliwa zimebainika kuwa na dosari mbalimbali katika uandishi wa majedwali ambayo hutoa ufanuzi wa ziada wa vifungu au kanuni katika sheria ndogo,

NA KWA KUWA, dosari ya uandishi wa Majedwali kwenye sheria ndogo inaathiri ukamilifu wa sheria na kutatiza utekelezaji wa sheria inayohusika kutookana na Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kuyatambua majedwali kuwa sehemu ya Sheria,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga sheria ndogo zilizobainika kuwa na dosari za uandishi wa majedwali zirekebishe dosari hizo.

4.3.5 Masharti yasiyo na uhalisia

KWA KUWA, zimebainisha sheria ndogo zilizo na dosari ya kuweka vifungu vyenye masharti yanayokinzana na uhalisia kutokana na kuwa na maudhui yasiyozingatia hali ya uchumi wa walengwa wala uwezekano wa utekelezaji wake,

NA KWA KUWA, dosari hizo zinaweza kuathiri utekelezaji na kusababisha matokeo mabaya ya sheria, kama vile kuweka viwango vikubwa nya faini, ada, ushuru na adhabu kuliko uwezo na hali halisi, hali inayoongeza kero kwa wananchi na kuzuia ustawi wa maisha yao,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizopewa madaraka ya kutunga sheria ndogo zilizobainika kuwa na dosari za kutoendana na uhalisia zirekebishe dosari hizo.

4.4 Hoja kuhusu Sheria Ndogo Mahsus

4.4.1 Wadau muhimu kutoshirikishwa katika mchakato wa utungaji wa Kanuni za Bodi ya Kitaaluma ya Walimu

KWA KUWA, ushirikishaji wa wadau katika utungaji wa sheria yoyote unawezesha mawazo jumuifu na kurahisisha utekelezaji bora wa sheria inayohusika, lakini mchakato wa utungaji wa Kanuni za Bodi ya Kitaaluma ya Walimu, 2020 umebainika kutowashirikisha wadau wanaoguswa moja kwa moja na sheria hizo,

NA KWA KUWA, Kutowashirikisha wadau wanaoguswa moja kwa moja na Kanuni hizo, kunasababisha changamoto ya utekelezaji ikiwemo kutoeleweka vizuri, manung'uniko ya wadau na kutotambulika kwa manufaa ya Kanuni hizo,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka iliyokabidhiwa madaraka ya kuweka Kanuni za Bodi ya Kitaaluma ya Walimu, ikutane na wadau wa sekta ya elimu wanaoguswa moja kwa moja na Kanuni hizo ili kupata maoni yao kabla ya kuziboresha na kuripoti matokeo ya kazi hiyo.

4.4.2 Dosari ya Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza kuwa na makatazo kwa namna inayotatanisha utekelezaji wake

KWA KUWA, imebainika kukosekana kwa ufanuzi bayana wa makatazo ya Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza, ikiwemo kuzuia uigizaji wa ulevi, matumizi ya dawa za kulevy, ukahaba na mengineyo kwa namna ya kukataza kama vile haikatazwi,

NA KWA KUWA, kukosekana kwa ufanuzi bayana wa maudhui ya Kanuni hizo kunatatanisha utekelezaji wake, jambo linaloweza kusababisha uonevu na kuathiri ubora wa sanaa ya uigizaji,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, maneno yanayoonesha hali ya kukataza moja kwa moja uigizaji wa masuala yenye mtazamo hasi kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa jamii yarekebishwe katika Kanuni hizo.

4.4.3 Dosari ya Msisitizo katika udhibiti na tozo zaidi kuliko ufanuzi na mwongozo

KWA KUWA, uchambuzi umebainisha dosari ya Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza kujikita katika maudhui ya kuweka tozo na kudhibiti, kuliko kuweka miongozo yenye lengo la kuilea na kuistawisha tasnia hiyo,

NA KWA KUWA, hali hiyo inaweza kudhoofisha ukuaji wa tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza ambayo imeajiri idadi kubwa ya vijana nchini na kuchangia kwa kiasi fulani kupunguza tazito la ukosefu wa ajira kwa vijana,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, serikali iangalie namna ya kuboresha Kanuni hizi ili zitoe miongozo ya kuboresha tasnia za filamu na michezo ya kuigiza kwa lengo la kuchochera ushiriki wa vijana wengi.

4.4.4 Ushirikiano katika Masuala yanayohusu Wizara zaidi ya moja

KWA KUWA, Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza, 2020 zilizotungwa na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Sheria Ndogo za (Ada za Vibali vya Burudani) za Halmashauri mbalimbali nichini chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, kwa pamoja zinatoza ada za vibali vya kuendesha kumbi za sinema/video na michezo ya kuigiza;

NA KWA KUWA, utozaji huo unaweka ugumu wa utekelezaji wa shughuli hizo katika jamii ya watu wenye kipato cha chini, jambo ambalo linaongeza kero kwa wananchi kinyume na matarajio ya kuboresha ustawi wao,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo zikae ili kuona namna ya kuhuisha viwango vya ada za kumbi za kuoneshea sinema na michezo ya kuigiza.

MWISHO

- 5.0 HITIMISHO**
- 5.1 Shukrani**

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Bunge lako tukufu kwa kuweka utaratibu wa taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika Bunge lako tukufu. Ni matumaini yangu kwamba, utaratibu huu utakuwa endelevu na umuhimu wa Kamati hii katika maendeleo ya nchi yetu utaonekana kwa kuwa kwa kiasi kikubwa sheria ndogo ndizo zinagusa maisha ya kila siku ya wananchi wengi.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa naomba nimshukuru Mhe. Jenista Mhagama (MB) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu) kwa kuendelea kuweka uratibu mzuri wa kuwasilisha Mezani Magazeti ya Serikali pamoja na viambatisho vyake (Sheria Ndogo) kwa wakati, pia uratibu mzuri wa uwasilishaji wa Jedwali la Uchambuzi kwa Wizara husika ambazo sheria

ndogo zake zimebainika kuwa na dosari. Hali hii kwa muda wote imekuwa ikiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Aidha, niwashukuru Mawaziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wa Wizara kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati na pia kwa kuanza hatua za utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ili kuondoa dosari mbalimbali zilizojitokeza katika sheria ndogo. Kwa heshima na taadhima naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

5.1.1 Mawaziri

1. Mhe. Jenista Mhagama (Mb) – **Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu;**
2. Mhe. William Lukuvi (Mb) – **Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.**
3. Mhe. Prof. Joyce Ndalichako (Mb) – **Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia;**
4. Mhe. Ummy Mwalimu (Mb) – **Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI);**
5. Mhe. Dotto Biteko (Mb) – **Waziri wa Madini;**
6. Mhe. Dkt. Doroth Gwajima – **Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;**
7. Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) – **Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na**
8. Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb) – **Waziri wa Maliasili na Utalii.**

5.1.2 Naibu Mawaziri

1. Mhe. Dkt. Angeline Mabula – **Naibu Waziri, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

2. Mhe. Abdallah Ulega (Mb) – aliyejkuwa **Naibu Waziri, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo;**
3. Mhe. Dkt. Festo Dugange (Mb) – **Naibu Waziri , Ofisi ya Rais – TAMISEMI;**
4. Mhe. Mary Masanja – **Naibu Waziri, Wizara ya Maliasili na Utalii; na**
5. Mhe. Omary Kipanga – **Naibu Waziri, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.**

5.1.3 Wadau

Mheshimiwa Spika, aidha niwashukuru wadau mbalimbali waliofika mbele ya Kamati tarehe 19 Machi, 2021 kwa ajili na kutoa maoni katika **Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza, 2020** na wale waliofika mbele ya Kamati tarehe 12 na 13 Aprili, 2021 kwa lengo la kutoa maoni yao katika **Kanuni za Bodi ya Kitaaluma ya Walimu, 2020** na **Kanuni za Wathamini, 2020**. Maoni yao kwa kiasi kikubwa yameisaidia Kamati kufanya uchambuzi wa kina katika Kanuni hizo. Naomba kipekee niwatambue wadau kama ifuatavyo;

1. Shirikisho la Filamu Tanzania;
2. HAKIELIMU;
3. Chama cha Walimu Tanzania;
4. (*Association of Real Estate Professionals of Tanzania (AREPTA)*); na
5. UWEZO TANZANIA.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Pili wa Bunge na hatimaye kufanikisha kazi hii. Kwa heshima kubwa naomba majina yao yaingie katika kumbukumbu rasmi za Bunge (*Hansard*):-

1. Mhe. Dkt. Jason Samson Rweikiza, (Mb) – **Mwenyekiti;**
2. Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete, (Mb) – **M/Mwenyekiti;**
3. Mhe. Ramadhan Suleiman Ramadhan, (Mb);

4. Mhe. Idrissa Juma Abdul-Hafar, (Mb);
5. Mhe. Simai Hassan Sadiki, (Mb);
6. Mhe. Sylvia Francis Sigula, (Mb);
7. Mhe. Emmanuel Mageni Kasalali, (Mb);
8. Mhe. Ndaisaba George Ruhoro, (Mb);
9. Mhe. Edwin Enosy Swalle, (Mb);
10. Mhe. Judith Salvio Kapinga, (Mb);
11. Mhe. Santiel Erick Kirumba, (Mb);
12. Mhe. Jacob Tarimo Priscus, (Mb);
13. Mhe. Regina Ndege Qwaray, (Mb);
14. Mhe. Esther Edwin Malleko, (Mb);
15. Mhe. Amour Khamis Mbarouk, (Mb);
16. Mhe. Esther Lukago Midimu, (Mb);
17. Mhe. Minza Simon Mjika, (Mb);
18. Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda, (Mb);
19. Mhe. Khamis Ali Vuai, (Mb); na
20. Mhe. Nicholaus George Ngassa, (Mb).

Mheshimiwa Spika, aidha napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* Katibu wa Bunge kwa ushirikiano wanaopatia Kamati hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, nimshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, *ndc* akisaidiwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Gerald Magili, kwa usimamizi mzuri wa shughuli za Kamati. Mwisho lakini si kwa umuhimu, niwashukuru Makatibu wa Kamati ya Sheria Ndogo Ndg. Mkuta Masoli na Ndg. Stanslaus Kagisa, wakisaidiwa na Bi. Imelda Ntimba Msaidizi wa Kamati kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

5.2 Kutoa hoja

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Dkt. Jason Samson Rweikiza, Mb

MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO

28 Juni, 2021

(Hoja imetolewa lamuliwe)

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete kwa kusoma vizuri taarifa ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, tutakumbuka kwamba tulikubaliana siku za nyuma na kwa hiyo tukarekebisha Kanuni zetu kukaa vizuri kwamba Kamati ya Sheria Ndogo ndio Kamati pekee ambayo inawasilisha taarifa zake mara mbili kwa mwaka kwa sababu ya umuhimu wa Kamati hiyo, umuhimu wa sheria ndogo katika utawala bora wa nchi yetu lakini pia kwamba tukizirundika zile sheria ndogo zote zikae mwaka mzima ndio taarifa moja itolewe, taarifa hiyo ingebidi iwe kubwa sana. Kwa hiyo, ndio maana tunakata kipande na kama walivyosema tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Jenista kwa ushirikiano mkubwa ambao anaipa Kamati, tunashukuru sana na nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati hiyo, hii ni Kamati ya watu watulivu ambao muda wote wao wanakaa hapa Dodoma na kufanya kazi zao hapa. (*Makof*)

Sasa ninao wachangiaji, tungepende mchana tumalize shughuli zetu za Bunge kusudi baada ya hapo tuendelee na yale mambo ambayo tulitangaza mapema, wengine waende Msekwa, wengine *St. Gasper*. Kwa hiyo, tutaenda na uchangiaji lakini tutahakikisha by saa 7.00, 7:15 mchana, hatufiki 7:30 mchana tuwe tumemaliza shughuli za leo.

Naomba nianze na uchangiaji sasa, Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle na atafuatiwa na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan. Nafikiri tupeane kama dakika saba hivi zinatosha.

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia taarifa ya Kamati hii ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kukushukuru sana wewe kwa kuniamini na kunitfea kuwa kwenye Kamati hii ya Sheria Ndogo ya Bunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kama ulivyo sema kwenye utangulizi, kwa mujibu na mifumo ya nchi yetu, sheria ndogo ndio sheria ambazo zinagusa kwa kiasi kikubwa wananchi walio wengi kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, na nitumie nafasi hii kuipongeza sana Kamati ya Sheria Ndogo kwa kufanya kazi kubwa sana katika uchambuzi wa sheria hizi ambazo katika uchambuzi huo imebainika dhahiri kwamba kulikuwa na dosari muhimu za kurekebisha hasa kwenye kulinda tasnia ya sanaa, tasnia ya walimu, tasnia ya watu wa bodaboda na wananchi mbalimbali kwenye kilimo na kadhalika. Kwa hiyo, niwapongeza sana Kamati ya Sheria Ndogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kamati na ripoti ambayo imetolewa hapa ni dhahiri kwamba ziko changamoto mbalimbali hasa kwenye ushirikishwaji wa wananchi kwenye kutoa maoni kwenye sheria hizi ndogo. Sote tunajua kwamba katika nchi yetu yapo maeneo kadhaa kumekuwa na mvutano na wafanyabishara wadogo pamoja na watu wa bodaboda wakilalamikia baadhi ya sheria ambazo zimekuwa zikitungwa na mamlaka ambazo zinatunga sheria ndogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali na mamlaka ambazo zinahusika na utungaji wa sheria hizi ndogo ni vizuri sheria hizi kwa sababu walaji na waathirika wa sheria hizi ni wananchi wa kule chini, kabla ya sheria kuanza kutekelezwa ni muhimu sana wadau hawa wakasikilizwa na ndiyo maana kwenye ripoti ya Kamati imeabainika dhahiri kwamba kwenye Sheria ya Bodi ya Walimu kwa mfano walimu walikuwa na maoni yao ya msingi sana ya kuboresha Bodi ya Taaluma ya walimu. Lakini kwa sababu tu ya kutokushirikishwa vizuri na kutoa maoni yao kwa ufasaha kumeleta mvuta usiokuwa wa lazima na kupelekea Kamati

ya Sheria Ndogo kutoa mapendekezo ambayo imewatoa ndani ya Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni muhimu kwenye siku za usoni, mamlaka hizi za kutunga sheria ndogo wafahamu kwamba sheria hizi ni kama huduma kwa wale walaji wasiposhirikishwa wale ambao ndiyo sheria inawagusa inaleta shida nydingi sana kwenye maeneo mbalimbali. Na ndiyo maana Kamati ilibaini mfano; kule Mbeya kulikuwa na sheria ndogo ambayo ilikuwa inaweka faini kwa watu wa bajaji kwenye fedha ambayo ni karibu sawa na mtu anayemiliki basi.

Sasa sheria hizi kama ambavyo kamati imebainisha ni kwamba hazina uhalisia wa mazingira ya wananchi na biashara ambazo wanafanya. Kwa hiyo, ni rai yangu mimi kama Mbunge basi mamlaka za kutunga Sheria ziweke mazingira ya wazi ili sheria zisiwe na malalamiko makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia kama ambavyo taarifa ya Kamati imesema, imeonesha ndani ya sheria ambazo zimefika kwenye Kamati kulikuwa na shida ya kiuandishi kwenye sheria karibu 15. Hii tafsiri yake nini? Na nimaoni yangu mimi kama Mbunge pengine mamlaka ambazo zimekasimiwa kutunga hizi sheria ndogo ni vema wakawa na muda wa kutosha wa kupitia sheria inayohusu utungaji wa sheria ndogo kwa ufasaha ili kusudi kuipunguzia mzigo kamati wa kuchambua kazi ambayo ingefanywa na mamlaka husika kwenye utungaji wa sheria yenywewe. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ni vyema basi kwenye siku za usoni ambako tutakwenda baadaye na nimuombe sana Waziri wetu wa Sera Bunge, Kazi na Ajira Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na kazi nzuri ambayo anafanya ya kusimamia utaratibu mzuri wa sheria ndogo basi asaidie pia hizi mamlaka zinazotunga sheria ndogo wajitahidi sana kufuata utaratibu ambao tumejiwekea kama nchi kwa ajili ya ustawi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kulichangia kwa mujibu wa taarifa ambayo imetolewa hapa ni kuhusu hoja mahususi ya hizi sheria zinazohusu watu wa filamu. Kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ni dhahiri kwamba sanaa ya muziki nchini ni sanaa inayaoajiri vijana wengi sana na vijana hawa wanafanya kazi hizi kwa ubunifu wao wenyewe, ni rai yangu kama Mbunge kwamba sekta ya sanaa nchini inahitaji kupewa ulezi na nafasi ya kukuzwa badala ya kuwekewa mazingira ya kudidimiza.

Kwa hiyo, ushauri ni kwamba Serikali ichukue hatua, inapotunga sheria za kusimamia sekta hii ya sanaa na muziki nchini basi sheria zake ziweke mazingira ya kuhamasisha sekta badala ya kuwavunja moyo wasanii wetu nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na nimatumaini yetu kwamba kama sekta hii ya muziki na sanaa itakuzwa kwa kiasi kikubwa itachangia sana kwenye pato la Serikali, lakini pia itachangia ajira kwa vijana wengi ambao nchi nzima sasa hivi wanafanya ubunifu katika sanaa na muziki. Kwa hiyo, niipongeze sana kamati kwa kazi nzuri walioyoifanya kwa ajili ya kuboresha kanuni za kusimamia filamu sanaa pamoja na muziki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia niwapongeze upande wa Serikali kwa Mawaziri ambao walienda kwenye Kamati ni dhahiri kwamba walitoa ushirikiano mzuri sana na hii imetoa picha kwamba dhamira ya Serikali imekusudia kuboresha maisha ya Watanzania na kuwapeleka Watanzania katika maisha bora zaidi. Kwa hiyo, hili ni jambo jema na niipongeze sana kwa hiyo kwa sababu ni sura nzuri, kwamba kama Taifa sasa na Serikali inatazama zaidi maslahi ya wananchi walioko kule chini ili kusudi kama Taifa tuweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Waziri wa Elimu Profesa Ndalichako, kwenye Kamati hii ya Sheria Ndogo ameeleza vizuri sana utayari wake wakushirikisha wadau mbalimbali kwa ajili ya sekta ya elimu na tumeona wiki iliyopita ameanza kutekeleza kwa kuanza kukaa na wadau mbalimbali kwenye hii sekta ya elimu katika kutekeleza maoni ya Kamati ambayo

imeanza kuyatoa hii ni sura nzuri na tukiendelea hivi kama Bunge basi mbele ya safari kazi itakuwa nzuri na nyepesi sana.

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Spika, baada ya hayo nakushukuru sana naunga mkono ripoti ya Kamati. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Edwin Swalle kwa kutuanzishia mjadala huu. Nimeshakutaja Mheshimiwa Ramadhani Suleiman Ramadhani na kengele inalia moja tu baada ya dakika saba, Mheshimiwa Suleiman na atafuatiwa na Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray.

MHE. RAMADHANI SULEIMAN RAMADHANI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia kwenye hoja ilioletwa mezani ya ripoti ya Sheria Ndogo kuhusiana na uchambuzi na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mheshimiwa Spika, na mimi kutoka mwanzo wa mchango wangu naomba nieleze kwamba ni mmoja kati ya *member* ambao wanahudumu katika hii Kamati ya Kudumu ya Bunge Sheria Ndogo, kwa hiyo namimi naomba nichukue fursa hii kukupongeza kwa imani yako kwangu kwa kuniamini na kunichagua na kuhudumia kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Spika, mimi mchango wangu nataka niulekeze kwenye uhalisia ulipo ambao unawekwa katika sheria ndogo mbalimbali zinazoletwa kwetu. Kwa mujibu wa Ibara ya 64(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977, mamlaka ya kutunga sheria yamewekwa kwa Bunge, lakini Katiba hiyo hiyo kwenye kifungu 97(5) ikatoa pia mamlaka kwa Bunge kukasimu madaraka yake kutunga sheria kwa vyombo vingine.

Mheshimiwa Spika, kutohana na wingi wa shughuli za Bunge, Bunge likapewa mamlaka kwamba linaweza

kukasimu madaraka yake ya kutunga sheria kwa mamlaka nyingine au vyombo vingine ili viweze kulisaidia kwenye kutunga sheria zinazogusa maisha ya watu kila siku huko. Kwa sababu tunajua mchakato wa Kibunge wa kutunga sheria unakuwa ni mkubwa baadhi ya wakati na mahitaji ya sheria kwenye jamii zetu yakiwa makubwa nayo kwa hiyo mamlaka ya Bunge zikapelekwa ziruhusu mamlaka zingine zitunge sheria ili sheria hizo zisaidie kwenye maisha ya watu.

Mheshimiwa Spika, sheria zilizoletwa mbele ya Kamati na tukazichambua, tumebaini kama Kamati kuna sheria 11 zilikosa uhalsia kutokana na vifungu vilivyomo kwenye sheria pamoja na maisha ya Watanzania, kwenye kiingereza tunaita *reasonability*, vifungu vya sheria havina *reasonability* ya maisha ya Watanzania na inavyoonekana kuna baadhi ya maeneo ikitokea mtu anafaida ya jambo au *interest* kwenye kitu fulani kimbillio lake anakimbilia kwenye mamlaka za kutunga sheria ndogo kwenda kuweka *sanctions* ya hayo anayotaka, anaona kwamba huko ni rahisi zaidi kuliko kuja Bungeni. Kwa hiyo wanatumia mwanya wa mamlaka za kutunga sheria ndogo kwenda kuweka vitu wanavyotikana wao. Kwa mfano, kuna sheria ndogo ililetwa mbele yetu na tukaijadili Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru Halmashauri ya Njombe, sheria imeweka tozo na ada ya ushuru ya shilingi 1,000 kwa pikipiki inayoingia *stand* pamoja na shilingi 1000 kwa gari zinazoingia *stand*.

Mheshimiwa Spika, huku ni kuvunja moyo au *ku-discourage* watu wanaojishughulisha na shughuli za pikipiki hao bodaboda; yeye unamwekea shilingi 1,000 mwenye daladala inayopakia watu 40 unamwekea shilingi 1,000 ni kumuonea. Kwa hiyo hayo ndiyo mambo sisi tuliyaona kama Kamati natukayajadili na tukaishauri Serikali na mamlaka zilizotunga hizo sheria kwenda kurekebisha.

Mheshimiwa Spika, kuna Sheria Ndogo ya Ada ya Ushuru wa Halmashauri ya Kiteto imesemwa hapa kwenye taarifa na msoma taarifa, imeweka ada shilingi 20,000 kwa shughuli za jando na unyago, siyo sahihi hata kidogo. Tumezifanya shughuli za jando na unyago kuwa kama chanzo

cha mapato, wakati zilivyowekwa uhalisia wake ni kuwa sehemu ya kufundisha vijana wetu nani shughuli za kijamii zinazokwenda kuwapa madarasa vijana wetu jinsi ya kuja kuishi kwenye jamii pana zaidi.

Kwa hiyo unavyoikeni kwamba lazima shughuli hiyo itoe shilingi 20,000 ni kuwaonea wananchi wasiokuwa na kipato wa kwenye jamii nydingi hasa za vijijini, kwa hiyo hayo ni mionganoni mwa vitu ambavyo tumeviona wakati tunajadili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuna Kanuni ya Filamu na Michezo ya Kuigiza; mchangiaji wa kwanza *Advocate Mheshimiwa Swalle* alisema hapa, Sheria Ndogo ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi Mjini wao wameweka kumiliki na kuendesha shughuli za kuonesha filamu kwenye mabanda ya filamu yale mabanda yetu yale tunaita mabanda umiza kibali kinaanzia shilingi 300,000 mpaka shilingi 1,000,000; huku ni kuwaonea wajariliamali wadogo waliojiwekeza kwenye hayo mabanda umiza, watu wenye ni maskini mtu ana mtaji wake mdogo, kaweka banda lake kwa ajili ya kuonyesha mpira na filamu wewe unamtaka akatoe shilingi 300,000 mpaka shilingi 1,000,000 hiyo shilingi 300,000 mpaka shilingi 1,000,000 anaitoa wapi.

SPIKA: Mheshimiwa Ramadhani Suleiman Ramadhani nakushukuru kwa mchango wako.

MHE. RAMADHANI SULEIMAN RAMADHANI:
Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja.
(*Makofî*)

SPIKA: Ahsante sana tunashukuru sana. Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray atafuatiwa na Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk. Mheshimiwa Regina yupo? Mheshimiwa Amour? Tunasonga mbele Mheshimiwa Ndaisaba. Mheshimiwa Amour amesimama.

MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK: Mheshimiwa Spika, nipo.

SPIKA: Endelea, Mheshimiwa Ndaisaba jiandae.

MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini kwanza nianze kwa kuwashukuru viongozi wetu wakuu wa nchi ambao ni Mama Samia, mwanamke pekee katika Afrika Mashariki anayetuongoza kwa wema sana na kwa heri sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nishukuru na nimpongeze Makamu wetu wa Rais Dkt. Philip Mpango kwa kumshauri vizuri mama na leo mafanikio yake tunayaona sana. Lakini nimshukuru pia na kumpongeza Waziri Mkuu kwa namna anavyosimamia Serikali hii ya Mama Samia nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa namna ambavyo mnavyotuongoza na katika muongozo ambao naushukuru sana ni kwamba leo mimi nipo kwenye Kamati hii ya Sheria Ndogo, najisifia kujua mambo mengi sana katika nchi hii ya Tanzania ambayo nilikuwa siyajui ni kwa sababu tu umechukua jukumu la kunipanga katika Kamati ya Sheria Ndogo, nakushukuru sana, Mwenyezi Mungu akupe uhai mrefu wenye manufaa hapa duniani na akhera, lakini akupe busara na hekima za kuliongoza Bunge hili mpaka pale Mwenyezi Mungu atakaposema basi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sheria ndijo kitu muhimu sana katika hii dunia na kila kinachofanikiwa katika dunia ni kwa sababu kimewekewa sheria madhubuti, lakini pia kusimamiwa sheria hiyo, ndijo maana hata dini zetu uislamu, ukristo na dini nyingine zinaendelea vizuri au zinafanikiwa kwa sababu ya sheria. Kwa hiyo, tunashukuru sana leo kwamba sisi tipo kwenye Kamati ya Sheria Ndogo na tunasimamia sheria hizi ili nchi iende vizuri, tunashukuru sana na tunawaomba wanaohusika sasa na sheria wazitekeleze kwa wema sana.

Mheshimiwa Spika, mimi ninamambo machache sana yaani ninayoyaomba katika mchango wangu huu; kwanza katika mijadala yetu mingi sana tulikuwa tunashuhudia kwamba ushirikishwaji wa wadau ulikuwa mdogo sana au ulikuwa hakuna katika kila sheria iliyotungwa,

kwa sababu unapomshirikisha mdau maana yake anatoa zile *concern* zake, zile hisia zako anazitoa kwako kwamba mkituambia hivi tutakuwa kuna tatzio hili, tatzio hili litajitokeza, lakini kwa vyovyote vile ukimshirikisha mdau utapunguza changamoto katika sheria, utapunguza makali katika sheria, lakini jambo hili limekosekana, unakuta kwamba sasa badala ya kwamba tunatunga sheria ili Serikali ipate mapato, lakini iende vizuri unakuta sasa kuna malalamiko ndani ya nchi. Jambo hili tunawaomba sana wale waliokasimiwa madaraka ya kutunga sheria na hasa hizi sheria ndogo ambazo sisi ndiyo tunazisimamia tunawaomba sana waweze kuwashirikisha wadau ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ambalo mimi ninapenda nishauri na niombi ni kuweka uwiano baina ya sheria mama kwa sababu sheria zote zinazoitwa ndogo maana yake kuna sheria kubwa ambayo tunaita sheria mama, ni muhimu sana tunavyoamini ni kwamba wale wanaotunga sheria ndogo wameaminiwa na tunaamini kwamba wamesomea zile sheria, kwa nini wasifanye ile sisi tunaita *murajaa*, kwa nini wasirudie kwenye zile sheria mama wakajua kwamba hiki ninachokifanya kinalingana na sheria mama. Sheria mama inasema adhabu ni shilingi 20,000 wao wanasema shilingi 200,000; haiendani kabisa yaani kama kwamba hawakusoma kabisa kwenye ile Katiba au sheria mama, sasa hii inapelekea kuleta *image* mbaya kufikiria kwamba waliotunga hii sheria walikuwa wana-*Interest* gani kwenye hiyo sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, ni kukomoana yaani kuna sheria unahisi hasa kwamba hii sheria imetungwa kwa kuwakomoa watu Fulani, sasa mimi nilikuwa naomba sana wanaotunga hizi sheria wasitunge kwa kukomoa au kwa sababu mtu fulani tu tunataka kumlinda kwenye hiyo sheria. Kwa mfano, hata Mheshimiwa Ramadhani alikuwa anasema hapa anatoa mfano wa shilingi 1,000 lakini hata bajaji wakati mwininge hata, kila ikiingia itoe kwa mfano shilingi 500 au shilingi 3,000 sawa sina gari, ila basi wanatoa 40 sasa hii inapelekea kujiona wale wengine kwamba ni *inferiority* na hawana haki katika nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nilikuwa naomba sana wale wanaopewa madaraka haya ya kukasimu/waliokasimiwa madaraka kwa ajili ya kutunga sheria ndogo wajitahidi sana watu wengine wasione kwamba tunawakomoa kwa sababu kazi hii waliyopewa, wamepewa na Bunge, wanaliwakilisha Bunge na sisi Wabunge tumechaguliwa na wananchi hao hao amba wao ndiyo wanawatungia sheria. (*Makofi*)

Sasa ikionekana sisi leo tumechaguliwa na wananchi, halafu Wabunge wanakuja kuitisha sheria ambayo imewakandamiza wao, wao watatuonaje. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana wanaokasimiwa madaraka wajitahidi sana kuangalia kutokuwakomoa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kupata fursa hii, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, ahsante Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk tunakushukuru sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro.

MHE. NDAISABA G. RUHORO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, awali ya yote nianze kwa kukushukuru kwa kunichagua nikawa Mjumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo ambapo mwanzoni nilipoona jina langu lipo kule nilikuwa nina wasiwas, lakini nilipofika kule kwenye Sheria Ndogo nikagundua kwamba kule ndiko ambako sheria zinazoongoza nchi kwenye *grassroot/ kwenye Halmashauri* zipo pale na mambo mengi yanayogusa wananchi yapo kule kwenye Sheria Ndogo, kwa unyenyekevu mkubwa sana nakushukuru sana kwa kunichagua nikawa Mjumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Spika, naomba mchango wangu niulekeze kwenye Kanuni za Sheria za Filamu na Michezo ya Kuigiza, naanzaa hapo. Taasisi ambazo zimekasimishwa madaraka ya kutunga sheria ndogo ndogo tunatarajia zifanye kazi hii kwa weledi mkubwa, lakini zifanye kazi hii katika

namna ambayo hizi sheria ndogo zinazotungwa haziji kuharibu mambo na badala yake zinakuja kujenga.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kanuni hii ya Sheria za Filamu na Michezo ya Kuigiza imeweka masharti kwa taasisi ya Serikali ikiwemo Bunge, kuomba kibali cha kutaka kutengeneza filamu pale ambapo taasisi hiyo inahitaji kutengeneza filamu. Taasisi kama *TANAPA*, Taasisi za Elimu zinahitaji kutengeneza filamu kwa ajili ya shughuli mbalimbali kwa mfano Taasisi za Elimu zinahitaji kutengeneza filamu kwa ajili ya kufundishia; taasisi kama *TANAPA* wanahitaji kutengeneza filamu kwa ajili ya kuvutia watalii ili tuweze kuongeza vivutio vyetu NA tuweze kuvitangaza kuititia filamu.

Mheshimiwa Spika, lakini kanuni hii inataka taasisi za Serikali kuomba vibali kabla ya kutengeneza filamu, mbaya zaidi kanuni illyotengenezwa inakinzana na sheria mama yenyewe ambayo sheria mama iliondoa hitaji hilo la kuomba vibali kwa taasisi za Serikali zinapotaka kutengeneza filamu. Niombe kanuni hii iweze kuondolewa/sharti hili liweze kuondolewa kwenye hii Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza.

Mheshimiwa Spika, kanuni ya 16 ya sheria hii imeorodhesha vitu ambavyo ni maudhui yanayokatazwa na sheria hii, matarajio yetu sisi nikiwemo na mimi mwenyewe ni kwamba muigizaji anapotaka kuigiza kwa mfano muigizaji anataka kuelezea madhara ya dawa za kulevyta ni matarajio yangu kwamba tunamuona mtu yule anaishi maisha yake halisi kwenye jamii, baadaye tutamuona anaanza kutumia dawa za kulevyta na baada ya hapo tutaona madhara ya dawa za kulevyta; lakini sheria hii maudhui yaliyooneshwa inakataza yule mhusika wa filamu kuigiza kile kipengele cha kutumia dawa za kulevyta.

Mheshimiwa Spika, sasa kama inakataza kile kipengele muhimu katika uigizaji maana yake ni kwamba inauwa kabisa tasnia ya uigizaji na filamu nchini. Sio hapo tu imeenda hadi kwenye mavazi, hadi kwenye umalaya na kadhalika sisi tunatarajia mtu akiwa malaya tumuone

anavyokuwa malaya, baadaye tumuone anavyopata magonjwa ikiwepo hayo ya zinaa, tuone madhara yake ili watu watakaokuwa wanatazama ile filamu yale maudhui waone lile jambo ni bayo na baada ya hapo waweze kuliacha kwenye jamii, lakini kwenye kanuni ya 16 imekataza mambo yote hayo naomba kwa kweli hii kanuni na yenewe ifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Spika, lakini kanuni hii ya sheria za filamu na michezo ya kuigiza imeweka maombi ya vibali bila ya kutumia njia za kisasa za mtandao; fikiria muigizaji yuko Jimbo la Ngara aje kuomba kibali cha kutaka kutengeneza filamu yake hapa Dodoma ama Dar es Salaam; fikiria mtu ambaye yuko Sumbawanga kwa kweli jambo hili na lenyewe halipendezi kwa sababu katika karne hii ya kutumia mtandao tunatarajia kwamba maombi haya yarahisishwe na yafanyike kwa njia kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tunaomba eneo hilo na lenyewe liweze kuboreshwa lakini niende kwenye kanuni ya Bodi ya Kitaaluma ya Walimu yaani *Tanzania Teachers Professional Board*. Kama alivyosema Mwenyekiti wetu wa Kamati wakati anawasilisha, ni kweli kwamba wakati tunachambua sheria hizi walikuja wadau mbalimbali wakiwa wanalalamika kwamba hawakushirikishwa wakati wa kutengeneza kanuni hizi.

Mheshimiwa Spika, ili sheria iende kwa walaji na waweze kuikubali ni muhimu sana sheria hiyo iweze kuwashirikisha hivyo sheria hii ni kama vile inakosa uhalali kwa sababu walaji walilalamika kwamba hawajashirikishwa. Lakini ukifuatilia kwa mfano kanuni ya 8(6)cha Kanuni ya Bodi ya Kitaalama ya Walimu, imemtaja Mwenyekiti mionganoni mwa watu wanaotakiwa kuweka sahihi kwenye kile cheti kinachomruhusu mwalimu aweze kufanya kazi ya ualimu.

Mheshimiwa Spika, huyu Mwenyekiti hajasemwa ni Mwenyekiti wa Kijiji, Kata, wa kitu gani kwa hiyo ukiangalia kwa ujumla sheria hii ina mapungufu makubwa ambayo yanahitaji kuboreshwa. Kanuni ya 8(2) ya sheria hii imetaja

cheti kinachoitwa *Ordinary Certificate of Secondary Education* wakati cheti kama hiki ndani ya nchi hii hakipo cheti kilichopo ni *Certificate of Secondary Education*, sasa tunajuliza hawa watu tulio wakasimisha madaraka ya kutunga sheria hawa angalii vitu vilivyopo?

Mheshimiwa Spika, hivyo hii kanuni ya walimu hii imelalamikiwa sana tunaomba ifanyiwe marekebisho, vitu vilivyokatazwa tunaona vinarudi.

Mheshimiwa Spika, naomba dakika mbili kuna mtu hakuwepo...

SPIKA: Haya malizia.

MHE. NDAISABA G. RUHORO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kuna kurejea kwa tozo za kero hapo nyuma Serikali iliyokuwepo ilikuwa imeshaanza kufuta tozo zote ambazo ni za kero, hebu fikiria Watanzania wanapokuwa wametoka kwenye kazi ngumu, wananchi wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanatakiwa waende wakapumzike, wengine wanakwenda kwenye kumbi za starehe wengine wanakwenda kwenye kumbi za sinema.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna hii kanuni za ada na tozo mbalimbali za Halmashauri zimeanza kuweka tozo kubwa kwenye maeneo haya ya starehe. Sisi tunapokuwa majumbani kwetu tunaangalia *tv* zilizoko majumbani kwetu lakini tukumbuke kuna watanzania wengi hawana *tv* eneo lao la kwenda kujidai mida ya jioni ni kwenye hizi kumbi za starehe pamoja na sinema. Ninaomba hili jambo liangaliwe ili tuache Watanzania wafurahie maisha hasa wanapokuwa wametoka kwenye kazi ngumu.

Mheshimiwa Spika, kuna tozo hizi zimesemwa bajaji shilingi 1,500 basi la abiria ambao lina siti 20 shilingi 1,500 hii ni Jiji la Mbeya wanataka kutoza vitu vya namna hii, wakati

mwagine bajaji anaongea na mteja shilingi 1,000/buku tu anampeleka mteja kutoka eneo moja kwenda eneo lingine. Hivyo vitu hivi visipoangaliwa vitaanza tena kurudisha zile kero ambazo kwa kweli tulishatoka huko na sasa hivi wananchi wanaishi maisha mazuri, hivyo hizi sheria ndogo ndogo zote ambazo zinaleta kero tusiweze kuzipitisha.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa unyenyekevu mkubwa kwanza kwa kuniongezea dakika Mwenyezi Mungu akubariki ninaunga mkono hoja ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge wa Ngara tunakushukuru sasa Mbunge Kiteto, Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kwenye hotuba hii ya Kamati ya Sheria Ndogo na kwanza kabisa niwapongeze Wajumbe wote wa Kamati ya Sheria Ndogo, wakiongozwa na Dkt. Wakili Msomi Mheshimiwa Rweikiza; Makamu Mwenyekiti rafiki yangu Wakili Msomi Ridhiwani Kikwete, Wakili Msomi Ramadhani, Wakili Msomi Edwin na Wajumbe wote wa Kamati hii, kwa kweli wamefanya kazi kubwa sana na wamefanya kazi kubwa ambayo kama walivyosema kwenye taarifa yao, kazi ya kutunga sheria ni ya Bunge la Jamhuri la Muungano wa Tanzania, lakini kwa mujibu wa Ibara ya 97(5) ya Katiba imelipa Bunge mamlaka ya kukasimu madaraka haya kwa mamlaka zingine ndogo zinazotunga sheria.

Mheshimiwa Spika, lakini ni vyema tukafahamu kwamba ikitokea dosari kwenye sheria ndogo, anayepata lawama ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hiyo kazi inayofanywa na hii Kamati ya Sheria Ndogo ni kazi kubwa sana wanafanya kwa niaba yetu wote kwa hiyo niwapoongeze sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, na nilikuwa nasoma taarifa yao wanasema mpaka Februari, 2021 sheria ndogo zilizofanyiwa

kazi na kuletwa ripoti hapa ni karibu sheria ndogo 915. Ni kazi kubwa sana na wamechambua vizuri sana wakaonyesha dosari mbalimbali zilizoko kwenye sheria nyingi ndogo zinazotungwa na mamlaka hizi za chini. Kwa mfano kwenye ukurasa wa 14 wanasema kuna sheria zaidi ya 15 ilikuwa na shida ya uandishi na ni kweli uandishi wa sheria sio kazi ndogo sana *legal drafting* ni soma kabisa linafundishwa na watu wengine wanachukua *degree* zao, kwa hiyo, sio kazi ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ndio maana Bunge liendelee kufanya hiyo *oversight*, kuangalia sheria ndogo hizi, ili zisiwe na dosari ya aina yoyote. Lakini ukisoma pia taarifa yao wanasema kuna sheria zaidi ya 10 utekelezaji wake ni mgumu sana kwa jinsi ilivyotungwa na wakati mwininge zinaleta kero nyingi sana kwa wananchi, lakini nyingine hata kuna sheria ndogo baada ya wao kufanya uchambuzi, yanapingana na masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo sio zile sheria mama tu, lakini hata zinakwenda mpaka zinakinzana na sheria mama, *which is very....*

Mheshimiwa Spika, nashukuru na Kamati nimesikia kuna sheria ndogo ya Halmashauri ya Kiteto hapa ambaye inatoza watu shilingi 20,000 kwa kweli ni sheria imepitishwa Disemba hapa kwa mujibu wa *G/N* hiyo, hata mimi Mbunge wa Kiteto bado sihifahamu hii sheria vizuri, lakini nitaangalia hii kwa ukaribu zaidi kwa sababu sasa sijui...

SPIKA: Yaani Mheshimiwa hiyo sheria ni kwamba sasa mmegeuza majando yale kuwa ni chanzo cha mapato ya Halmashauri; yaani ndio mantiki yake. Kwa hiyo sasa matokeo yake watu wanakuja kuweka majando Kongwa. (*Kicheko*)

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Spika ahsante sana na jirani yangu unajua mimi na wewe vitu vingi tunashirikiana pamoja na wananchi wetu wa pande zote mbili wanafanya shughuli hizi, lakini lazima tuangalie ili isilet kero kwa wananchi kwa sababu inawezekana wale wanafanya shughuli hiyo labda wanatoza hela nyingi zaidi

mpaka Halmashauri labda imefikiria labda ni chanzo cha mapato, lakini ni kweli nakubaliana na kamati tutaangalia vizuri sana ili isiletie kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, lakini zipo sheria nyingi sana hapa mimi wakati nachangia kwenye bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii ile kero ile ya kutoza ng'ombe shilingi 100,000 kwa kichwa, nilisema hapa inakinzana na Sheria ya Wanyamapori na nilishamwambia Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwanza hawafahamu kuna ng'ombe unaweza kununua kwa shilingi 100,000. Sasa kama faini inaweza kutozwa kwa shilingi 100,000 sasa si afadhalii nikuachie huyo ng'ombe mimi nikanunue mwingine huko sokoni.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuwa inakinzana na sheria mama tusikubali kabisa madaraka ya Bunge hili na mamlaka hizi za chini zituletee kero za namna hiyo na kutufanya watu waichukie Serikali kumbe mtu mmoja tu ndio ametunga sheria hizo, lakini sheria nyingine ya shoroba au marafiki zangu wa wanyamapori ilitungwa sheria na Bunge wakaambiwa wakatunge *regulation* kwa ajili ya shoroba hizi.

Mheshimiwa Spika, lakini Bunge likasema muoneshe haki za wananchi kwenye sheria hiyo yaani ndio *obligation* ya kwanza wao wakaweka masharti kwamba hawaruhuswi kufanya moja, mbili, tatu wakati *interest* ya Bunge ilikuwa ni kuona haki gani wananchi wanazo kwenye sheria hizi.

Mheshimiwa Spika, mijadala ya sheria ndogo hizi na naendelea kupongeza Kamati hii na muendeleee kutufanya hii kazi wananchi wengi wanaumia kwa sababu ya sheria hizi ndogo ndogo ambazo zinatungwa na mamlaka za chini bila kuangalia sheria mama ama Katiba ama na sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia hotuba hii na kama ulivyosema Sheria ya Tafsiri (*The Interpretation Act*) kifungu cha 36 kama alivyosema hapa inasema; “*Subsidiary legislation shall not be inconsistent with the provisions of the written law under which it is made, or of any Act, and*

subsidiary legislation shall be void to the extent of any such inconsistency,” inapatikana kwenye sheria hiyo. Kwa hiyo, ni *clearkwamba* sheria ndogo hairuhusiwi hata kisheria tu *infact haitakiwa iwe operational* kama itakuwa *inconsistency* na sheria mama.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na huo ndio mchango wangu kwa leo, ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, Mbunge wa Kiteto tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge katika utungaji wa sheria zipo baadhi ya sheria ambazo mapendekezo yanapokuja hapa Bungeni katika *areas ambazo ni critical/Serikali* inaweka pale kwamba hili litawekewa kanuni, kwa hiyo pale Wabunge hamshiriki kwenye kutunga ile sheria, kuhusu jambo lile sasa likishaenda kwenye kanuni wataalam sasa kule wanapiga msumari wa nchi sita ambao ungekuja hapa Bungeni msingekubali. (*Makof*)

Kwa hiyo ndio maana kamati yetu hii kazi mojawapo ni kuangalia maeneo kama hayo ili kuweza kuweka mambo sawasawa baadhi ya sheria inakuwa nyepesi kwa sababu vitu vyote vile muhimu vimetupwa kwenye kanuni. Lakini kumbe sasa wameweka kwenye kanuni kule kama mahali pa kujifichia hivi sasa ndio waende wakabandike vitu vyao ambavyo wao walikuwa na nia navyo kuviweka matokeo yake maisha yanakuwa ni magumu sana. Kwa hiyo kamati hii, kwa kweli inafanya kazi kubwa sana na muendelee kutusaidia kuangalia maeneo yanayofanana na hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo atafuatiwa na Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda.

MHE. PRISCUS J. TARIMO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia kwenye taarifa hii ya Kamati ya Sheria Ndogo nanikushukuru sana kwa nafasi ya kunitfea kuwa katika Kamati hii, na nikiri imekuwa ya

manufaa sana kwangu hasa ukilinganisha kwamba mimi nilikuwa Diwani miaka 10; kwa hiyo, chini kule niliona sheria hizi zinapoanza, na namna zinakuja kuhitimishwa huku juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nitakwenda kwenye ujumla tu; la kwanza ambalo limeongolewa na watu wengi ni lile suala la ushirikishwaji wa wadau. Kuna upungufu mkubwa sana, yapo mambo mengi ambayo Kamati inafanya kazi lakini wadau wangeshirikishwa tangu awali wala hayo mambo yasingetakiwa yatufikirishe sana kwenye hizi ngazi za juu. Kwa hiyo ninaomba sana sheria ndogo hizi hasa za Halmashauri ushirikishwaji wa wananchi usiangalie tu ile ya kutoa matangazo kwenye mbao za matangazo, lakini viko vikao vya chini kama vikao vya mitaa ambavyo sheria hizi zikipelekwa na wataalam wakitoa elimu kule basi mambo mengi yanaweza yakajaziwa nyama na mengine yakarekebishwa kabla ya kuja ngazi za juu na kuja kwenye Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sura nyingine ambayo inaonekana kwa haraka katika kodi nyingi ambazo tumeziona hasa za Halmashauri ni *position* ya watu wawili ambao wanahusika na utungaji.

Mheshimiwa Spika, wataalam inaonekana wao wanakuwa na *pressure* ile ya kuongeza mapato kwa hiyo wanakuwa wanazijazia tu mapato unakuta kuna mahali tuliona sheria imeletwa eti kuuza dawa za kienyeji kuwe na tozo kwa siku shilingi 1,000/shilingi 5,000; hizo dawa za kienyeji ukiangalia zingine hata hayo makusanyo ya siku hayaifikii hiyo shilingi 5,000. Kwa hiyo, kunakuwa na ile presha tu ya kuhakikisha kwamba watendaji wanataka kukidhi kiu ya kupandisha mapato na inapoenda kwa *pressure* na kwa viongozi kama Madiwani nayo inapita basi ikija huku uhalsia unaonekana hauwezekani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nadhani inahitajika wakati makundi haya mawili kwa maana ya kwamba watendaji pamoja na wawakilishi waangalie uhalsia wa

ukusanyaji wa kodi kwa sababu baadhi ya kodi ilionekana, hata gharama yake ya kukusanya ni kubwa kuliko kile ambacho kinahitajika kuja kuwa kinakusanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini lipo suala lingine ambalo limekuwa linaleta matatizo sana kwenye Sheria Ndogo za Halmashauri, baada ya vile vitambulisho vya ujasiriamali wapo watu ambao wanakuwa *excluded* kabisa kutokana na ile *definition* kwamba *turnover* yao haizidi shilingi milioni nne. Lakini unakuta halmashauri nyingine wamewaleta hawa na kuwatungia sheria ambayo inawatambua katika kutozwa tozo mbalimbali. Sasa ukiangalia inakinzana na ile sheria au *definition* ya vile vitambulisho vya wajasiriamali wadogo. Kwa hiyo unakuta kuna muingiliano wa sheria mbili katika sehemu moja.

Mheshimiwa Spika, niongelee kidogo suala la filamu; tumepata matatizo sana kwenye sheria ile. Pamoja na mambo mengine, inasemekana waigizaji wetu wakitaka kuigiza kwa mfano kama polisi, wakaombe kibali polisi ili kuвая zile nguo zinazofanana na polisi au jeshi. Lakini hata kutumia maeneo yanayofanana na ya Serikali wanasesma inakinzana na usalama.

Mheshimiwa Spika, sasa wenzetu wanatengeneza mpaka maeneo ya bandia, hawa wa kwetu hawana uwezo huo, lakini sheria na kanuni unakuta zimewanyima kuingia huko na kama unavyofahamu, filamu ni jambo la kimataifa, zinakwenda kushindana na filamu nyingine. Sasa unakuta filamu zetu watu wanakuwa ni polisi lakini amevaa kama mwanamichezo, kwa hiyo uhaliasia unakuwa hauwezi kuonekana kwa sababu ya masharti ambayo tunaweka ambayo haywasaidii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hata kwenye mavazi, wadau walipokuja walituuliza swali ambalo pengine nafikiri hata Wabunge watashangaa; walisema masharti yamekuwa magumu kana kwamba inabidi hata mtu anayekwenda kuogelea kwenye filamu ya Kitanzania aogelee na hijabu. Sasa inaleta shida, ushindani kwenye soko la kimataifa, filamu

zetu haziwezi kushindana na zile nyingine kwa sababu ya masharti ambayo tunajiwekea wenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa kifupi kabisa huo ndiyo mchango wangu, na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo. Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda nilishakutaja na utafuatiwa na Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi ya kuendelea kufanya kazi ya kulitumikia Taifa letu kupitia Bunge lako hili na pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi, na zaidi ya yote, kunateua na mimi kuwa mionganini mwa Wabunge wanaounda Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilipata shida kidogo, mimi taaluma yangu ni mwandishi wa habari, nilipopelekwa kwenye sheria ndogo nikasema sasa inakuaje hii? Lakini kumbe ulikuwa unanipeleka shule nyingine ya kujifunza ili niweze kujuua mambo mengi zaidi, nakushukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Wanakamati wenzangu wametoa hoja nyingi za mambo ambayo tuliyapitia na kwa kweli niseme waraka huu ulioletwa na Kamati yetu mbele ya Bunge lako, tumefanya uchambuzi wa kutosha na kusaidiwa vya kutosha na wataalam tuliowashirikisha na wadau tuliowaita kwenye vikao vya Kamati na kwa maana hiyo nataka niseme tulijikita kwelikweli kuangalia na kufanya uchambuzi ili tuone namna nzuri ya kulishauri Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, nifanye mapitio madogo tu katika baadhi ya mambo ambayo wengine inawezekana wamekwishayataja; kwa mfano, tumejadili sana kuhusu sheria ndogo zinazoongoza masuala ya filamu. Na katika kujadili sana, kwa sababu yalikuwa ni mambo ambayo katika sura

na tamaduni za kwetu bado ni mambo ambayo hayajazoleka sana kwa Watanzania, hii tasnia ya filamu hajachukua kasi kubwa sana kama nchi za wenzetu. Kwa maana hiyo kuna mambo ambayo tulyakuta yamewekwa kwenye mapendekezo ya sheria ndogo ambayo yalikuwa yananyima uhuru tasnia yenyewe kuendelea.

Mheshimiwa Spika, kikubwa ni kwamba kama mtu anataka kuonesha kitu juu ya tatizo la dawa za kulevyta, lazima aoneshe, lazima awepo mtu anayeonesha hizo dawa za kulevyta yanatumiwaje na yanaathiri vipi. Lakini mwisho lazima matokeo yake yaoneshe madhara.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, haiwezekani filamu ioneshwe mtu anaiba mali ya umma halafu baadaye inaonekana ametajirika, maisha yake yanamekuwa mazuri, anaendelea na maisha yake. Ut-a-entertain watu wengi kufikiria kuiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani filamu ioneshe mtu anatumia dawa za kulevyta halafu ione kane huyu amekuwa mchezaji bora mpaka akapata tuzo kwa sababu alikuwa anatumia dawa za kulevyta. Lakini tunategemea hiyo filamu itakapoonesha mtu iruhusiwe kuonesha mtu anatumia dawa za kulevyta, lakini matokeo ya mwisho ya filamu hiyo yaoneshe jinsi alivyoathirika na ambavyo amekuwa siyo wa msaada kwa Taifa. Kwa hiyo, hayo ndiyo mambo ambayo tumeyaelekeza katika maoni yetu kwenye Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo vilevile tulyaona ambayo umeyaeleza hapa kidogo, juu ya utungaji wa kanuni, sheria mama inatoa *loophole* kwamba Waziri mwenye dhamana atatunga kanuni zinazosimamia sheria hii. Sasa anapokwenda kutunga zile kanuni unakuta kwenye kanuni kule kuna sehemu inasema, katika jambo hili uamuzi wa Waziri utakuwa wa mwisho. Tukasema hapana, lazima useme kwamba asiyeridhika atakwenda mahakamani, Mahakama ndiyo kiwe chombo cha mwisho cha kuamua juu ya watu. Usiseme uamuzi wa Waziri katika jambo hili utakuwa wa mwisho. Mambo hayo nayo tuliangalia katika baadhi ya

sheria ndogo na tukafika mahali tukayaweka katika mapendekezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla mimi nirudie kusema kwamba nakushukuru sana kwa kunipanga kwenye Kamati hii. Bado ninaendelea kujifunza, lakini kwa ujumla ni kazi kubwa na muhimu, na niseme muda siku zote umekuwa hautoshi kwa sababu mpaka tunachambua sheria zote hizo unazosikia, bado kuna nyingi hazijafanyiwa uchambuzi, na bado kuna nyingi zinazolalamikiwa. (*Makofii*)

Kwa hiyo ni busara yako na Bunge lako kuona namna ya kuiongezea Kamati hii muda ili tusiendelee kuwa na sheria ndogo ambazo zinalalamikiwa huko mtaani. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini. Mheshimiwa Kasalali atafuatiwa na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na uzima, lakini pia nikushukuru wewe, kwanza kwa nafasi hii uliyonipatia ya kuchangia hoja hii ambayo imewasilishwa kwa umaridadi mkubwa na Makamu Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete. Lakini pia nikushukuru kwa kuamua kinitfea kuhudumu katika hii Kamati ya Sheria Ndogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama wenzangu waliotangulia, mimi pia kwa taaluma yangu ni mwaliimu, nilipoona nimepelekwa kwenye Kamati ya Sheria Ndogo nilishtuka kidogo nikasema sasa huku Mheshimiwa Spika amenipeleka nikafanye nini?

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya kuanza kufanya kazi mule niligundua ulinipa jukumu nyeti, kubwa na ambalo linahitaji umakini na muda. Kwa sababu mambo mengi yanayoendeshwa kwenye nchi hii yanaendeshwa kwa utaratibu wa kanuni na sheria ndogo ambazo sisi kwenye

Kamati yetu ndiko tunakozipitia. Kwa hiyo nakushukuru sana kwa nafasi hii na ninakuahidi nitafanya kazi kwa nguvu zote na weledi mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda kwenye vitu mahususi, niliomba kushauri kidogo, nadhani katika uwasilishaji tumeona katika muda huu mfupi tu kuna sheria ndogo zaidi ya 915. Hizi sheria ndogo zote zinaathiri maisha ya watu wa chini huko, zinapitishwa na mamlaka mbalimbali zilizokasimiwa na Bunge kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Spika, lakini katika sheria chache ambazo tumezипития tumegundua mapungufu makubwa sana. Kuna mapungufu ambayo ukiyaangalia tu unasema hawa watu wakati wanatengeneza hizi sheria walikuwa wamejifungia wapi.

Kwa hiyo, kama alivyomalizia Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda wakati anamaliza mchango wake, mimi mwenyewe nimeona lipo hitaji la Kamati ya Sheria Ndogo kupata muda zaidi wa kupitisha sheria ili kupunguza kero tunazokutana nazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naamini kama sheria iliyopeleka zao la choroko na dengu kwenye Stakabadhi Ghalani ingeanzia kwenye Kamati ya Sheria Ndogo, wala tusingekuja kutoa maelekezo hapa Bungeni kuwaambia Wizara kwamba waandike waraka mwingine wa kwenda kuviondoa kwenye Stakabadhi Ghalani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ambacho mimi nimekigundua katika muda mfupi kwenye Kamati hii, inawezekana kwenye maeneo mengi tunapeleka watu ambao hawayajui hayo maeneo kwenda kuyatengenezea sheria ndogo. Kwa sababu ninaamini, kwenye maeneo kama ya – tulikuwa tunaangalia hapa Sheria ya Bodi ya Filamu, kwamba mtu anakwenda kutengeneza kanuni za filamu, mtu ambaye kwenye maisha yake hata filamu kuiangalia huwa haiangalii, lakini anakwenda kuwatengenezea watu

wanaoangalia filamu na watu wanaofanya maigizo kanuni pale.

Kwa hiyo, ipo haja ya Kamati hii kupata muda wa kutosha ili kuweza kuzipitia sheria hizi, naamini ofisi yako italiangalia hili.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi naomba nijikite kwenye baadhi ya mambo, lakini kitu cha msingi kabisa ambacho nataka nikiangalie, kuna sheria nyingi ndogo na kanuni ambazo zinatengenezwa zinakuwa hazikidhi uhaliasia wa mambo.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo wachangiaji awali wamechangia, unakuta sheria imetungwa lakini ukiangalia uhalisia wake, nilikuwa naangalia Sheria Ndogo ya Jiji la Mbeya ambayo naamini illitungwa huko nyuma, sasa imekuja kuanza kazi sasa, iliyokuwa inasema kwamba kila bajaji ilipokuwa inatoka *stand* inatakiwa illipe shilingi 1,500. Unajiuiliza huyu mtu aliyetunga hii sheria alikuwa amejifungia wapi? Yaani bajaji kila ikitoka *stand* shilingi 1,500. Yaani hii unakuta kabisa hawa watu ukiangalia, wakati huo kuna daladala wanalamikia zile bajaji.

Kwa hiyo, mimi naamini wale daladala wanakwenda kuhonga wale au inawezekana kuna mtu aliyekuwa anatunga hizo sheria labda ana daladala ili afanye kabisa bajaji zisiingie *stand*, kwa sababu bajaji ikibeba watu labda wa shilingi 500 kila mtu kwa watu watatu ina maana yeye bajaji anakuwa kazi yake ni kulipwa na kulipa ushuru. Hakuna kinachofanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hii ilinishtua lakini nilipofuatialia na kwa faida ya Bunge hili, kwa sababu Mheshimiwa Naibu Spika ni Mbunge wa Mbeya, lakini ukiangalia, hii sheria imetungwa bado Mheshimiwa Naibu Spika hajawa Mbunge wa Mbeya. Inawezekana walijua watashindwa, kwa hiyo wakaona watengeneze sheria ambayo itakuja imfanye Mbunge anayekuwa afanye kazi kwa ugumu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ukiangalia sheria hizi zinapotengenezwa, ni lazima watu wanaozitunga wawe wana...

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Kasalali, inaelekea ilitungwa wakati ule CHADEMA ndio wanaongoza Jiji, eh?

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa.

SPIKA: Mheshimiwa Cecilia nimekuona umesimama.

TAARIFA

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba utungaji wa sheria haumlengi mtu, utungaji wa sheria yoyote, ama sheria mama au sheria ndogo, unalenga utekelezaji wa jambo fulani kwenye jamii uweze kufanikiwa. Kwa hiyo, jamii yoyote inayolengwa, hajjalishi ni CHADEMA, CCM au asiyekuwa na chama, mkristo au mpagani, vyovyyote vile, inalenga jamii kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na wanaoandaa sheria ndogo hizi wengi ni watendaji wetu kwenye ofisi zetu za Serikali. Kama mchakato unaanzia kwenye ngazi za kata, vijiji, inapanda kwa mfumo wa...

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninataka nimpe hiyo taarifa. (*Makofi*)

SPIKA: Yaani alichokuwa anasema ni kwamba sheria hii ilitungwa kipindi kile ambacho Meya na Madiwani wengi wa Jiji la Mbeya walikuwa ni wa CHADEMA; ndicho alichokuwa anasema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Kasalali, sijui kama ulimaanisha hivyo?

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Spika, hii taarifa niliyopewa ngoja niendelee kuwa nimepewa, lakini mimi kitu cha msingi ambacho nilikuwa nataka kukieleza ni kwamba Baraza la Madiwani liliopita la Halmashauri ya Jiji la Mbeya ndilo lilioshiriki kutengeneza sheria hii ndogo ambayo ilikuwa inawakandamiza waendesha bajaji na bodaboda wa Jiji la Mbeya ambayo sisi wakati tunajadili kwenye... (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Bahati mbaya muda umekwisha. Tunaendelea na mchangiaji mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nillona taarifa yako, basi tunaendelea. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika.

T A A R I F A

MHE. DKT. TULIA ACKSON: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Kasalali Mageni kwa mchango wake. Jambo alilolisema ni kweli asilimia mia moja, zipo sheria ndogo nydingi ambazo kwa kweli namna zilivytengenezwa zilikusudia kuwaumiza sana wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfano mmojawapo ni sheria ndogo ambayo inatoa faini kwa mwenye chombo cha usafiri cha bajaji na daladala, alipe kati ya shilingi 200,000 na shilingi milioni moja kwa kosa la *wrong parking*. Sasa wanakuwa wametazama wapi mpaka wakatunga sheria ndogo kama hiyo?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Kasalali Mageni ni kweli kabisa uliyosema, hawa watu walijipanga kushindwa wakataka kutengeneza mazingira magumu kwa

watakaokuja wakati utekelezaji wa sheria ndogo hizi utakapoanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niiombe Kamati hii iendelee kufanya kazi nzuri wanayofanya ya kuchambua hizi sheria ndogo ambazo zinawaumiza sana wananchi, hasa katika maeneo ambayo wanakuwa wametoka hawa ndugu zetu, ikiwemo Mbeya Mjini. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, atafuatiwa na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi kuchangia katika mjadala huu muhimu sana wa sheria ndogo na awali ya yote niwapongeze sana Wajumbe wote wa Kamati hii kwa namna ambavyo wamechakata na kuleta mapendekezo yao juu ya nini sasa kifanyike kwa ajili ya kufanya marekebisho ya sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo limenisimamisha hapa leo ni ushirikishwaji wa wadau kwenye kutunga hizi sheria ndogo kwenye mamlaka zetu. Tumeshuhudia maeneo mengi sheria hizi zimetungwa katika mazingira ambayo hazitekelezeki, lakini katika mazingira mengine sheria hizi zinakinzana moja kwa moja na Katiba na sheria mama.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba sana Bunge lako pamoja na Kamati hii ya Sheria Ndogo kuzichambua zile sheria ndogo ndogo zote ambazo zinakinzana na sheria mama lakini zinatengeneza mtafaruku kwa wananchi katika utekelezaji wake ili kuendelea kuishi katika nchi ambayo ina amani na utawala wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, nitakupa mfano wa sheria moja ndogo ya rumbesa. Kuna sheria ambayo inazuia kupakia mzigo kwenye magunia isizidi kilo kati ya 100(+5 na -5). Lakini namna wanavyotekeliza hii sheria, wanapima yale magunia baada ya kupakiliwa kwenye magari badala ya kupima uzito wa gari kwenye mizani.

Mheshimiwa Spika, mimi ninachofahamu, kama unataka kudhibiti rumbesa na kwa sababu rumbesa imewekwa kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wasilanguliwe kwenye biashara ya mazao, pale wakati wa ununuzi wa mazao, kama unanunua mahindi kwenye eneo la soko pale ndipo ambapo vipimo vinasimamiwa, mnunuzi anunue kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa katika soko lile.

Mheshimiwa Spika, lakini wakati ameshapakia ule mzigo, kwa sababu unakuta mnunuzi mwingine amenunua mahindi au kabichi au karoti, amekwenda kuzimwaga kwenye chumba kimoja halafu baada ya kununua mazao yake yote anakwenda kuyapaki kwenye magunia na kusafirisha. Wakati anapaki kwa kuwa tayari alikuwa ameshapima wakati wa kununua, wakati wa kupaki anaweza kupaki kienyeji kadri ambavyo anaweza ili kuweza kupunguza gharama pia ya vifungashio.

Mheshimiwa Spika, sasa kinachotokea wenzetu wana-block barabarani, wanaweka vizuizi barabarani na kuanza kupima gunia mojamoja ambalo liko ndani ya gari, kinyume na utaratibu ambaao umewekwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninaomba sheria hizo zote kwa sababu zimebekwa kwa nia njema na ni sheria nzuri na lengo ni kumlinda Mtanzania aweze kufanya shughuli zake katika mazingira yenye ustawi, ziangaliwe na zitengenezewe kanuni nzuri za utekelezaji ili tusiwaumize hawa pia wanaofanya biashara ya usafirishaji wakati wa kusafirisha mazao haya.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ninapenda kuchangia ni hili la kuandaa sheria hizi kwa mujibu wa sheria mama. Tumeona katika mazingira mengi, na moja amelizungumza Mheshimiwa Naibu Spika kwenye taarifa yake, uki-park gari vibaya Dar es Salaam, gharama ambayo unapigwa inakwenda tofauti na gharama ile ya tozo/faini za magari kwa maana ya makosa barabarani; zinakwenda tofauti.

Mheshimiwa Spika, lakini sheria ambayo tunaifuata ya msingi ni ile ya faini za barabaran. Kwa nini huyu wa jiji akamate tozo kubwa ya faini unapo-*park* sehemu pengine ambayo siyo rasmi, au unapofanya kosa lolote la matumizi ya magari kwenye maeneo hayo, tofauti na ile tozo mama ambayo imekuwa-*defined* kwenye sheria.

Mheshimiwa Spika, maeneo hayo yote yakifanyiwa kazi tutaendelea kuishi kwenye mazingira ambayo kila mmoja ataiheshimu sheria na mwisho wa siku tutaendelea kufanya vizuri.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Taarifa, Mheshimiwa Ester Bulaya.

TAARIFA

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nilikuwa tu nampa taarifa kwa sheria ndogo ndogo ambazo zinakera, kulikuwa na mgomo wa waendesha bajaji wa Musoma Mjini, Manispaa ile Halmashauri ni ya Chama cha Mapinduzi. Bajaji akimpeleka mteja haruhusiwi kumpakiza mtu, arudi kwenye kituo chake bila abiria, akipakiza faini shilingi 3000. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Husna, unapokea Taarifa hiyo?

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Spika, ubaya wa hizi sheria ndogo nyngi zimetungwa kipindi cha miaka mitano iliyopita ambapo halmashauri zetu nyngi zilikuwa na mchanganyiko wa vyama vingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee mchango wangu kwenye eneo la elimu, tuna sheria nzuri sana nchini, lakini wananchi hawazifahamu sheria kwa sababu hakuna utolewaji ...

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko.

TAARIFA

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nataka nimpe tu taarifa Mheshimiwa Husna kwamba tukiangalia michango yote ni kwamba kweli hizi sheria ndogo ndogo zinakera, lakini ukitaka kuweka mizania ya vyama mchanganyiko na nini kwa zaidi ya asilimia 80 Halmashauri zilikuwa chini ya Chama cha Mapinduzi na sheria nyingi ambazo zinakera nyingi nyingi Tanzania zimetungwa na hao wa Chama cha Mapinduzi.

Kwa hiyo tuondoe mambo ya uvymama tuangalie nini *solution* kubwa kwa kuondoa hizi kero ndogo ndogo tukianza kuchagiza CHADEMA, CCM mtajikuta mnajimaliza, maana yake zaidi ya asilimia 80 ilikuwa chini ya Chama cha Mapinduzi, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Taarifa hiyo Mheshimiwa Husna unaipokea?

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Spika, siipokei hiyo taarifa kwa sababu Mheshimiwa Esther Matiko alikuwa ana nafasi ya kuomba kuchangia, nimuombe tu aheshimu nafasi yangu ya kuchangia ili niweze kumaliza mchango wangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa la utekelezaji wa sheria nchini ni watu kukosa elimu juuu ya sheria na unafahamu kabisa kwamba kutokujua sheria siyo utetezi mbele ya sheria. Ningemba sana Kamati ya Sheria Ndogo hii ya Bunge kuelekeza mamlaka zetu kutoa elimu kwa wananchi kabla ya utekelezaji wa sheria iliyotengenezwa kwenda kutekelezwa, hii itatusaidia sana kupunguza migogoro, kupunguza manung'unico na mwisho wa siku kutekeleza sheria hizi katika hali ambayo ni salama kwa ajili ya malengo ya sheria zilizotengenezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maeleo hayo naombaa kuunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunipa ruhusa ya kuzungumza, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko kwa mchango wako mzuri.

Waheshimiwa Wabunge, michango hii mkiitazama mnaweza mkafikiri kwamba mambo haya ni madogo, lakini ni mambo mazito. Mimi wiki iliyopita kuna vijana hao *graduate* tunaosema wajajiri, wawili kati yao wana *degree* za hesabu wazuri sana katika hesabu, lakini ukishamaliza hesabu sasa unaajiriwa wapi, ngumu. Kwa hiyo wakajunga kama watatu/wanne hivi wakanunua mahindi yao pale Kibaigwa kwenye soko letu, wakapakia mzigo wao wakaupitisha kwenye mzani wa soko, kwa hiyo, gari lile linajulikana lina tani ngapi, na kadhalika, unaweza ukapiga hesabu kirahisi tu kujua mzigo, maana yake linapima kabla ya mzigo, linapima baada ya kupakia mzigo kwa hiyo unajua ni kiasi gani na kwa hiyo mzani hauna shida. (*Makofii*)

Walipofika mbele kule Dumila, Dumila hivi wakakamatwa wamekaa pale siku nne, faini shilingi 2,500,000 na wao mzigo wao ndio ule, yaani ile ndio mtaji wao ndio wameshaweka na wamefuata taratibu zote walichokamatiwa pale ni ile anayosema Mheshimiwa Husna kwamba sasa shusheni gunia moja moja tuanze kuangalia mzigo kila gunia; je, lipo kilo 90? Limezidi au halijazidi? Sasa ndiyo hizo sheria ndogo ndogo ambazo kwa kweli, yaani vijana wanani pigia simu sasa sisi tufanyeje, tumesoma tunama-*degree*, ajira hamtupi, halafu tena tunakamatwa hovyo kila mahali, mambo yenye we tumefuata sheria zote, tumepima, halafu tena tunakamatwa yaani vitu Mbunge akisema hapa mtu anaweza akaona ni kama *light* lakini *it's very frustrating* kwa vijana hawa ambao tunasema wajajiri wenye we. (*Makofii*)

Baadhi ya sheria ndogo hizi kwa kweli ni *anti-vijana kujishughulisha* kiasi ambacho Serikali ina nia njema ya kuhakikisha kwamba vijana wanahangaika, lakini baadhi ya sheria hizi zinakuwa nyingi na zinasumbua sana. Kwa hiyo, napokea kabisa mchango wako Mheshimiwa Husna, tuangalie na Kamati tufuatilie zile sheria ambazo unazona ni kandamizi tufuatilie kuhakikisha zimebadilika, maana baada

ya miezi mtatuletea tena taarifa. Kama kuna sheria ndogo ambazo mlishauri kabisa *strongly* zibadilishwe halafu hazijabadiishwa mtatuletea tena hapa ili tuelleze Serikali kwa herufi kubwa zaidi kwamba maisha yawe mazuri kama vile Chama cha Mapinduzi kinavyotaka na Serikali yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira.

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA: Mheshimiwa Spika, kwa kunipatia fursa hii na mimi nitumie fursa hii kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati na Makamu wake na timu yao nzima kwa kazi kubwa nzuri wanayoifanya kwa kweli sheria ndogo hizi ndio uhai wa utekelezaji wa sheria katika maeneo yetu Tanzania nzima. Na Katiba imetoa ruhusa sisi Wabunge kukasimisha madaraka hayo katika maeneo hayo ambayo yanahusika kwa ajili ya kutunga hizo sheria ndogo, lakini pia tumepewaa jukumu la kudhibiti sheria hizi sasa na hili sio jambo la tofauti, ni jambo la utaratibu wa kawaida katika Mabunge yote ya Jumuiya za Madola. Kwa hiyo tupo sawa sawa na tunakwenda vizuri na Sheria ya Tafsiri za Sheria kifungu 38 kimeeleza wazi kama ambavyo amesema Makamu Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na mimi nikubaliane na wewe kwamba kutungwa kwa hizi sheria ndogo kunategemeana pia na utungaji wa sheria wa sisi hapa Bungeni kupitia Kamati yetu ya Katiba na Sheria. Kwa hiyo ningefurahi kama tungeweza kuwa na ushirikiano wa karibu sasa baina ya Kamati ya Katiba na Sheria na wenzetu wa Sheria Ndogo ili tukaweza kuona kwamba zile sheria ambazo zinatoa mianya kwenye kutengenezwa sheria ambazo zinakosa masharti na vigezo basi angalau tupunguze hilo suala.

Mheshimiwa Spika, changamoto ni nyingi sana ameeleza katika Kamati ya Sheria Ndogo ikiwemo na kukinzana kwa Sheria Ndogo na Sheria mama kama ambavyo nimeeleza, lakini sheria hizi kukosa uhalisia na utekelezaji wake kuwa mgumu katika maeneo yetu, lakini pia tumeambiwa hapa mawasiliano hafifu kutoka kwenye

Ofisi ya Mwanasheria Mkoo pamoja na mamlaka husika au baadhi ya mamlaka husika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nafikiri Mwanasheria Mkoo akijipanga vizuri na timu yake basi marekebisho mengi hayatofika kwenye Kamati ya Sheria Ndogo, kwa hiyo hilo nafikiri mwenyewe yupo na amelipokea. Lakini suala la kutoshirikishwa wadau ni suala ambalo ni changamoto kwa sababu hata sisi hapa katika utunzi wa sheria tunaona kwenye Kamati ya Katiba na Sheria tunawaalika wadau wengi, tukipata maoni ya wadau wengi ndio sheria inakwenda kuwa afadhali nzuri kwa sababu wanatoa maoni ndio wale wanaoenda kuzitumia hizo sheria zetu huko kwenye maeneo yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine la tozo kwenye tasnia ya filamu, lakini kwenye hiyo jando imetajwa basi hayo mambo ni ya kuzingatia ya kuangalia siyo lazima mpaka yafike kwenye Kamati yetu ya Sheria Ndogo, nafikiri wenyewe huko wanaweza kurekebisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuna suala muhimu sana ambalo nitalzungumza hapa leo ni kuhusu suala la michezo ya kuigiza hii; kama tuna kumbukumbu nzuri Bunge la Kumi na Moja tulipitisha sheria katika kurekebisha kuipa Bodi ya Filamu mamlaka ya kudhibiti mporomoko wa maadili tunavyofanya maligizo yetu hapa kwenye filamu zetu Tanzania, sisemi kwamba napingana na kamati moja kwa moja, lakini ninachotaka kusema ni kwamba ikiwa ulevi, ikiwa ukahaba, ikiwa mavazi mabovu yatalenga kuielimisha jamii basi michezo huo hauna tatizo, lakini ikiwa ulevi, ukahaba pamoja na mambo mengine yanayofanywa kwenye filamu yanaelekeza kuiharibu zaidi jamii hilo sasa ni tatizo na ndiyo maana Bodi ya Filamu ikapewa mamlaka ya kudhibiti filamu zote ambazo zinaoneshwa kwenye nchi yetu, hili ni jambo la msingi sana. Kwa sababu kila pahala kama ambavyo wenzangu wamesema kwamba tukisema wavae hijabu wote michezo itakuufa au haitoonekana vizuri, siyo lazima kuvala hijabu au kuvala kama mimi ndiyo unazidi kupendeza, hapana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ila sema tunavyokwenda kwenye mabasi tunafuatana na familia zetu na watoto wetu, michezo inayoonyeshwa kwa kweli hasa kwa sisi wanawake yaani siyo kama ndiyo amevaa, hajjavaliwa nguo yaani mwili wote upo wazi nguo ipo juu ya paja ni hatari kwa kweli. Kwa hiyo tunawafundisha Watoto wetu mambo ambayo siyo ya maana na siyo maadili ya nchi yetu. Kwa hiyo, hilo mimi napenda nigongee sana hapo na ninaomba kamati inielewe hivyo kwamba hii Bodi ya Filamu imepewa Mamlaka kwa mujibu wa sheria tuliyotengeneza wenyewe katika Bunge la Kumi na Moja kwa hiyo tuendelee, tuwaachie wafanye kazi yao, lakini watoe elimu kwa namna ambayo itaielimisha jamii na siyo kuipotosha jamii. (*Makoff*)

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho kabisa pamoja na kuomba ushirikiano mzuri baina ya kamati yangu na Kamati ya Sheria Ndogo kifungu cha 38(2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinatoa ruhusa Bunge kuitisha azimio la kukataa Sheria Ndogo ambayo inakiuka masharti ya sheria mama. Kwa hiyo, naomba sana kamati yetu ya sheria ndogo ilizingatie hilo, tunapoona kwamba sheria ndogo inakinzana na sheria mama na inaleta mtafaruku huu katika utekelezaji basi kama kuna uwezekano izuiliwe kuititia Azimio la Bunge kwa mujibu wa sheria ya kifungu 38(1). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ahsante sana kwa kunipa fursa. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga kwa mchango wako. Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira atafuatiwa na mchangiaji wa mwisho Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii, nami ningependa kuchangia kidogo katika eneo hili la sheria ndogo. Kwa uwelewa wangu sheria ndogo zinapaswa zifuate utunzi wa sheria na kuhakikisha kwamba hazikinzani na yale ambayo yameelekezwa kwenye Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, na kati ya vitu ambavyo Katiba yetu inatambua ni pamoja na suala nzima la *freedom of association* na huu ndiyo msingi wa sekta ya Asasi za Kiraia kwa maana ya *CSOs, NGOs* na kadhalika ambao wanakuja pamoja kwa lengo la kuchangia maendeleo katika jamii.

Mheshimiwa Spika, sasa katika upande huu wa sheria ndogo ziko sheria ndogo ambazo zinatungwa na Halmashauri, lakini pia zipo kanuni ambazo zinatungwa na Mawaziri wenyе dhamana ya maeneo husika. Hapa ningependa kurejea kwenye Sheria ya *NGOs*. Katika sheria hii ilitoa mwanya wa Waziri mwenye dhamana kuandaa kanuni kutunga kanuni na kati ya kanuni ambazo zimetungwa chini ya sheria hii ya *NGOs*ipo kanuni ambayo inataka *NGOs* kwa maana ya sekta Nzima ya Asasi za Kiraia pale ambapo zinapata ufadhili wa mradi wowote hata kwa kiwango cha milioni 20 uwasilishe lile andiko lake, uwasilishe pia na mkataba na nini ambacho unataka kwenda kufanya, uwasilishe kwenye ofisi mbili tofauti yaani unatakiwa uwasilishe kwenye Ofisi ya Msajili wa *NGOs*lakini pia Hazina na baada ya kuwasilisha hivyo vitu vyote huyu *NGOs*hawezи kutekeleza ule mradi mpaka apate kibali kutoka kwa msajili wa *NGOs*na Hazina, jambo ambalo kwa kawaida linaongeza mlolongo mrefu. (*Makofii*)

Kwa hiyo unakuta labda *NGOs* imegundua kuna changamoto fulani kwenye jamii, imetafuta ufadhili imepata ufadhili labda milioni 20/30 lakini hawezи kutekeleza mpaka apewe kibali na unakuta ufadhili ule kapewa labda mradi unatakiwa utekelezwe ndani ya miezi sita mpaka mwaka, mlolongo mzima huu wa mpaka kupata kibali unachukua miezi sita, kwa hiyo mpaka unakuja kupata kibali ile fedha inabidi umrudishie mfadhili au inakuwa ni muda mfupi sana umberaki kiasi kwamba huwezi kutekeleza ule mradi jinsi ambavyo umetakikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa jambo hili linafifisha ile *financial freedom* ya hii sekta ya Asasi za Kiraia, lakini mbaya zaidi unapelekea pia kuwapa changamoto wadau wa maendeleo kwa maana ya wafadhili wanakuwa na hofu

kuona je, mradi utatekelezeka ndani ya muda ambao umepangwa?

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kukiri kanuni hii iliwekwa kwa nia njema kabisa ya kuhakikisha kwamba tunaimarisha uwazi na uwajibikaji kwenye Sekta ya Asasi za Kiraia, lakini hapo hapo tutambue ya kwamba hizi *NGOs* zinakuwa zimesajiliwa kwa hiyo Serikali kupitia Msajili wa *NGOs* imepitia katiba zake, imepitia malengo ikawapa usajili, kila mwisho wa mwaka wanatakiwa wawasilishe ripoti yao ya mwaka ya kazi/*audited accounts*.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi napenda kupendekeza hii kanuni Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana aiangalie upya ili pia basi hizi *NGOs*, sekta ya AZAKI kwa maana ya *NGOs*, *CSOs*, wanatakiwa watakapokuwa wanawakilisha taarifa zao za mwaka (*audited accounts*) pia wawasilishe mikataba ya zile fedha walizopata na namna walivyoztumia. Kwa sababu kinyume na hapo tunaenda kinyume na lengo zima ambalo kwanza limewekwa kwenye Katiba, lakini hata lengo la ile sheria mama ya *NGOs* ambayo inataka kuhakikisha ya kwamba Sekta hii ya AZAKI inachangia katika maendeleo ya jamii na sekta hii inafanya kazi kubwa sana kwa kushirikiana na Serikali na hata juhudzi zake zimetambuliwa kwenye llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2025. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa hiyo kwa kumalizia napenda kuiomba sana Serikali kupita wizara husika izipitie upya kanuni hizi, lakini...

MHE: SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Taarifa.

TAARIFA

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, ninaomba nimpe taarifa anayezungumza kwa sababu mimi

pamoja na wengine najua wamo hapa tumefanya kwenye *NGOs* kwa muda mrefu. Ni lazima upeleke taarifa kwenye Wizara husika na *audited account* huwa wanafanya hivyo kwa watu wa *NGOs* sijajua labda anazungumzia eneo lipi?

SPIKA: Nakuongezea dakika Mheshimiwa fafanua.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Spika, ahsante nashukuru kama alinisikiliza vizuri kwenye mchango wangu nilisema kwamba kila mwaka *NGOs* zinawasilisha taarifa zao za mwaka za hesabu, lakini pia zinawasilisha *audited accounts*, lakini kwenye kanuni imesema kwamba *NGOs* itakapopata mradi wa kuanzia shilingi milioni 20 isitekeleze mradi huo mpaka ipate kibali kutoka kwa Msajili wa *NGOs* na Hazina. (*Makofii*)

Kwa hiyo, mimi ninachoongelea hapa kwa sababu tunaongelea sheria ndogo na mojawapo ya sheria ndogo zipo za upande wa halmashauri, lakini pia zipo zile ambazo zinatungwa na Mawaziri wenyewe dhamana kupitia kanuni, kwa hiyo, hicho ndiyo nilichokuwa nakiongelea na ningependa na ye ye ajielimishe zaidi katika eneo hili ili kwa pamoja tuweze kuishauri Serikali vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kurejea tena naiomba sana Wizara yenye dhamana ya masuala ya maendeleo ya jamii ipitie upya kanuni hizi ili iweze kuimarisha *financial freedom* ya sekta hii ya AZAKI maana hivi sasa inakinzana na inafifisha juhudzi za sekta za AZAKI kuchangia katika maendeleo ya jamii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia napenda kumshukuru sana Waziri mwenye dhamana ya masuala ya maendeleo ya jamii kwa sababu mchango wangu kwenye bajeti ya Wizara hii niliombwa sana itusaidie ili ufanyike uchaguzi wa Baraza la *NGOs* la Taifa (*NACONGO*) ambalo liko ngazi ya Wilaya, Mikoa mpaka Taifa na hivi sasa uchaguzi huo unaendelea, kwa hiyo, napenda kumshukuru sana kwa kutusaidia katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, majuzi kwenye kikao chake na Baraza la Maaskofi wa Kikatoliki Tanzania alikumbushia kwamba yeze ni mwanaharakati na ni mwana-AZAKI pale ambako walipokuwa wanamtambulisha Askofu Kilaini. Kwa hiyo, na kwa kutumia hiyo hiyo napenda kuendelea kumwakikishia kwamba sekta ya Asasi za Kiraia tunamtambua kama mwana-AZAKI mwezetu na tunaahidi kuendelea kumpa ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza azma yake ya maendeleo ya jamii kwa Taifa letu na hakika tutafika pale ambapo anataka tufike kama Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana kwa fursa hii na nakubaliana na maoni ya kamati husika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, atakayetufungia shughuli yetu ya uchangiaji leo ni Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mbunge wa Mwanga na baada yake nitamuita mtoa hoja.

MHE. JOSEPH A. TADAYO: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kupata nafasi hii ya mwisho ya kufunga jamvi la uchangiaji. Awali ya yote niishukuru na kuipongeza sana Serikali kwa jinsi ambavyo imeendelea kuziongezea nguvu Mamlaka za Serikali za Mitaa na bajeti hii inashuhudia hayo, kwa hiyo, kwa hilo nipende kuwapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na kuongezea nguvu Serikali za Mitaa ni pamoja na suala hili la *by-laws* ambazo tunazzungumzia leo, kwa hiyo niwapongeze sana Kamati husika, wasilisho lao limekuwa zuri na ambalo nadhani pia limerahisisha uchangiaji wetu kwa siku hii ya leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni wazi kabisa kwamba taarifa ya Kamati imeonyesha umuhimu mkubwa sana wa kuziongezea uwezo mamlaka zinazohusika na utungaji wa hizi wa hizi *by-laws* na kwa sababu Mwanasheria Mkuu wa Serikali yupo hapa na amesikia na hili niseme kwa nidhamu kwa sababu

kwa taratibu zetu huyu ndiye wakili namba moja au msomi namba katika nchi, kwa hiyo, sisi wote tukimkuta huwa tunampisha kitu kwanza, naamini kwa vile yupo hapa na amesikia basi hiyo kazi itafanyika. Sheria ndogo ni muhimu siyo kwa uchumi wa nchi tu, lakini hata katika kulinda utulivu wa nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tatizo la sheria ndogo lipo kwenye kukinzana na sheria mama, lakini pia kupatikana kwa ule murua na sheria zingine zinazohusika, ile *harmonization*. Nitoe mfano, kwenye Jimbo langu la Mwanga sisi tunategemea sana mapato kwenye chanzo kimoja kinachoitwa madini ya ujenzi hasa mchanga. Ilitungwa ile Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga ya mwaka 2019 ambayo ilizipa halmashauri mamlaka ya kukusanya mauzo pamoja na ushuru kwenye hivi vyanzo vya madini haya ya ujenzi na hilo linaendelea kufanyika. Sasa hilo limefanyika bila kuangalia upande mwingine wa sheria ya madini ambapo Kamishna wa Madini anayo mamlaka ya kutoa hizi *primary mining licenses* kwa watu binafsi hata kwa mamlaka hata kwa vijiji.

Kwa hiyo, utakuta kweli Halmashauri ina mamlaka hayo chini ya *by-law*, lakini wapo watu ambao wanazo *primary mining licenses* kwenye maeneo yao. Kwa hiyo, hapo sasa kunakuwa na mgongano kwamba mimi nina leseni mbona wewe unakuja kukusanya hapa. Kwa hiyo, hilo linahitaji sana kutazamwa tusitazame tu zile sheria mama, lakini pia tutazame pia hizi sheria zingine ambazo zinahusika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, limesemwa vizuri hapa suala la rumbesa, kwa tatizo la rumbesa linatoka wapi! Tatizo la rumbesa linatokana na Sheria ya Vipimo (*Weights and Measures*), rafiki yangu, Mheshimiwa Shangazi atakubali kule kwake wanalima viazi sana, *by-laws* inasema rumbesa hapana, lakini ile Sheria ya Vipimo yenyewe inazungumzia juu ya uzito kwamba kilo 100 bila kujali imejaa mpaka wapi *as long as* ni kilo 100 imetimiza sheria. Sasa swali linakuja kwamba hivi gunia ni kipimo au ni kifungashio? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa hawa wengine sasa huko kwenye *barriers* sasa/kwenye vizuizi vya barabarani, ndio wanachukua sasa faida hapo wakifika hapo wanaweza kukubabaisha. Kwa sababu upande mmoja anaweza akasimama na *by-laws*, upande mwingine akasimama na Sheria ya Vipimo. Sasa wewe hapo katikati ndio unakuwa uko katikati ya nyundo na msumari unaendelea kuumia.

Mheshimiwa Spika, nikirudi nyuma kidogo ni kwamba hizi *by-laws* zinapotoa mamlaka fulani, lazima pia ziende kubana hizi Halmashauri kwenye suala la matumizi; kwa mfano kabla ya mwaka 2019 kwenye Jimbo langu vijiji vilikuwa vinakusanya mapato na ushuru wa mchanga kwenye vijiji kule, sasa ikachukuliwa na Halmashauri, lakini bado suala la kuzibana halmashauri kuhakikisha kwamba, ile asilimia 40 inarudi kwenye shughuli za maendeleo za maeneo husika yanayoonekana, sio tu tusikie sikie tu kwamba hapa sijui kuna gharama fulani ilitumika, *no.* vitu ambavyo vinaonekana na vitu *tangible* hilo bado halijafanyika vizuri. (*Makof!*)

Sasa hilo linaleta ile *resistance* kwamba watu wanaona kama vile wamenyang'anywa mapato yao, lakini kwa sababu hawaoni kile kinachorudi wazi. Kwa hiyo, nadhani nguvu inayotumika kwenye kukusanya, pia itumike katika kuhakikisha kwamba ule wajibu wa kurudisha yale mapato nyuma kwa wale wananchi unatekelezwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mimi kama mchangiaji wa mwisho siwezi kuwa na mengi sana ya kusema, labda tu nimalizie kwa kusema kwamba yapo mambo mengine ya kisera ambayo yanatakiwa yatangulie kwanza kabla ya *by-law*. Kwa mfano, tuna tatizo la kutenga maeneo ya malisho, ya mifugo na maeneo ya wakulima. Leo hii ukitunga *by-law* kabla ya sera ya matumizi bora ya ardhi ile *by-law* lazima italeta mgogoro tu. Kwa hiyo, zitangulie kwanza hizi sera husika ziweze kuititia katika michakato na zikubalike halafu, ndio twende kwenye *by-law* hapo zitatekelezwa vizuri. Suala la kutimiza sheria bila shuruti tutalionna kwa vizuri zaidi, kuliko sasa hivi ambapo inaonekana wakati mwingine kama ni vita

kati ya wananchi na mamlaka zetu husika. Vinginevyo kwa kweli mimi niendelee kushukuru kwamba hasa katika bajeti hii mamlaka hizi za Halmashauri zimepeewa nguvu ya kutosha. Kwa hiyo, sisi kama sehemu ya Mabaraza ya Madiwani tukitimiza wajibu wetu, nina hakika tutakwendwa vizuri na wananchi wataona faida ya ushuru na tozo mbalimbali ambazo wanalipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, tunakushukuru sana.

Sasa kabla ya mhitimishaji tumkaribishe Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali dakika kama tano. Mheshimiwa Waziri na yeye tano hivi, halafu mhitimishaji. Mheshimiwa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Profesa Kilangi, tafadhalii.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kidogo katika taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla kama ambavyo imekuwa ikitokea kila mwaka tunazipokea changamoto mbalimbali ambazo zimeainishwa na Kamati na kwa kweli tunawashukuru na kuwapongeza sana. Kama ambavyo wengi wa Waheshimiwa Wabunge wamezungumza hapa ndani, wanafanya kazi kubwa sana ya kufanya uchambuzi na hasa kwenda kwenye maudhui. Kwa sababu, sisi wakati mwingine tunaangalia tu yale masuala ya kiufundi ya kisheria, lakini masuala ya maudhui kwa kweli, Waheshimiwa Wabunge na Kamati wanaweza wakatusaidia sana katika eneo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kila wakati tunapokea mapendekezo hayo na maono hayo tunayachukua na tunayafanya kazi kila mwaka. Lakini pengine wengi watakulaliana nasi kwamba kadri tunavyokwenda hizi

changamoto zinazidi kupungua, ndio kusema kwamba, tunazifanya kazi changamoto ambazo zinakuwa zimekwishaelezwa kila wakati uchambuzi unapofanyika.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa ufupi tu zimeelezwa bado zile zile changamoto za sheria ndogo kupingana na sheria mama, kuna masuala ya kuweka tozo katika Kanuni au katika sheria ndogo, kuna masuala ya kutoshirikishwa wadau wakati wa utengenezaji wa sheria ndogo na pengine katika mazingira baadhi ya sheria hizi zinaonekana zinabeba labda maslahi binafsi.

Mheshimiwa Spika, sisi kama walivyosema Wabunge wengine tunaendelea kusisitiza kwamba misingi ya utengenezaji wa sheria ndogo ipo wazi na imeelezwa vizuri sana na tumeendelea kuieleza. Tunaomba kwamba misingi hiyo lendelee kufuatwa wakati wa utengenezaji wa hizi sheria ndogo na wakati wowote misingi hii isiachwe.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna jambo nilipenda niliseme hapa, sheria nyingi zinazolalamikiwa ni sheria ndogo zilizotungwa na Halmashauri zetu. Sasa katika Halmashauri zetu Waheshimiwa Madiwani ndio wanahusika, lakini pia Waheshimiwa Wabunge pia ni Wajumbe katika Mabaraza hayo. Nilikuwa napenda kutoa wito kwamba ningewaomba sana Waheshimiwa Wabunge, wachukue muda wa kutosha waangalie hizo sheria zinazopendekezwa katika Halmashauri hizo na kuona kama baadhi ya changamoto hizi ambazo zinalalamikiwa zipo na basi zifanyiwe kazi katika ngazi hiyo. Tukifanya hivyo na Wabunge wote wakitimiza wajibu wao tutakuwa tumepunguza sana changamoto nyingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto za kiuandishi tumekuwa tunaendelea kuzungumza kwamba tuna zoezi na ambalo ni endelevu la kuwapatia uwezo wanasheria wetu waliopo maeneo mbalimbali kwenye Halmashauri, kwenye Taasisi, kwenye Wizara, uwezo wa kuweza kufanya hiyo kazi ya uandishi wa sheria katika weledi unaotakiwa. Hata hivyo, kama ambavyo tumekiri na imeelezwa na watu wengi taaluma ya uandishi wa sheria sio jambo rahisi. Kwa hiyo,

pengine hutegemei sana kwamba, kwa semina ya wiki moja utaweza kuwafanya watu wawe na umahiri kama alionao Mwandishi Mkuu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Iakini vinginevyo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ipo tayari wakati wote na tunatoa msaada wakati wowote tunapotakiwa kuweza kuboresha hizi sheria ndogo.

Mheshimiwa Spika, kwa mchango huo, naomba kuwasilisha na nakushukuru sana kwa nafasi. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Profesa Kilangi. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa, Jenista Mhagama.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, KAZI, BUNGE, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, na mimi kwanza nianze kwa kukushukuru sana kwa kuipa nafasi Serikali, ukianza na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Iakini na mimi pia kwa niaba ya Serikali kuweza kupata fursa ya kutoa mchango kidogo, kuhusu hoja hii ambayo umeiweka leo mbele ya Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Kwanza kabisa nadhani tutakubaliana Waheshimiwa Wabunge wote tuchukue nafasi nyingine ya pekee kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kutimiza siku 100 za utendaji wa kazi akiwa ameonesha historia ya kufanya vizuri ndani ya siku 100 za utendaji wake wa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Iakini ninaposimama hapa majukumu mengine niliyopewa kwenye Hati Idhini ambayo inanipa kazi hii ya kuwa *Chief Whip* ndani ya Bunge ni kuwa kama mchezaji kiungo katika Serikali na Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba tu niseme kwamba mafanikio haya ambayo tunayapata ndani ya Serikali, hatuwezi kusema pia hayajachagizwa na wewe mwenyewe Spika na Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais,

Iakini tuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kuishauri Serikali katika masuala mbalimbali na hatimaye kufanya Serikali iweze kutekeleza wajibu wake sawasawa na kwa kweli tuweze kusimamia masuala mbalimbali ya uendeshaji wa Serikali wa siku kwa siku. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hoja iliyopo hapa mbele yetu imeletwa na Kamati ya Bunge lako Tukufu, Kamati ya Sheria Ndogo inayoongozwa na Dkt. Rweikiza akisaidiwa na Ndugu yangu Dkt. Ridhiwani Kikwete. *Inshallah* na wewe siku chache zijazo nadhani mambo yatakuwa sawasawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli niwapongeze sana viongozi hawa wawili wa Kamati ya Sheria Ndogo, pamoja na wajumbe kwa kazi kubwa wanayoifanya. Umesema hapa na umewasilka Wajumbe waliposimama hapa mbele, kila mmoja mjumbe aliyechangia alikuwa anasema wakati anateuliwa kwenye Kamati hii alikuwa haelewi hii Kamati maudhui yake na utendaji wake wa kazi, Iakini alipoingia ndani ya Kamati ndio aliona umuhimu wa Kamati hii ndani ya Bunge, Iakini umuhimu wa Kamati hii katika kusimamia haki za Kikatiba za wananchi wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba niungane na Kamati na kazi nzuri inayofanywa na Kamati na niseme kwa kweli kama tunahesabu Kamati ambazo ni muhimu kwa utendaji kazi wa kila siku wa Serikali, Iakini mapokeo yake kwa wananchi Kamati hii inayoshughulikia sheria ndogo pia ni Kamati muhimu na inafanya kazi nzuri sana. (*Makof*)

Mheshimiaw Spika, ninasema hivyo kwa nini, kwa sababu, kifungu cha 38(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, ikienda sambamba na kifungu cha 43(2) cha Kanuni za Bunge kinatuagiza sisi Serikali kuweka mezani nakala ya Magazeti ya Sheria Ndogo zote zilizotungwa kwa mujibu wa Katiba. Ili Bunge lenye majukumu ya kutunga sheria litutizame sisi Serikali na watendaji wote ndani ya Serikali, kama tunayatumia madaraka hayo vizuri na Bunge liweze kuturekebisha pale ambapo hatutendi haki kwa niaba ya Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kazi hii tumekuwa tukiifanya na Waheshimiwa Wabunge mmeniona nikiweka hayo magazeti hapa mezani. Bunge lako la Kumi na Moja liliweza kufanya kazi ya kupitia sheria hizi ndogo takribani 2,601 na sheria 547 zilifanyiwa kazi na kukutwa na dosari na ikatupasa Serikali turudi tukajipange upya na kufanya mabadiliko kwenye sheria hizo kwa ustawi wa Watanzania. (*Makof*)

Kwa hiyo, nataka kuyasema haya tuone Bunge hili liliivo na nafasi nzuri na nakumbuka Kamati ile iliyopita, ilifanya kazi nzuri wakina Mheshimiwa Mdee na Mheshimiwa Chenge akiwa Mwenyekiti, ilikuwa kweli ukienda kwenye Kamati ya Sheria Ndogo unaona unakwenda kukutana na miamba na sasa hivi, unapowakuta kina Ridhiwani na kina Dkt. Rweikiza, unajua kabisa ile Kamati inaenda kufanya kazi yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, na mimi ninapokwenda kule huwa ninajiandaa kweli kweli kwa sababu hakuna mchezo unatakiwa ukatoe maelezo fasaha. Bunge lako hili kwa siku hizi 100 limeweza kupitia Sheria Ndogo 915, kwenye hii Kamati ya Sheria Ndogo na imegundua dosari 119 kwenye sheria 23. (*Makof*)

Ninaomba nitoe ahadi mbele yako; kwanza, tutaendelea kuyaheshimu mamlaka ya Kikatiba ya Bunge katika udhibiti wa sheria hizi ndogo zifanane na matakwa ya sheria mama ambazo zimekuwa zikitungwa na Bunge lako Tukufu. Kwa niaba ya Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Serikali nzima kwa ujumla tutaendelea kuheshimu jukumu hili la kikatiba mlilopewa Wabunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, Wizara yangu inasimamia masuala ya sera, tutajitahidi kuhakikisha Sheria ndogo, sheria mama zinaendana na sera zilizotungwa ili ziweze kwenda sambamba na ziweze kutekelezeka vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini tuna maazimio hapa kama manne ambayo yameletwa na Kamati hii ya Sheria Ndogo, yanatutaka Serikali tukayafanyie kazi. Ninaomba nikuhakikishie Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ina jukumu la

kuratibu shughuli za Serikali Bungeni, tutahakikisha kila Wizara na kila Taasisi, ambayo imepewa maelekezo ya kufanya maboresho na marekebisho ya sheria hizi, tutakwenda kuyafanya kazi na tatarudi kutoa taarifa ndani ya Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la mwisho Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesema ndani ya Serikali tumeamua kujipanga, yapo mambo ambayo tutayafanya ilkiwa ni pamoja na kufanya *training* ya kutosha kwa wanasheria wetu kwenye *level* mbalimbali, lakini kufanya uunganishaji kwa sababu ni lazima sheria hizi zizungumze katika Taasisi moja, Wizara moja, Wizara nyingine, Halmashauri, sheria hizi ziweze kuzungumza. Tumeona hapa tafsiri ya sheria moja kwenye taasisi nyingine na taasisi nyingine zitatofautiana, lakini lengo ni moja.

Kwa hiyo, mapungufu ya namna hii kwa kweli kwa mikono miwili tunayachukua na tunaahidi kwamba tutakwenda kuyafanya kazi lengo letu mwisho wa siku tuweze kufanya vizuri. Ufanyaji vizuri wa sheria ndio utendaji wa haki kwa watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaunga mkono kabisa hoja ya Kamati na kama Serikali, tunachukua wajibu wetu wa kwenda kuyatekeleza yale yote ambayo yamewekwa kwenye maazimio haya ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, na ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, tunakushukuru sana kwa mchango wako. (*Makofii*)

Sasa nimuite mtoa hoja, uje uhitimishe hoja yako. Ahsante sana, dakika zisizozidi 20. (*Makofii*)

MHE. RIDHIWANI J. M. KIKWETE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:
Mheshimiwa Spika wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania, Waheshimiwa sana Mawaziri, Wabunge wenzangu, wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana na mimi kwanza nianze kwa kushukuru kwa sababu mwanzo nilikuwa natoa salamu za jumla za Kamati, lakini sasa nimepata nafasi ya kutoa maazimio au majumuisho, naomba nikushukuru wewe binafsi kama walivyotangulia wenzangu kusema, kwa kunipa nafasi na mimi kuwa mmoja kati ya Wajumbe wa Kamati hii ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, kwa hakika sio tu kwamba, nimeendelea kujifunza kama mwanasheria, lakini pia imenipa nafasi ya kuendelea kujuu Tanzania na sheria ambazo zinaendelea kuhitaji marekebisho au uangalizi wa karibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hilo pia natambua kwamba michango iliyotolewa na Wabunge mbalimbali, Wabunge 14; lakini pamoja na hao pia ameongea Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulika na Sera, Vijana na Walemaru ameeleza naye katika hayo mambo yake. Lakini pamoja na hilo pia, niishukuru Serikali kwa kukubali kuchukua yale yote yaliyopendekezwa na Kamati yetu na kwenda kuyafanya kazi. Lakini kwa umuhimu zaidi niwashukuru pia wachangiaji wote, kwa michango yao mizuri iliyolenga kuboresha taarifa yetu na kuifanya taarifa hii sasa iwe taarifa ya Kibunge, iwe na sifa za kuitwa taarifa ya Kibunge, lakini pia iwe taarifa ambayo inatosha katika maudhui yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mambo ambayo yameelezwa na mimi napenda niyasisitizie ambayo kwangu kama mtoa hoja, ni vyema nikayapazia sauti ili Serikali iweze kuyachukua katika uzito wake.

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa ambalo tumelizungumza ndani ya Kamati, lakini pia kutoka kwenye michango ya wajumbe wa Bunge lako, ni juu ya huu mtazamo ambao upo wa baadhi ya watu kutunga Sheria, ambazo zimekuwa kandamizi sana. Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa *Attorney General* ni ukweli kwamba haya mnaenda kuyafanya kazi, lakini kiukweli sheria zetu bado

haziendelei kufurahisha watu wengi na hivyo kwenu ninyi kuchukua na kwenda kuyafanya kazi ni jambo la msingi sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, yameibuka hoja hapa ya ile ya bajaji ya kutozwa mpaka shilingi 200,000 kwa faini, kwa ajili ya *wrong parking*. Mheshimiwa Waziri mhusika ningeomba utoe maelekezo kwa Halmashauri zako na ikiwezekana utaratibu mzuri uwekwe, ikiwezekana kwamba sheria hizi kabla hazijaanza kufanya kazi basi Bunge hili liweze kuzipitia. Tofauti na sasa ambazo zinafanya kazi kwanza halafu baadaye, ndio Bunge linakuja kuziangalia kama zimefuata utaratibu au hazijafuata utaratibu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia limezungumzwa jambo hapa la vijana kuwa wanaminywa katika ajira. Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa *Attorney General*, ndugu Wabunge wenzangu, jambo la ajira limekuwa ni kilio kikubwa cha muda mrefu, kama sisi Wabunge hatutakisimamia hiki katika ile dhana ambayo, Rais wetu mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan anataka vijana wapate ajira, sio tu katika zile ajira zilizo rasmi zinazotangazwa Serikali, lakini pia katika mazingira wanayoishi hatuteweza kufanikiwa kama jambo hili halitoangaliwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini naishukuru Serikali imesema jambo hili inalichukua na kwenda kulifanya kazi ili liweze kuwa jambo ambalo linakwenda kutatua kero hizi. Lakini hili liende sanjari na lile jambo la ile Sheria ya Filamu ambayo nayo imelalamikiwa sana na wajumbe wengi wameipazia sauti ili kuweza kuweka sawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini ipo sheria nyingine ambayo imeonekana kwamba ni inaweza ikasababisha shughuli za kihalmashauri zisifanyike vizuri. Hiyo sheria inatambulika kama Sheria ya Kukusanya Ushuru ambayo sisi kwenye taarifa yetu tulionesha hiyo taarifa ya Same, lakini ndugu au Msomi Mheshimiwa Tadayo akaelezea juu ya pia taarifa nyingine inayofanana na hiyo ya kule Mwanga.

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali iliangalie jambo hili vizuri, tukifanya mchezo Halmashauri zetu zitakosa vyanzo vya mapato na kwa kukosa mapato huko kutapelekea shughuli zetu baadhi yao zikwame. Sisi leo ndani ya Chalinze kwa mfano, moja ya chanzo chetu kikubwa ni mapato yanayotokana na kokoto. Kama ukitunga Ssheria ukasahau chanzo hiki cha mapato maana yake ni kwamba Halmashauri ya Chalinze itaingia katika mgogoro mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, jambo la kufundisha wataalam wetu ili wawe waandishi wazuri hili ni jambo ambalo lazima lipangiwe mkakati ili liwe jambo endelevu lakini liweze kusaidia halmashauri zetu kuweka mikakati vizuri na waandishi wetu waweze kuwa wamejengewa weledi ulio mzuri.

Mheshimiwa Spika, nimezungumzwa jambo linge hapa la watunzi au waandishi wa sheria kutozingatia misingi ya Katiba. Katika jambo lilito muhimu ambalo sisi pamoja na wewe Spika wetu, tuliliahidhi mbele ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni ulinzi wa Katiba yetu. Bila kulinda Katiba sisi ambao ndio watunzi wa sheria hizo tutakuwa ndio kituko na kichekesho cha kwanza katika nchi hii. Tusikubali Bunge lako ligeuzwe kuwa sehemu ya kuponda na kuvunja Katiba hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hilo pia kuendelea kukumbushana Wabunge wenzangu ambao pia ni Madiwani kwamba tusiache mambo yakaendelea kule kwenye Halmashauri zetu bila sisi kushirikishwa. Maana yapo mambo mengine haya tunaweza kuyamaliza kule majimboni kwetu au kwenye maeneo yetu kwa sisi kufuatilia mara kwa mara. Kitendo cha sisi kukaa huku Bungeni kisiwe kisingizio cha kuitishwa kwa mambo ndani ya halmashauri zetu bila kushirikishwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hilo pia nikushukuru Mheshimiwa spika kwa maelekezo yako uliyoyatoa na hadithi uliyotupa hapa ya kweli juu ya wale vijana ambao wamejajiri wenyewe na tabu wanayoipata, kwangu mimi hili sio tu kwamba ni maelekezo labda kwa

Kamati au kwa Serikali lakini pia kwetu sisi sote kama Wabunge tujaribu kusimamia sheria hizi ili kutatua kero hizi ambazo zinakwenda kukabili vijana wenzetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo la rumbesa limezungumzwa hapa, hili jambo nadhani kwa yale maeneo au Halmashauri ambazo zina sheria hizi hebu tuziangalie tena vizuri ili tuweze kuweka mambo yetu vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho katika michango hii, nizungumzie mchango mzuri uliochangiwa na Mbunge Ndugu Neema Lugangira juu ya Asasi zisizo Kiserikali na zile ambazo zinafanya kazi katika jamii yetu. Kamati imesikia juu ya matatizo makubwa yaliyopo katika Kanuni hizi zinazokabili *NGOs* na *CSoS* kwangu mimi kwa kuwa mamlaka ya kuita kanuni hizi unayo wewe na Kamati yako imeendelea kufanya kazi kwa maagizo yako, tukuombe kupitia Kanuni yako, kupitia Katiba inayokupa nguvu wewe, uielekeze Serikali ituletee Kanuni hizo na sisi kama Kamati tupo tayari kwa ajili ya kuziangalia ili *NGOs*, *CSoS*na Asasi nyingine ziende kufanya kazi katika utaratibu tuliokulaliana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hilo pia niwaambie tu ndugu zagu wa *NGOs* na *CSoS* kwamba kuja kwa kanuni hizo sio kwamba tunapata tiketi ya uvunjivu wa kanuni, hapana. Kamati itaangalia vizuri na kujiridhisha juu ya yale ambayo yanalamikiwa na baada ya kujiridhisha mapendekezo yetu yatakuja hapa katika Bunge ili ninyi Bunge muweze kuamua katika haya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, umeniambia kwamba unanipa dakika 20; lakini dadika 20 katika maana ya kufunga hoja kwangu mimi ni nyingi sana. Ningependa kutumia nafasi hii ya mwisho; kwanza kumshukuru kabisa Rais wetu mpandwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya, kazi ambayo kwa hakika inaigwa katika dunia nzima. (*Makof*)

Tumeshuhudia ndani ya siku zake 100 kupitia hotuba ya Waziri Mkuu aliyoisema jana pale Dar es Salaam, akieleza

kwamba Mama Samia amekwisha fanya na kuendelea kukamilisha miradi zaidi ya 73 ambayo inafanywa kwa fedha za ndani na nyingine kutoka katika fedha za wahisani ambayo inaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hilo pia tumeshuhudia Mama Samia Suluhu Hassan katika akitimiza kwa vitendo nia yake nzuri ya kuhakikisha kwamba mazingira mazuri ya biashara yanaendelea kuimarika katika nchi yetu. Amefanya vikao zaidi ya viwili, akishirikiana na Waziri Mkuu na Makamu wetu wa Rais na Mawaziri wetu na tumeshuhudia nia yao nzuri ikianza kwa vitendo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hilo pia nimpongeze sana Mama yetu Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hakika ameanza vizuri sana kazi yake ya kutimiza ndoto za Watanzania. Sisi kama Kamati ya Sheria Ndogo au sisi kama Wabunge tunaendelea kumuunga mkono na niwaombe Wabunge wenzangu tuendelee kumuunga mkono mama yetu akitimiza nia nzuri ya kuhakikisha kwamba nchi yetu inakwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo mwisho kwa umuhimu wake, niishukuru pia familia yangu; katika kipindi cha miezi miwili/mitatu ambayo tumekaa Bungeni hapa, tumekuwa mbali na familia lakini wanangu wamekuwa wanani pigia simu wakinishukuru, wakinipa moyo na kunifariji, mke wangu amekuwa anafanya hivyo na kwangu mimi imekuwa ni faraja kubwa sana hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hilo pia leo asubuhi umewatambulisha rafiki zangu wawili; nisingependa jambo hili nichukue muda sana lakini kwa upekee uniruhusu nifanye hivyo; amekuja rafiki yangu mmoja hapa anaitwa Azizi. Azizi kwa taaluma yake yeye kinyozi, ni mtu ambaye ukimuona utamuona ni mtu mdogo sana, lakini Azizi ndiye ambaye anafanya mimi na wenzangu wengine tunapendeza na kuonekana hivi tulivyo. (*Makofii*)

Amekuja hapa nimemualika na ni mgeni wangu, nataka mjue ndugu zangu Wabunge wenzangu kwamba kuna umuhimu wa kwamba *chamber* hii kama alivyozungumza Mheshimiwa Spika ikawa *chamber* ya kila mtu. Siyo tualike tu wale wapiga kura wetu wa Katibu, Wenyeviti, Madiwani hapana na watu wengine ambao wanafanya Maisha yetu yanakwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hilo pia yupo rafiki yangu Dkt. Mwinyi; Dkt. Mwinyi amekuwa ananisaidia sana, mimi kama alivyozungumza mama yangu Waziri Jenista Mhagama mimi bado nasoma pia, nipo *UDOM* hapo nasoma na ile ndoto ya Mama Jenista Mhagama huenda siku moja ikawa kweli na mimi nikawa Daktari. (*Makofi*)

Nakushukuru na ninaamini kabisa maneno yako hayawezi kuanguka na amekuwa msaada mkubwa sana Dkt. Mwinyi akinisaidia kuhakikisha kwamba na mimi natimiza ndoto za kuwa Daktari siku moja, lakini kuwa katika jamii ya vijana ambao ni wasomi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa maana siasa tuna mwisho kabisa, tuna mwisho kwa umuhimu kwa umuhimu wake; mwisho kabisa niendelee kukushukuru wewe kwa kunipa ruksa hii. Umenipa nafasi kubwa ya kuhudumia katika Kamati hii na mimi binafsi yangu namshukuru tena Mwenyezekiti wangu Dkt. Rwekiza kwa nafasi kubwa aliyonipa ya kuja kusoma mbele yako, lakini pia ruksa hii inatupa nafasi na sisi ya kutokuwa na woga tunaposimama mbele yako. Maana hapa panatisha, lakini kwa kipekee nikushukuru wewe pamoja na Wabunge wenzangu tuendelee kupeana ushirikiano. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Makamu Mwenyezekiti wa Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo kwa kuhitimisha vizuri sana hoja yako. (*Makofi*)

Nakupongeza wewe na Wanakamati wenzako, Mwenyezekiti wako kwa kazi nzuri ambayo mnaendelea kuwa mnaifanya na sisi tunaendelea kuwaaminia katika kazi hiyo

ngumu. Tofauti ya Kamati hii na Kamati nyingine ni kwamba hii Kamati ya kukaa chini na *ku-scrutinize*, kupitia vitu. Hii Kamati haina safari, haina nini enhee na wala hawanisumbui. (*Kicheko*)

Katika Kamati baridi, safi kabisa Kamati ya Sheria Ndogo, naomba muwapigie makofi jamani. (*Makofi*)

Nawashukuruni sana. Sasa tumalizie wageni kama nilivyosema kwa kweli tunapata wageni wengi na ni jambo jema. (*Makofi/Kicheko*)

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani kutoka Chato, Ndugu Danford Biyagosha na Ndugu Stephen Kinsabi, kama wapo wengine wanaweza wakawa wametoka asubuhi.

Wageni 20 wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ni wanafunzi wa *UDOM* wanaotoka Moshi wakiongozwa na Ndugu Juma Omari baadhi yao inaweza ikajirudia wale pale, ndiyo ahsante sana na karibuni sana, kutoka Moshi hao. (*Makofi*)

Wageni 29 toka wa Mheshimiwa Michael Kembaki ambao ni walimu wa Shule ya Msingi *Ghati Memorial* toka Tarime Mkoani Mara wakiongozwa na Ndugu Fadhira Stephen. *Ghati Memorial* enhee karibuni sana, karibuni sana, karibuni sana, ndugu zetu kutoka Tarime. (*Makofi*)

Wageni 20 wa Mheshimiwa Shaashisha Mafuwe ambao ni wanafunzi wa *UDOM* kutoka Hai, karibuni sana, karibuni sana, sana. (*Makofi*)

Wageni 45 wa Mheshimiwa Justine Nyamoga ambao ni kwaya ya Kanisa KKKT Image, Iringa wakiongozwa na Saidi Kiyeue ambaye ni Diwani. Ohooo, karibuni sana Image kutoka kule Iringa. (*Makofi*)

Kwa wale ambao hawakuona Mheshimiwa Ridhiwani wakati anahitimisha hapa alitoa hoja na iliungwa mkono

tangu wakati ule mwanzoni kwa hiyo baadaye nitaiamulia hoja yake. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Oscar Kikoyo na Mheshimiwa Charles Mwijage ambao ni wanafunzi wa *UDOM* wakiongozwa na Ndugu Melkizedek Kaijage, enheeee nafikiri walikuwepo asubuhi hao.

Mgeni wa Mheshimiwa Bahati Ndingo kutoka Mbeya ambaye Ndugu David Mwangaba, ahsante yule pale. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Mwasi Kamani ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana kutoka Mkoa wa Mwanza, Ndugu Jonas Mwiuhula, karibu Jonas.

Wageni sita wa Mheshimiwa Asia Halamga ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, wakiongozwa na Ndugu Aneth Charles, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni sita kutoka Shirika la Ndege Tanzania (*ATCL*) wakiongozwa na Meneja wa *ATCL* Dodoma, Ndugu Mohamed Ngamanya. Ooh, *ATCL* karibuni sana, karibuni sana sana Shirika letu la Ndege, watoto wapendwa ninyi. (*Makofi*)

Wageni 41 na walimu wawili kutoka Shule ya Al-Kaeem Seminari hapa Dodoma, wanafunzi wa Al-Kaeem hongereni sana na karibuni sana, sana sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

Wale wapanda mlima wetu sijui kama bado wapo, *actually* ni wawili kuna Rawan Dakik ambaye ni mwanamke aliyepanda mlima mwaka 2021 ambaye nilimtambulisha mwanzoni amesimama enheeee! Enheeee yule pale. (*Makofi*)

Waheshimiwa makofi haya hayatoshi jamani enheeee Mlima Everest siyo masihara; enheeee naona ndio maana anenepi aisee. Enhee, kupanda Mlima Everest siyo mchezo katika wanawake. (*Makofi*)

Sasa yuko katika wanaume Wilfred Mushi ambaye alipanda mwaka 2012. Ahsanteni sana, hawa ni wageni wa Naibu Waziri, Maliasili na Utalii, karibuni sana. (*Makof*)

Lakini pia nina tangazo la Mheshimiwa Najma Giga, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria anaomba Wajumbe wake wa Katiba na Sheria na wale tuliovateua juzi kukutana pale Ukumbi wa Msekwa D, ili waweze kupangilia mambo yao ya namna ya kuititia yale marekebisho ya sheria mbalimbali yaliyoletwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Tarimba asubuhi tuliwapongeza mlioteuliwa kuwa Wadhamini wa Klabu ya Yanga, maana yake mmetuliwa wazito watupu kwa Mheshimiwa Tarimba anapeleka *Sports Pesa* yote huko; yupo Mheshimiwa Kepteni George Mkuchika, Ofisi ya Rais, yupo Mheshimiwa Geoffrey Mwambe yeye Uwekezaji, uwekezaji wote na nini na masuala ya uwekezaji kwenye Yanga huko sasa yapo nyumbani, lakini Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba sasa Wizara ya Fedha nzima.

Kwa hiyo, tunawapongeza sana Wabunge wetu kuaminiwa kwa kweli. (*Makof*)

Lakini jambo moja nataka niwaambie, mmeamua kuiga ni jambo jema unajua kuiga kuzuri na siyo jambo baya, kuwa katika klabu ya kisasa ya uendeshaji siyo kutembeza bakuli bakuli na nini; enhee sasa mnakuja kwenye mfumo wa uendeshaji wa kisasa wa kampuni na kadhalika, kwa hiyo, mtauza hisa.

Katika hisa zile nawaomba Wanayanga wazinunue kwa wingi ili klabu yao iweze kwenye kadri walivyojipangia, kwa sababu mpira ukikua ni mpira wa Tanzania, ila wakizubaa kuzinunua sisi tutahamasisha Wabunge Wanasingha tuzinunue hizo hisa, kwa wingi halafu kwenye Bodi yao tutapeleka mjumbe sasa mle, maana si hawakununua hisa. Nafikiri Mjumbe wetu anaweza akawa Msemaji Mkuu Haji Manara akawa Mjumbe kwenye Bodi ya Yanga, maana yake tutakuwa na Hisa nyngi nhahaaa. (*Makof/Kicheko*)

Kwa kusia hilo Wanayanga ili wazue hilo inabidi wanunue Hisa nyngi sana za klubu yao. Tunashukuru jamani michezo inasaidia katika Nchi yetu ya kutuweka Pamoja, tunataniana siku zinakwenda. Lakini juzi wale mliongania mpira wa *Kaizer Chiefs* na wale nini sijui Casablanca Wydad wale, aaah, utaona yaani tungevuka pale kumbe tungefika finali aisee. (*Makof!*)

Kwa hiyo mpiri wetu Tanzania ni mkubwa jamani, tuendelee kuimarisha, na tuache visingizio; Mheshimiwa Tarimba visingizio oooh viwanja nini; halafu mkifungwa mnasingizia *TFF*. Sasa kama tatizo ni kiwanja *TFF* finalaumiwa nini? (*Makof!/Kicheko*)

Ndugu zangu baada ya mazungumzo hayo baada ya habari basi niwashukuru sana muda wetu kama mtakavyoona umefika mahali pale ambapo tullenga tangu mwanzo. Tunashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu amerudi sasa tupo naye. Naamini kabisa anajiandaa kwa ajili ya kesho kutwa, ili kuja kuhitimisha hapa mchana wa kesho kutwa. (*Makof!*)

Lakini sasa hii hoja ya Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na Kamati yake ni lazima ihitimishwe hii na katika kuhitimisha ni kwamba ningependa kuwahoji Bunge kama mnaikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano huu wa Tatoo wa Bunge.

(Hoja ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo illafikiwa na Bunge)

SPIKA: Wote kabisa wameafiki Taarifa ya Kamati. (*Makof!*)

Nashukuru sana Kamati tumeshasema muendeleee tena awamu ijayo; tutapata Taarifa ya Kamati ya pili ndani ya mwaka huu wa fedha yaani ya kwanza katika mwaka wa fedha ujao. Na Kamati nyngine mjiandae pia wakati

muafaka utakapofika tunatarajia kupokea taarifa zenu za utendaji kazi na natumaini mnaendelea vizuri.

Kwa jinsi hiyo basi, kwa kuwa shughuli za leo zilizopangwa zimekamilika basi naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi. (*Makofi*)

*(Saa 07:00 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne,
Tarehe 29 Juni, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*